**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 6 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaingia katika kipindi cha Maswali Majibu, ninalo tangazo moja tu. Naomba muwatambue wageni wa Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mbunge wa Mbeya Vijijini ambao ni Madiwani 23 na Maafisa wa Wilaya watano kutoka Mbeya Vijijini. Wapo sehemu hii ya kulia pale, naomba wasimame Waheshimiwa Madiwani. Ohoo hawajafika. Basi tunatambua kwamba labda bado wako njiani. Ahsante. *(Makofi)*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 157

**Barabara ya Mkendo/Shabani**

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Mukendo/Shabani ni kioo cha Manispaa ya Musoma, na kwa kuwa barabara hiyo ni ya muda mrefu na lami yake imeharibika sana; na kwa kuwa, mwaka jana Serikali iliahidi kuikarabati barabara hiyo kuanzia Januari, mwaka 2006:-

Je, ukarabati wa barabara hiyo utaaanza lini na kukamilika baada ya muda gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vedastusi Mathayo, Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilikwishaagiza Miji yote iliyopandishwa hadhi kuwa Manispaa kuandaa makisio kati ya urefu wa kilomita 3 hadi 4 za barabara kwa ajili ya kuandaa mpango wa ukarabati. Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ni kati ya Manispaa zilizokwishawasiliana makisio hayo.

Aidha, katika mpango uliowasilishwa Halmashauri imepanga kukarabati barabara za Mkendo, Shabani, Sokoni, Kusaga na Indira Ganthi kwa kiwango cha lami zenye jumla ya urefu wa kilomita 4.8 kati ya barabara zake zote zenye urefu wa kilomita 14.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mkendo/Shabani yenye urefu wa kilomita 3.8 iko kwenye mpango wa ukarabati ambao unakisiwa kugharimu shilingi bilioni 1, 630,769,500/=. Mpango huu utaanza kwa awamu ya kutegemea fedha za Mfuko wa Barabara. Halmashauri za Manispaa mpya zinazotakiwa kuleta mipango ya ukarabati wa barabara kwa kiwango cha lami ni Musoma, Sumbawanga, Kigoma, Singida, Bukoba, Mtwara na Songea. Zoezi hili litakapokamilika Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI itaandaa mpango makini wa kuanza kutekeleza kwa awamu angalau hata kwa kilomita moja moja kwa Manispaa hadi kutimiza kilomita zote. Na hii itaanza rasmi mwaka wa fedha 2007/2008.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi niweze kuuliza swali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, pamoja na kwamba barabara hizi zinashughulikiwa na Halmashauri za Manispaa. Lakini *specific* kwenye hii barabara ya Mkendo ilikuwa ni ahadi iliyotolewa mwaka jana na Mheshimiwa Waziri husika. Kwa jinsi barabara hiyo ilivyokuwa imeharibika Serikali ingeanza kuishughulikia kuanzia mwezi Januari, mwaka huu. Kwa hiyo, ninachotaka kujua je, huo mpango wa Serikali Kuu kuishughulikia hiyo barabara upo au umeisha. *(Makofi)*

La pili, Lakini kwa kuwa sasa inaonekana hizi fedha ambazo zinaenda kwenye *Local Government* kwa ajili ya utengenezaji wa barabara zinakuwa ni fedha ambazo siku zote hazitoshi. Hivi Serikali haioni kama kuna haja sasa kazi ya barabara zote iweze kuachiwa Serikali Kuu ili iweze kuzishughulikia kuliko kugawana hiki kipato kidogo kilichopo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza la ahadi ya Waziri wa Ujenzi wakati ule ni kweli aliahidi kwamba watatengeneza barabara hiyo. Ni ahadi ya Serikali siyo ahadi ya mtu binafsi. Kwa hiyo, sisi tunaahidi kwamba tutatekeleza ama Serikali za Mitaa. Lakini tutatekeleza kwa awamu kulingana na fedha ambazo zinapatikana kutokana na Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe Waheshimiwa Wabunge, kwamba mmepitisha fedha za Mfuko wa Barabara bilioni 25 tu kwa ajili ya barabara zote za Halmashauri na ni asilimia 10 ambayo itaingia kwenye Manispaa zote. Kwa hiyo, fedha hizo ni kama

alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba ni chache. Kwa hiyo, tutatekeleza kwa awamu.

Kuhusu swali la pili, kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu kwamba suala hili linaangaliwa, kuangalia kwamba je, ni asilimia ngapi aidha iongezwe au ipunguzwe katika Barabara za Serikali za Mitaa.

Na. 158

**Uhaba wa Maeneo ya Makaburi**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Manispaa za Dar es Salaam zinaonekana kutotosha wakati wowote katika suala zima la mahali pa kuzikia (makaburi):-

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuandaa eneo jingine kubwa kwa maandalizi muhimu kwa ajili ya mazishi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Jimbo la Mfenesini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa baadhi ya maeneo ya mazishi ya watu yameanza kujaa katika Manispaa za Dar es Salaam. Hata hivyo Manispaa za Kinondoni, Ilala na Temeke, zimetenga maeneo mpya kwa ajili ya makaburi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji kama ifuatavyo:-

- Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imetenga maeneo sita maeneo hayo ni pamoja *Tegeta Block F, Bunju,* Mbweni Mpiji, Mbweni JKT na Mivumoni ambalo lina jumla ya hekta 72.5.

- Halmashauri ya Manispaa ya Ilala imetenga maeneo manne ambayo ni Kibaga, Kitunda, Buyuni na Mwanagati ambalo lina jumla ya hekta 6.8.

- Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imetenga maeneo tisa ambayo ni Tua Ngoma, Vijibweni, Kisota, Kigamboni, Tanita, Chamazi, Buza, Mtoni Kijichi na Gezaulole lenye jumla ya hekta 5.

Mheshimiwa Spika, maeneo yote yamepimwa na mengi hayajaanza kutumika, kutokana na kuwepo kwa makaburi ya wenyeji ambayo bado yanatumika. Kwa mfano, Manispaa ya Ilala ina maeneo 28, Kinondoni ina maeneo 79 na Temeke ina maeneo 17.

Aidha, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hali ya maeneo ya makaburi bado ni ya kuridhisha katika Jijini Dar es Salaam.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri. Kwa kuwa sehemu kubwa ya makaburi hasa ya Kinondoni yapo karibu kabisa na barabara kuu. Hivyo, kupelekea wakati mwingine magari makubwa kuyakanyaga. Je, Serikali inaweza kufanya utaratibu wa kuyahifadhi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, wazo lake tumelipokea na tutaenda kulifanyia kazi. Kwa sababu sijalifanyia utafiti. *(Makofi)*

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa kwenye majibu ya msingi imeelezwa kwamba kuna maeneo hivi sasa bado hayajaanza kutumika hayo mapya kutokana na kuwepo kwa makaburi ya wenyeji. Kwa vile sasa Serikali ina mpango wa kuendeleza Mji hasa Jimbo la Kigamboni. Je, hayo makaburi ya wenyeji ya asili yatahifadhiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, sehemu hizo ambazo ni za makaburi ya asili Serikali itaangalia na kulifanyia kazi. Kwa sababu mengi hayajachunguzwa mpaka sasa hivi.

Na. 159

**Rushwa katika Vyuo vya Elimu ya Juu**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR (K.n.y. MHE. ZUBEIR ALI MALIUD)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Nne imethibitisha kwamba, imekusudia kupiga vita rushwa katika sekta zote nchini; na kwa kuwa, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu kwamba, wakufunzi wamekuwa wakiwapa usumbufu hasa wanafunzi wa kike hasa kupitia matokeo ya mitihani na kazi za darasani:-

(a) Je, Serikali inatambua kuwepo kwa hali hiyo ya rushwa katika Vyuo vyetu hapa nchini?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais katika kupiga vita rushwa katika sekta hii ya elimu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zubeir Ali Maliud, Mbunge wa Kwamtipura, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwepo na uvumi katika baadhi ya Vyuo vya Elimu ya Juu kuwa kuna rushwa inayohusiana na unyanyasaji wa kijinsia, hasa wakati wa mitihani.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi uvumi huo unapojitokeza hatua za kufuatilia ukweli huwa zinachukuliwa. Mathalani, mwaka 2004 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilifuatilia uvumi huo ili kubaini ukweli. Hata hivyo, Mheshimiwa Spika, kitendo cha rushwa hufanywa kwa siri kubwa, na mbaya zaidi ni hii rushwa ya unyanyasaji wa kijinsia ambayo huwa ni siri kubwa kati ya mtoaji na mpokeaji. Ni pale tu ambapo mtoa rushwa asiporidhika ndipo anaweza kutoa taarifa kwa vyombo vinavyohusika. Kutokana na hali hiyo ya usiri uchunguzi uliofanywa na Chuo hicho haukuzaa matunda.

Lakini kwa kuzingatia ugumu wa kupata ushahidi pia, uongozi wa Chuo uliiomba Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU) kufuatilia uvumi huo ambao tata hivyo uchunguzi bado haukufanikiwa kuwapata wahusika wa pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, katika Chuo Kikuu cha Mzumbe tukio pekee ni la mwaka 2001 wakati Taasisi hiyo bado inaitwa Chuo cha Uongozi wa Maendeleo Mzumbe. Mhadhiri aliyebainika kujihusisha na rushwa ya unyanyasaji wa kijinsia alifukuzwa kazi na Mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, Katika Vyuo vingine kama vile Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, hatuna taarifa rasmi za kujitokeza kwa rushwa ya unyanyasaji wa kijinsia. Hata hivyo, kuna uvumi kwamba vitendo kama hivyo vimejitokeza katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Stadi za Ushirika na Biashara Moshi na Uongozi wa Chuo Kikuu Kishiriki hiki bado unafanya uchunguzi wa kina ili kubaini wahusika na kuwachukulia hatua kali za kinidhamu endapo itathibitishwa kwamba wanajihusisha na vitendo hivyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete za kupiga vita rushwa katika Sekta zote ikiwemo Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. Hatua kadhaa zimechukuliwa na taasisi husika zilizo chini ya Wizara yangu katika kuhakikisha kwamba, vitendo vinavyokiuka maadili havijitokezi. Kwa mfano, kila Chuo kina Kanuni za Maadili ya Wafanyakazi (*Code of Ethics of University Staff*),

Pia kuna Sheria ndogo za Wanachuo (*University Students By- Laws*); na kuna Sera ya Jinsia kwa kila Chuo Kikuu (*University Gender Policy*) ambayo ni kwa vijana

wote wa jinsia zote wa kiume na kike. Aidha, Wizara yangu mara nyingi huchukua ya kuzikumbusha taasisi hizi kufuata Kanuni, taratibu na sheria zinazozingatia nidhamu ya watumishi ndani taasisi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ningependa kumalizia kwa kusema kwamba nawasihi vijana wetu katika Vyuo Vikuu na Vyuo vingine vya Elimu ya Juu kuwa na ujasiri na watoe taarifa mara moja pindi inapobainika kuwepo kwa unyanyasaji huu wa kijinsia. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipatia nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini inaonyesha kuwa bado rushwa katika Vyuo vyetu inaendelea. Japokuwa hatua zinachukuliwa za kuikomesha rushwa hiyo lakini bado inaonyesha kuwa bado inaendelea. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kuwa kama tutaendelea na tabia kama hiyo tunawadhalilisha wanawake? *(Makofi)*

Pili, licha ya kuwa rushwa tu ambayo inachukua nafasi katika Vyuo, lakini hata wizi na uvujaji wa mitihani unachukua nafasi katika Vyuo Vikuu vyetu. Je, katika hili Mheshimiwa Naibu Waziri anachukua hatua gani au kuna mikakati gani ambayo wanahakikisha kuwa wanalifanyia kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu, ingawa sina hakika kuvuja mitihani na rushwa kama vinahusiana.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nafikiri nimeshajibu katika jibu langu la msingi kwamba kila inapojitokeza na tunapopata taarifa Vyuo husika vinafuatilia.

Siyo rahisi kufanyia kazi uvumi kwa sababu hili ni suala nyeti na huwezi ukamtuhumu mtu bila kuwa na uhakika. Na kama ikibainika licha ya Vyuo husika kuchukua hatua basi taratibu za kisheria zinazohusiana na masuala haya zinachukua mkondo wake. Lakini vitendo vilivyojitokeza ndiyo nilivyovisema hapa na hatujapata taarifa nyingine rasmi kutoka katika Vyuo kwamba hivi vitu vinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema swali lake la pili, naona halihusiani na rushwa. Hili linahusiana na wizi wa mitihani ambalo ni swali jipya na ambalo linahitaji kufanyiwa kazi na kuleta jibu sahihi mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri. Kwa kuwa amekubali kwamba rushwa ipo na sera ipo. Na Vyuo Vikuu vina sheria za maadili katika Vyuo vyao. Je, Serikali inahakikishiaje kwamba wanafunzi wanapofika Vyuoni wanapata ufahamu kwamba ni haki yao kutendewa haki na siyo kutoa rushwa na

kueleweshwa kwamba kuna hizo Kamati za maadili pamoja na sera ya kuwalinda watoto wa kike?

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu yake ya msingi mazuri kabisa ambayo yanajitosheleza. *(Makofi)*

Lakini la pili, ni kwamba katika kila Chuo kuna taratibu za kuwapokea vijana wanaojiunga na Chuo Kikuu kwa mara kwanza na huwa tunatenga wiki mzima ya kuzoea mazingira na kufahamishwa taratibu mbalimbali za Vyuo inaitwa *Orientation Week*. Wakati huo wanafunzi hupewa maelezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kanuni za mitihani, mazingira ambayo wataishi. Haki zao ambazo wanastahili ikiwa ni pamoja na mambo ya kijinsia. Kwa hiyo, wanafunzi huwa wanaanza masomo wakiwa wameishafahamishwa mambo yote haya ya kimsingi. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. NG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu walishawahi kueleza kwenye Mkutano Mkuu wa UKIMWI uliofanyika Arusha kwamba suala la rushwa ya ngono ipo mashuleni hasa katika Vyuo Vikuu; na kwa kuwa suala hili kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyojibu ni siri. Serikali itakubaliana nami kwamba sasa wakati umefika wa kupiga kura za siri ili wanafunzi waweze kubaini hili tatizo. Kwa sababu wanaogopa kusema wazi wanaweza kufukuzwa. Je, sasa Serikali haioni kwamba waandike kwa siri ili wabainike walimu wanaojihusisha na tatizo hili?

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, suala la kupiga kura kwa siri inaweza kuwa na madhara yake vilevile. Lakini huko nyuma katika jibu la msingi imeelezwa kwamba tayari kuna hatua mathubuti ambazo zimekwishachukuliwa kwa wale watu ambao walibainika. Nafikiri jambo la msingi na la wazi zaidi ni kuwaomba vijana wetu pale inapotokea tatizo walitoe hadharani. Walipeleke kwenye mamlaka zinazohusika ili kusudi hatua kamili ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kura za siri pamoja na uzuri wake zinaweza ku-*victimize* watu wengi ambao kwa kweli kwa namna moja ama nyingine hawahusiki. Ombi langu ni kwamba vijana wetu katika Vyuo Vikuu yanapotokea mambo kama hayo wapeleke malalamiko yao katika mamlaka zinazohusika ili hatua kamili ziweze kuchukuliwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 160

**Elimu ya Juu Nchini**

**MHE. DR. ALI TARAB ALI (K.n.y. MHE. FATMA M. MAGHIMBI**) aliuliza:-

Kwa kuwa Elimu ya Juu ni suala la Muungano:-

(a) Kuna idadi maalum inayotengwa kwa ajili ya wanafunzi kutoka Tanzania Zanzibar?

(b) Je, ajira ya wafanyakazi katika Wizara huwa zinatenga idadi maalum ya wafanyakazi kutoka Tanzania Zanzibar kushika nyadhifa mbalimbali?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mbunge wa Chakechake, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Elimu ya Juu ni moja ya masuala ya Muungano. Aidha, tafsiri ya Muungano wa Elimu ya Juu niliufafanua ndani ya Bunge lako Tukufu hapo juzi tarehe 4 Julai, 2006 wakati najibu sehemu (a) ya swali namba 141 la Mheshimiwa Yahya Kassimu Issa, Mbunge wa Chwaka. Katika jibu langu nilieleza kuwa Elimu ya Juu kama kipengele cha Muungano ina kwamba sehemu zote za Muungano zina fursa sawa katika ushindani wa nafasi katika Vyuo Vikuu na Taasisi nyingine za Elimu ya Juu nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo, hakuna idadi maalum inayotengwa kwa ajili ya wanafunzi kutoka Zanzibar.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hivi sasa kuna *quarter system* kwa ajili ya wanawake kupitia *CANAG Scholarship Programme*. Na Vilevile historia inaonyesha kwamba huko zamani kulikuwa na idadi maalum ya wanafunzi kutoka Zanzibar isipokuwa kwa sababu Wazanzibar walikuwa wanaomba kuingia Chuo Kikuu Dar es Salaam kupitia Wizara ya Elimu ya Zanzibar ambayo ilikuwa inachelewesha majina kwenda kwenye *selection* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Je, hawaoni sasa ni wakati muafaka kuendeleza mfumo huo ambao ulikuwepo kuhakikisha kwamba kuna nafasi maalum kwa ajili ya Zanzibar? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu yake ya msingi ambayo ni sahihi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba kulikuwa na *quarter system* ya wanafunzi waliokuwa wanatoka Zanzibar kujiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Taratibu zilizotumika siku zote ni hizi za ushindani ambazo zipo. Mimi nafikiri wakati umefika sasa wa kuangalia ni kwa nini kunakuwa na tofauti. Pengine ni vizuri tukaangalia

mitaala yetu hasa ya Elimu ya Msingi na mafunzo ya awali na vilevile mitaala ya *Secondary Schoo*l ili tuone kwamba upungufu uko mahali gani. Lakini kutoa nafasi katika Vyuo Vikuu kwa *quarter* hili litashusha ushindani ambao umewekwa katika Elimu ya Juu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni kweli kwamba tukiwa na *quarter sytem* pengine ushindani utapungua. Lakini je, tuna hakika kwamba Zanzibar inapata wataalam wa kutosha kwa *system* hii tuliyonayo hivi sasa?

**SPIKA:** Ni swali moja tu kwa sababu wewe siyo mwenye swali.

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, jitihada za kupata wataalam wa kutosha katika nchi yetu iko katika Ilani ya Uchaguzi na hilo linafanyika kwa kuongeza nafasi katika Vyuo Vikuu na kwa kujenga Vyuo Vikuu vingine ili kusudi Watanzania kwa ujumla wao waweze kupata nafasi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika napenda kurudia tu kwamba ile *quarter system* kwa kweli halitakuwepo. Tunachohitaji ni kutazama ni kitu gani cha msingi kinaleta tofauti. Kwa sababu hata Tanzania Bara kuna sehemu ambazo watu hawapati nafasi za kutosha. Kwa mfano, wafugaji wana matatizo hayo. Sasa tukianza kusema wafugaji wapewe nafasi maalum, basi tutakwenda kwenye hiyo *quarter system*.

Naomba tuzingatie mambo ya msingi ili tutatue matatizo tuliyonayo. Ili kusudi vijana wengi zaidi kutoka Tanzania Zanzibar waweze kujiunga na Vyuo Vikuu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 161

**Watoto Kufanyiwa Vitendo Viovu vya Kubakwa**

**MHE. OMAR S. KWAANGW' (K.n.y. MHE. DORAH H. MUSHI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna watoto wengi wadogo walioko kwenye mazingira magumu na wengine bado wako shule za msingi, lakini wanafanyiwa vitendo viovu kama vile kubakwa na pale wahusika wanapobainika na kupelekwa kwenye vyombo vya sheria, baadaye hukutwa mitaani wakitamba:-

(a) Je, uonevu huo kwa watoto utakomeshwa lini?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia watoto hao kwa kuifanya sheria iliyopo itumike kikamilifu?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mushi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa siku za karibuni yametokea matukio ya uonevu na yanayowadhalilisha watoto. Ni wajibu wetu, mmoja mmoja na kwa ujumla wetu kuhakikisha kwamba vitendo hivyo vinakomeshwa na havitokei tena. Ili hili liweze kutekelezwa ni lazima jamii katika ngazi ya familia kuwalinda watoto na kuzingatia sheria zinazohifadhi haki za watoto. Naomba kutumia fursa hii kutoa rai kwa raia wema kushiriki kikamilifu katika vita dhidi ya ubakaji wa watoto na vitendo vinavyowadhalilisha watoto. Kwa upande wa Serikali tutaendelea kushirikiana na asasi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kutoa elimu kwa jamii ili watoto wasifanyiwe vitendo vya uonevu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba Sheria ya Makosa ya Kujamiiana inatekelezwa ili kuwanusuru watoto kutoka kwenye makosa yanayosimamiwa na Sheria hii. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka jana wafungwa 6662 walikuwa wakitumikia adhabu ya kifungo kutokana na makosa hayo ya kujamiiana. Kadhalika mahabusu 2687 walikuwa magerezani kutokana na kutuhumiwa kuhusika katika makosa ya kujamiiana.

Aidha, Mahakama zimekuwa zikitoa adhabu za kifungo kwa watu waliopatikana na hatia ili kutoa fundisho kwa watu wengine na pale ambapo watuhumiwa wa makosa hayo wanaonekana hawana hatia Serikali imekuwa ikiomba rufani kwenye Mahakama za juu zaidi ili kutengua maamuzi ya kuwaachia watuhumiwa hao kama inaonekana upo ushahidi wa kuridhisha kuwatia hatiani.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, jukumu la kuhakikisha kwamba sheria hiyo na sheria nyingine zote zinatekelezwa kikamilifu ni la wanajamii wote ikiwa ni pamoja na Serikali yenyewe, vyombo vyote vya umma na Mashirika yasiyokuwa ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa siku za karibuni yametokea matukio ya uonevu na yanayowadhalilisha watoto. Ni wajibu wetu mmoja mmoja na kwa ujumla wetu kuhakikisha kwamba vitendo hivyo vinakomeshwa na havitokei tena. Hili ili liweze kutekelezwa ni lazima jamii katika ngazi ya familia, kuwalinda watoto na kuzingatia sheria zinazohifadhi haki za watoto. Naomba kutumia fursa hii kutoa rai kwa raia wema kushiriki kikamilifu katika vita dhidi ya ubakaji wa watoto na vitendo vinavyowadhalilisha watoto. Kwa upande wa Serikali tutaendelea kushirikiana na Asasi na Mashirika Yasiyo ya Serikali kutoa elimu kwa jamii ili watoto wasifanyiwe vitendo vya uonevu.

Mheshimiwa Spika, pili Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba Sheria ya Makosa ya Kujamiiana inatekelezwa ili kuwanusuru watoto kutoka kwenye makosa yanayosimamiwa na sheria hii. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka jana wafungwa 6,662 walikuwa wakitumikia adhabu ya kifungo kutokana na makosa haya ya kujamiiana. Kadhalika mahabusu 2,687 walikuwa Magerezani kutokana na kutuhumiwa kuhusika katika makosa ya kujamiiana.

Aidha, Mahakama zimekuwa zikitoa adhabu ya kifungo kwa watu waliopatikana na hatia ili kutoa fundisho kwa watu wengine na pale ambapo watuhumiwa wa makosa hayo wanaonekana hawana hatia Serikali ilikuwa ikiomba rufaa kwenye Mahakama za juu zaidi ili kuchukua maamuzi ya kuwaachia watuhumiwa hao kama imeonekana upo ushahidi wa kuridhisha kuwatia hatiani.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo jukumu la kuhakikisha kwamba sheria hiyo na sheria nyingine zote zinatekelezwa kikamilifu ni la wanajamii wote ikiwa ni pamoja na Serikali yenyewe, vyombo vyote vya umma na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa ngazi za utawala za Serikali zinaanza kwenye vitongoji na Serikali za Mitaa na kwa kuwa sasa tunataka tugeukie hawa ambao kwa kweli ni vibaka baada ya kufanya kazi kubwa ya ujambazi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba ngazi hizi za msingi za vitongoji na mitaa zinakuwa na mikakati maalum kabisa ya kupambana na vibaka?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nadhani hilo ni swali jipya? Kwa sababu vibaka ni tofauti na wababakaji. (*Makofi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vitendo vya kubaka watoto wadogo na wanawake vinazidi kushamiri hapa duniani pamoja na sehemu nyingi. Na sheria tuliyonayo ni ya kumfunga tu huyu aliyebaka baadaye anamaliza miaka anarudi. Je, Serikali haioni haja sasa tukabadilisha hiyo sheria ya kumfunga iletwe hapa tuibadilishe wakanyongwe ili wapungue watu kama hawa? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge umesema vibaka au wababakaji?

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA**: Na swali la msingi ni kubaka watoto. Wanaobaka muda huu wa kufungwa wanarudi tena wanaendelea kubaka. Sasa kwa nini tusibadilishe hii sheria ikabadilishwa tuwanyonge moja kwa moja waishie huko. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya msingi. Kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Nyawazwa naomba kujibu kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kama jibu la msingi lilivyoeleza kwamba idadi ya watu wanaopatwa na makosa haya yanaongezeka mwaka hadi mwaka. Nafikiri imefika wakati ambapo lazima Watanzania waone kwamba adhabu ya kifungo peke yake haitoshi. Na kwa hivyo ningependa kwanza nafikiri ni sawa kwamba sheria hii irudi hapa Bungeni lakini sio kwa madhumuni ya kunyonga bali kuangalia upya. Ila ninafikiri lililo la muhimu ni kutoa elimu kwa jamii kwamba makosa kama hayo yanadhalilisha na yanaondoa heshima ya jamii kwa ujumla. Pili, lazima wazazi wajaribu kujenga tabia nzuri ya watoto ili toka wanapokuwa wadogo mpaka wanapokuwa wakubwa waone kwamba vitendo vya kubaka au kudhalilisha watoto au wanawake si vitendo ambavyo vinapaswa kuendekezwa na vinadhalilisha wale wanaofanya hivyo.

Na. 162

**Utekelezaji wa Sheria ya Kujamiiana**

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O (K.n.y. MHE. ZAYNAB M. VULU)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Sheria na Mambo ya Makosa ya Kujamiiana ya Mwaka 1998 ilitungwa ili kupunguza unyanyaswaji kwa wanawake na watoto nchini:-

(a) Je, ni kwa kiasi gani Sheria hiyo imepunguza unyanyaswaji kwa wanawake na watoto hasa kwa suala la ubakaji?

(b) Je, Serikali ina takwimu zozote zinazoonyesha ni kwa kiasi gani makosa ya ubakaji yamepungua?

(c) Kama hayajapungua. Je, Serikali imechukua hatua gani ili kuwanusuru wanawake na watoto katika madhara ya ubakwaji?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Zaynab Vulu, Viti Maalum, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kuwa tangu kutungwa kwa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya 1998 kesi za unyanyasaji dhidi ya wanawake na watoto zinazofunguliwa Mahakamani zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka, kwa mfano Julai – Desemba, 1988, sheria ilipoanza kesi za ubakaji zilizofikishwa Mahakamani ni 1,203, mwaka 1999 – zilikuwa 2,430, mwaka 2004 zilikuwa 4,795.

Ongezeko hili la kesi linaonyesha kwamba sheria hii imechangia kwa kiasi kikubwa, katika kuwaamsha Watanzania ambao sasa wameamua kutoa taarifa katika

vyombo vya dola kuhusu unyanyasaji unaofanywa dhidi ya wanawake na watoto hususan makosa ya ubakaji, tofauti na ilivyokuwa siku za nyuma kabla ya kutungwa kwa sheria hii ambapo vitendo vya ubakaji vilikuwa vikitokea kwa wingi lakini wahusika hawakuwa tayari kutoa taarifa za vitendo hivyo kwa wingi katika vyombo vya dola.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zaynab Vulu, yenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, si rahisi kupata takwimu zinazoonyesha ni kwa kiwango gani sheria hii imepunguza vitendo vya unyanyasaji kwa wanawake na watoto hasa kwa suala la ubakaji. Lakini kutokana na takwimu nilizotoa hapo juu kufunguliwa kwa kesi nyingi za ubakaji Mahakamani chini ya sheria hii kunaonyesha ufanisi wa sheria hii pamoja na mwamko wa jamii katika kupambana na vitendo vya unyanyasaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kumpongeza Mheshimiwa Zaynab Vullu na wanaharakati mbalimbali waliohamasisha matumizi ya sheria hii, bila shaka wataendeleza juhudi zao, ili kuendelea kupunguza unyanyasaji na hasa ubakaji wa wanawake na watoto. Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma hasa kwa akinamama na watoto ili waelewe namna ya kujikinga na matukio haya mabaya ya unyanyasaji na sheria itaendelea kuchukua mkondo wake kuwabana watuhumiwa wote watakaojihusisha na matukio haya ya aibu.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na ya uchambuzi wa kina. Lakini napenda kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa idadi ya wanawake ambao wamebakwa inaendelea kuongezeka na kwa takwimu hizi inakaribia toka sheria itungwe ni karibu wanawake 10,000 wamebakwa. Na kwa kuwa hao wabakaji wengi wao hawajui hali zao kama wana virusi vya UKIMWI . Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka kwa wale wanaobaka wapimwe virusi vya UKIMWI ili kama watakuwa wamewaambukiza hao akinamama au wasichana waweze kuchukua tahadhari ya kupewa dawa mapema?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ubakaji ni kosa baya sana na ni kosa la aibu. Lakini kupimwa virusi kama anavyofahamu Mheshimiwa Mbunge ni suala la hiari, hakuna sheria inayolazimisha Serikali kuwapima watu virusi. Kwa hiyo, nafikiri labda kama Bunge lako Tukufu litaridhia basi itakuwa vizuri. Lakini kwa sasa hali ilivyo ni kwamba huwezi kumpima mtu virusi kwa nguvu hata kama ni mkosaji.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wanaobakwa huathirika kisaikolojia. Je, Serikali ina vituo vingapi kwa ajili ya kuwafanyia *counselling* na kama havipo kuna mkakati wowote wa kuanzisha vituo hivyo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nimeeleza katika swali la awali kwamba ni kweli vifungo peke yake hata kunyonga pengine haitakomesha vitendo hivyo. Na kwa hivyo suala la *counselling* ni muhimu sana. Sina hakika kama tuna vituo ambavyo ni mahsusi kwa ajili ya kuwa-*counsell* wabakaji au wale waliobakwa.

Lakini naona umuhimu wa kufanya hivyo kama njia moja kwanza ya kuwaponya wale waliopatwa na matatizo hayo kwa sababu tatizo kama hilo likimpata mtu huwa halitoki kwenye akili yake. Kwa hiyo, Serikali inachukua ushauri mzuri ambao Mheshimiwa Mbunge ameutoa.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa hadi hivi sasa kuna sheria mbili zinazopingana. Sheria moja inasema umri wa mtoto wa kike kuolewa ni miaka 14 na kuendelea. Na Sheria ya pili ni ile inayosema mtoto mdogo ni yule ambaye umri wake ni chini ya miaka 18 na ukijamiiana naye umekwishabaka. Je, kwa kuwa sheria hizi mbili zinapingana kiasi hicho ni sheria ipi tutaifuata ambayo haitamdhalilisha mwanamke ambaye anaonekana kuwa ni mdogo na kwamba ukijamiiana naye sasa hujambaka?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli hilo limejitokeza kwamba kuna sheria mbalimbali ambazo zina tafsiri mbalimbali za mtoto. Hivi sasa Serikali ipo katika mchakato wa kuandaa sheria inayomhusu mtoto ambayo katika sheria hiyo itakuwa ni moja tu ambayo itatafsiri kwamba mtoto ni yule ambaye yuko chini ya miaka 18. Sheria hiyo kabla ya kufika hapa Bungeni inapelekwa kwa wananchi kama *White Paper* ili kutoa maoni. Kwa hiyo, kabla ya mwaka huu kwisha tutakuwa na mjadala huo kwa kutoa maoni kwamba mtoto ni yule ambaye yule ambaye yuko chini ya miaka 18.

Na. 163

**Kununua Meli Mpya**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA (K.n.y. MHE. SAVELINA S. MWIJAGE)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais Mstaafu aliwaahidi wananchi wa Mikoa ya Mwanza na Kagera kuwa Serikali itanunua meli mpya itakayofanya kazi kati ya Bukoba na Mwanza, kwa kuzingatia kuwa meli ya MV. Victoria imetumika kwa zaidi ya miaka hamsini sasa:-

Je, Serikali imefikia wapi katika kutekeleza ahadi hiyo ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Katika kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

1. Kwanza imetoa leseni kwa Kampuni ya *Lake Fast Ferries Ltd.* kuendesha meli za kutoa huduma za usafirishaji katika Ziwa Victoria. Meli hizi kwa hivi sasa ziko katika ukaguzi baada ya kufanyiwa ukarabati. Tunategemea kuwa zitaendelea kutoa huduma zake mara Mkaguzi atakapojiridhisha juu ya ubora wake.

2. Pili, imetoa leseni nyingine kwa *Speke Shipping Lines Ltd;* Kampuni hii imepewa leseni ya kujenga meli moja ya mwendo wa kasi ya kubeba abiria na shehena za tani 350. Hadi tarehe 29 Juni, 2005, mwekezaji huyu alikuwa ameanza kufanya tathmini za usanifu wa meli – *Structural Design* kwa kushirikiana na wataalam wa usanifu meli *Sea Transport Solutions Ltd.* ya Australia.

3. Tatu, Kampuni ya *Sea Lines on Lake Victoria Enterprises (SOLVE)* toka Sweden imeonyesha nia ya kuwekeza kwenye usafiri wa abiria huduma za utafutaji na uokoaji pamoja na elimu ya mabaharia. Bado hajaanza kazi Ziwani ingawa Serikali tumeufurahia mradi huu.

Ni nia ya Serikali kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa wale wote wenye nia ya kuwekeza katika nyanja hii. Lengo kuu ni kuboresha usalama kwa usafiri na uchukuzi katika Ziwa Victoria. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa ukanda wa Ziwa Victoria na popote nchini na ng'ambo wajitokeze kuwekeza kwenye vyombo vya usafirishaji kwenye Ziwa hilo kwa lengo la kuboresha maisha ya wananchi na kujipatia faida kibiashara.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa kuuliza suala moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina suala dogo tu la kumwuliza. Kwa kuwa historia inaonesha kuwa kwenye Ziwa Victoria ajali nyingi zimetokeza na zilizoua watu na hii inaonesha kuwa ni uchakavu wa vyombo hivi vya usafiri ndani ya Ziwa lenyewe. Pamoja na kuwa Serikali inawaruhusu watu binafsi kufanya kazi hiyo lakini kwa sababu ya kuokoa maisha ya watu haioni kuwa Serikali yenyewe inapaswa kununua angalau meli moja ili kuwasaidia wasafiri wa ziwa hili? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, napenda nimkumbushe Mheshimiwa Khalifa kwamba hapa

tulipitisha sera kwamba tunajiondosha Serikali katika masuala mazima ya biashara. Tukatoa nafasi kwa sekta binafsi ifanye shughuli zake. Kwa sasa msimamo huko hapo na ni kuwaomba wananchi waweze kuwekeza katika nyanja hii.

Pili, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Ziwa Victoria tuna meli kama kumi zinafanya hizo shughuli na zinatoa huduma ipasavyo na tunahakikisha kila mwaka meli zile zinakaguliwa na kupewa cheti cha ubora. Napenda niwahakikishie Waheshimwa wananchi kwamba Serikali yao inawajali na itawashughulikia ipasavyo katika masuala ya usafiri na uchukuzi katika Maziwa.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa meli zinazoitwa *Lake Fast Ferries* zilianza kazi katika Ziwa Victoria kati ya Mwanza na Bukoba mwezi Oktoba, 2005 kwa maana nyingine ni meli mpya. Lakini kwa kipindi hicho zimeshasimama mara mbili kufanya kazi ama kwa ukaguzi ama kwa ubovu. Je, zitakapokuwa zimerudi wananchi wataziamini kwa kiwango gani kwamba sasa ni safi wanaweza wakazitumia? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Ruth kwamba meli zile zilipata hitilafu mbili tatu. Kwanza kulikuwa na matatizo ya uchafu wa mafuta ndio maana zikawa zinasimama njiani na pili tulipoona kwamba hatukuridhika na uendeshaji wake ndio tulipozisimamisha. Sio kwamba ni mwenye meli alizisimamisha. Tulizisimamisha sisi ili zikaguliwe kwa kina ipasavyo na tuweze kuziruhusu zifanye tena huduma zake.

Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeamua meli hizo zikaguliwe na wakaguzi kutoka nje ili tuweze kujiridhisha ipasavyo.

Na. 164

**Kilimo cha Umwagiliaji Maji**

**MHE. FRED M. TUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa, Seikali ya Awamu ya Nne inatoa kipaumbele zaidi katika suala la Kilimo cha Umwagiliaji na msisitizo umewekwa kwenye miradi midogo na ya kati ya umwagiliaji na kuvuna Maji ya Mvua, na kuendelea kupanua maeneo yanayofaa kwa Kilimo cha Umwagiliaji Maji:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia wananchi kupanua na kuboresha Kilimo cha Umwagiliaji katika Kata ya Itilima Wilaya ya Kishapu ambako kuna mradi wa hekta 225 ili uweze kuongeza uzalishaji wa zao la Mpunga toka magunia 25 hadi 40 kwa ekari moja na kupata chakula cha kutosha na kwa ajili ya biashara?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kubaini maeneo mengine ya umwagiliaji, mfano bonde la Mto Tungu, Mto Manonga na Mto Mhumbu katika kijiji cha Bulekela, Mwajidalala, Ng'hwang'harala, Dijongo na Mihama ili kuongeza uzalishaji wa chakula na kuondoa tatizo la njaa Wilayani Kishapu?

(c) Je, Serikali inakubali kuwa kuna umuhimu wa kujenga mabwawa ya kuvuna maji ya mvua kwenye Mto Tungu, Mangu na Mhumbu katika mpango wa dharura ili kuweza kukabiliana na ukame, na kuepuka upungufu wa maji kwa kilimo na kusababisha mifugo kuhamishiwa sehemu nyingine?

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa haya ni mapya au una cha sasa au ndivyo ulivyolipeleka hili swali Bungeni? Kwa sababu kinachoruhusiwa hapa ni kusahihisha kosa la upigaji chapa, huwezi kubadili ukame ikawa njaa, ukabadili. Inaleta taabu kwa Serikali. Nataka uhakika tu huo?

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Spika, uhakika ni kwamba hatuondoi ukame tunaondoa tatizo la njaa.

**SPIKA:** Nafahamu hivyo lakini uliuliza nini?

**MHE. FRED M. TUNGU:** Niliuliza hivyo hivyo.
**SPIKA:** Njaa?

**MHE. FRED M. TUNGU:** Ndiyo.

**SPIKA:** Basi Ofisi ya Katibu muangalie mambo haya unabadili vipi ukame ukaweka njaa au njaa ikawa ukame?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Fred Mpandazoe, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, nitoe maelezo mafupi sana kama ifuatavyo:- kwamba katika kujibu maswali ya umwagiliaji nimegundua kwamba tunafanya *reference* kwa *National Irrigation Master Plan* ambayo Waheshimwa Wabunge wengi hasa wapya hawana. Kwa hivyo nataka niwaahidi kwamba tutaandaa nakala ili tunapofanya *reference* hii *National Irrigation Master Plan* tuwe tunaijua maana Wabunge wengi wanafuatilia sana mradi wa umwagiliaji. Baada ya maelezo hayo kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fred Mpendazoe Tungu, Mbunge wa Kishapu lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umwagiliaji wa Itilima ulikwishajengwa na kukamilika tarehe 25 Julai 2005, na uligharimu kiasi cha shs. 302,131,545. Mradi huu ulijengwa na Serikali chini ya Mpango Husishi wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji

(*Participatory Irrigation Development Programme (PIDP).* Baada ya mradi kukamilika, Wizara yangu imepanga utaratibu wa kuendesha mafunzo kwa wakulima na wataalamu kuhusu mbinu bora za ukulima wa kisasa wa mazao na matumizi bora ya maji ili kuinua tija, mavuno, na mapato ya wakulima.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekwisha kuona umuhimu wa kubaini maeneo ya Umwagiliaji kwa nchi nzima. Kwa kutambua hilo, Wizara yangu, katika mwaka 2003/2004 ilikamilisha Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji (*National Irrigation Master Plan*), ambao umeainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu inashauriwa kushirikiana na Ofisi ya Kanda ya Umwagiliaji iliyopo Mwanza ili maeneo ya umwagiliaji yaliyoibuliwa na Wilaya kwa utaratibu shirikishi kutoka miongoni mwa wakulima Vijijini ifanyiwe uchunguzi na michoro ya kitaalamu ndipo iingizwe katika Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya ya Kishapu *(DDADPs,)* au kuombewa fedha kutoka ama kwenye kapu la Mfuko wa *ASDP (ASDP Basket Fund)* au vyanzo vingine kama vile *TASAF* au *FACF.*

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuvuna maji katika maeneo kame na ndio maana ilianzisha mradi wa *(Participatory Irrigation Development Project (PIDP)*

Katika mwaka wa 2006/2007, Wizara yangu inaanza kutekeleza Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP)* ambao utagharamia shilingi Trilioni 2.5. Sehemu kubwa ya fedha hizi zitaelekezwa kwenye

Mipango ya Maendeleo ya Wilaya *(DADPs)* ambayo itakuwa sehemu ya Mipango ya Maendeleo ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Mradi wa uwekezaji katika Sekta ya Kilimo ngazi ya Wilaya *(District Agricultural Sector Investment Project, DASIP)* ulizinduliwa mwezi Aprili 2006 na unajumuisha Wilaya zote 25 za Mikoa mitano ya Mwanza, Tabora, Kigoma, Kagera na Shinyanga. Mradi huu unasimamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* kwa *USD 78* milioni kwa miaka mitano (5). Ofisi Kuu ya Mradi huu iko Mwanza. Aidha, mradi wa aina hiyo unaandaliwa mwaka huu kwa Wilaya zote za Mikoa ya Tabora, Rukwa, Singida na Dodoma na kwa uhisani wa *ADB.* Miradi yote hii ni ya utekelezaji wa *ASDP* na kwa hiyo itatoa fedha kwa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs).*

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafsi ili na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imetilia mkazo ili kilimo cha umwagiliaji na imesema tujitahidi kumwagilia kutoka katika kila chanzo cha maji kinachopatikana. Ningependa kujua sasa Serikali ina mpango gani katika kupunguza huu muda unaotumika kusubiri kibali hiki cha *Water Right* ambacho mpaka Bodi ikae na wakati mwingine *process* zinapokamilika inachukua hata mwaka?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeunda mabonde 9 nchini pote ambayo yamepewa mamlaka ya kuchunguza na kutoa vibali vya matumizi ya maji katika maeneo mbalimbali nchini. Hiyo imefanyika ili kusogeza huduma ya utoaji wa *Water Right* karibu zaidi na watumiaji.

Kwa hiyo Wizara yangu haina habari juu ya ucheleweshaji anaoungelea lakini tunaweza kuzungumza na kuyahimiza mabonde haya kutoa *Water Right* kwa haraka inavyowezekana ili kutochelewesha huduma za maji na za umwagiliaji katika maeneo mbalimbali. Bonde la Ziwa Victoria ndilo linalohusika zaidi na eneo analotoka Mheshimiwa Mbunge.

Kwa hiyo tutawasiliana nao ili wasicheleweshe utoaji wa huduma muhimu kwa watumiaji maji.

Na. 165

**Vijana Kujitegemea**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (K.n.y. MHE. JANETH M. MASSABURI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, vijana wengi wa vijiweni na wa *Camps* nyingi nchini wameonyesha nia ya kushirikiana na Serikali katika suala la kujitegemea na kupunguza umaskini; na kwa kuwa, Serikali imeahidi kuwawezesha vijana kwa kuwapatia ajira mbalimbali:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengwa vijana wetu Vyuo vya Ufundi Stadi kwa kila Wilaya nchini kama Mhe. Rais wa Awamu ya Nne alivyoahidi?

(b) Je, ni jitihada gani za dhati zilizochukuliwa kuwatambua vijana wote wa *camps* vijiwe na mashina ya wakereketwa kwa takwimu sahihi hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa wale vijana wenye uwezo wa kufanya kazi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE JEREMIA S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua umuhimu wa mafunzo ya ufundi stadi katika kuwawezesha vijana kushiriki katika soko la ajira. Ili kukidhi umuhimu huo, Serikali ilikwishatayarisha mpango kamambe wa kujenga vyuo vya *VETA* katika kila Mkoa Tanzania Bara. Mpaka sasa Mikoa 18 kati ya Mikoa 21 ina vyuo vya *VETA* vya Serikali. Mikoa mitatu ya Manyara, Lindi na Pwani ndiyo haijapata vyuo vya Serikali. Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Korea Kusini zimetiliana saini Mkataba wa kujenga vyuo vinne vya *VETA* katika Mikoa hiyo kikiwemo Chuo cha *Information Technology* kitakachojengwa eneo la *VETA*, Chang'ombe Jijini Dar es Salaam. Ujenzi wa vyuo hivyo

utaanza wakati wowote baada ya kukamilika kwa taratibu zinazohusu mkataba huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi imemteua *Consultant* ili aangalie upya namna bora ya kuhuisha Elimu ya Ufundi wa *VETA* katika mitaala iliyopo na kupendekeza njia nzuri ya kupanua Elimu hiyo hadi kuwa na vyuo hivyo katika ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, sanjari na vyuo hivyo vya *VETA* vya Serikali vipo pia vyuo vya ufundi vya watu binafsi na taasisi za dini vipatavyo 842 ambavyo vinatoa mafunzo ya ufundi stadi, mafunzo ambayo huratibiwa na *VETA* ili kuhakikisha kuwa viwango vya mafunzo ya ufundi stadi vilivyoainishwa na *VETA* vinazingatiwa

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekamilisha sensa na kuwatambua vijana waliopo kwenye vikundi vya uzalishaji mali na vijiwe *(Youth Mapping)* katika Wilaya 78 za Tanzania Bara. Zoezi hili litaendelea katika Wilaya 43 zilizobakia katika mwaka wa fedha wa 2006/2007. Madhumuni ya zoezi hili la *youth mapping* ni:-

- Kuvitambua aina ya vijiwe pamoja na *camps* za vijana ili kujua vijana wako wangapi, wanafanya nini na wanahitaji nini ili Serikali iweze kuwasaidia katika kuwezesha kimtaji na kuwapa ushauri wa jinsi ya kujikwamua kwenye matatizo waliyonayo.
- Kuvigeuza vijiwe na *camps* hizi baada ya kuvisajili kuwa Vyama vya Akiba na Mkopo ili vianzishe miradi/shughuli za uzalishaji mali.

- Kuvitambua kihalali na rasmi vijiwe hivi ili viwe ni kichocheo cha kuhamasisha vijiwe vingine vitakavyoanza kuwanufaisha vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa mkoa wa Dar es Salaam, zoezi hili limeainisha kuwepo kwa vijiwe 509 ya vijana ambavyo baadhi vinashughulika na kazi za ufundi wa magari, uchongaji vipuri, waosha magari, wasukuma mikokoteni, wapiga rangi n.k. Aidha katika zoezi hili pia, vijiwe vingine vimebainika kutumika kama sehemu ya uuzaji wa madawa ya kulevya, vibaka na vitendo vingine visivyokubalika kijamii.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili ambalo limefanyika katika Wilaya 78 limetupa taarifa muhimu sana kwa Wizara yangu ambayo itatusaidia katika kuandaa pogramu mbalimbali za kuwasaidia vijana katika kuwapa ushauri, kuwawezesha kujiajiri pamoja na kuwawezesha kupata mikopo yenye masharti na riba nafuu.

**SPIKA:** Waheshimiwa kipindi cha maswali kimekwisha na ninayo matangazo, wale wageni wa Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mbeya vijiji, Waheshimiwa Madiwani kutoka Halmashauri ya Mbeya vijijini, naarifiwa kwamba sasa wamewasili, ningeomba tuwatambue wakisimama pale walipo. Ahsante sana karibuni sana. Pia kuna wageni wa Mheshimiwa Ngeleja, kutoka Jimbo la Sengerema, ni wageni 11, wakiwa ni wajumbe waliokuja kwenye Mkutano Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa yaani *TALGWU* wale pale. Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, ana mgeni mmoja

ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Wilaya ya Songea Mjini, Mheshimiwa Abdallah Ndege. (*Makofi*)

Matangazo mengine semina ya Kamati ya Kilimo na Ardhi na Wabunge wanaotoka kwenye Wilaya zinazozalisha zao la kahawa, ambayo ilikuwa imepangwa kufanyika tarehe 7/7 imeahirishwa na wahusika watatangaziwa baadaye tarehe mpya. Kwa hiyo, semina ya Kamati ya Kilimo na Ardhi pamoja na Wabunge wa kutoka maeneo ya Kahawa imeahirishwa tutatangaziwa baadaye. Kamati ya Kilimo na Ardhi Mwenyekiti wake Mheshimiwa Gideon Cheyo, anakuombeni Wajumbe wote mkutane leo hii saa saba mchana katika ukumbi gorofa ya mbili, chumba Na. 231 Jengo la Utawala. Kwa hiyo, Kamati ya Kilimo na Ardhi saa saba mchana chumba namba 231. *(Makofi)*

Sikuliona mapema hili tangazo la wageni, kuna wageni wetu kutoka nje ambao wanatoka Uingereza, *from the United Kingdom* Mr. Thobias Ditman and Mr. Bastian Jonas. Hawa wamekuja kufundisha katika Chuo cha Ufundi maeneo ya Mkoa wa Kagera na wamekuwapo sasa kwa mwaka mmoja pia miongoni mwao wapo washiriki 27 wa mafunzo ya Utawala Bora, yanayoendeshwa na Chuo cha Mipango cha Dodoma ambao nao wako hapa. Chuo cha Mipango wale pale, karibuni sana. Nimearifiwa pia kuna watoto wetu, wanafunzi wa Shule ya Msingi Chadulu Dodoma, na Walimu wao. Kutakuwa na semina ya Wabunge wote, tarehe 8, Julai itakayohusu utekelezaji wa programu ya maji vijijini, imeahirishwa. Nadhani inazingatia kwamba Waheshimiwa Wabunge wengine watakuwa Sabasaba Dar es Salaam si rahisi kurudi mapema. *(Makofi)*

Katika siku nadhani ya juzi na baada ya hapo kumekuwa na mjadala miongoni mwa Wabunge kwamba Spika wa Bunge la Jamhuri amekataza neno: "kazana" amelipiga marufuku. Waheshimiwa Wabunge nilivyosema na naomba nieleweke kuwe na tahadhari sana ya kutumia neno hilo. Bunge ni mahali pa heshima sana, na kama mnavyofahamu, watu wengi sana, mamilioni ya Watanzania hivi sasa kutokana na mafanikio ya Serikali hii kufikisha umeme sehemu nyingi sana, watu wanaangalia sio tu kutusikiliza lakini wanaangalia kwenye vyombo mambo yote yanayotendeka humu. Sasa neno linaweza kuwa ni sahihi kwa mujibu wa Kamusi. Lakini Spika anawajibu katika kulinda heshima ya Bunge, kama neno hilo namna linavyotumika linaweza kuzua maana tofauti katika jamii. Basi Spika anawajibu kusaidia Waheshimiwa Wabunge ili tusionekane kama tunatumia neno ambalo kwa hakika kwa siku hizi na hasa kwa kizazi kipya, kusema kukazana, kukazana, ni neno ambalo halichukui maana nzuri. Utafanya jitihada, ongeza juhudi, tufanye jitihada, kwa nini usitumie hayo mengine ung'ang'anie kukazana kukazana tu. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mkumbuke siku ile lilipotumika, Mheshimiwa nilitaka tu basi nilimwachia tu lakini alikuwa analitumia kwa mzaha, kwa sababu alikuwa analirudia rudia kila sentensi katika namna ambayo ilikuwa ni kero kubwa kwa Bunge na hasa mahali ambapo watu wanajua vizuri Kiswahili kama Zanzibar. Maneno kama haya yanaleta kero. Kwa hiyo, Waheshimiwa sikupiga marufuku kwa sababu sina uwezo huo wa kuzuia na aina fulani ya Kiswahili. Kwa hiyo, tahadhari sana pale kunapokuwa na neno ambalo linaweza kuwa bora zaidi halileti maana chafu katika jamii basi tulitumie hilo kuliko kutumia neno ambalo linaleta matatizo, huo ndio ufafanuzi wangu. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007
### Wizara ya Kilimo, Chakula na Shirika.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa muda wa kuchangia hotuba yenye mipango inayohusisha suala zima la Kilimo katika nchi yetu ya Tanzania pamoja na masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kwanza niseme kwamba ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri wote wawili ambao wameshika dhamana hiyo ya kuendeleza masuala yote ya uzalishaji katika kilimo na masuala ya ardhi katika nchi yetu ya Tanzania. Lakini vilevile ninaomba nichukue nafasi hii kuwapongeza watendaji wa Wizara wakiongozwa na Katibu wao Mkuu pamoja na Kurugenzi zote zilizomo ndani ya Wizara hiyo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa Bajeti ya mwaka huu ya Kilimo, ninaomba na mimi nikiri kwamba imetoa picha na taswara nzuri sana ya kuendeleza kilimo katika nchi yetu ya Tanzania, na ninaomba niseme kama haya ambayo tumesomewa katika vitabu kama yatatekelezeka hivyo hivyo yalivyo, mimi naamini kabisa sasa hivi tungeweza kutangaza ushindi mkubwa sana katika mabadiliko ya Kilimo nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini hofu yangu kubwa ni utekelezaji, na tatizo kubwa katika nchi yetu linalotupata mara zote ni jinsi ambavyo tunaweza tukatekeleza mipango mizuri ambayo tumejiwekea. Wengi huwa wanasema kwamba mara nyingi tumekuwa wataalam wazuri wa kupanga lakini kutekeleza imekuwa ni tatizo kwetu.

Mimi kwanza napongeza juhudi za Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nakumbuka kipindi kabla hatujaanza kikao hiki cha Bunge alichukua hatua ya ziada ya kukusanya wakulima na wadau wa mazao mbalimbali ya biashara, na katika vikao vile tuliweza kupata muda muafaka wa kujadiliana na kupeana ushauri na kuweka mikakati itakayo tuwezesha kujivusha katika suala zima la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nisikitike tu, nilifikiri kwamba hata wale wazalishaji wa mazao ya chakula nao wangeitwa ili na wao waweze kutoa mchango wao katika hayo. Yako mazao mchanganyiko lakini yako mazoa makuu ya chakula katika nchi yetu na yamekuwa yakizalishwa na wananchi wa nchi hii ya Tanzania. Ninaomba nikumbuke wakati wa kikao chetu na wadau wa korosho nilianza kutoa uzoefu wa suala zima la ongezeko hili la ruzuku hiyo ya bilioni 7 hadi bilioni 21, na nikataka kuanza kuzungumzia ni namna gani tunaweza kuendeleza maeneo mengine kwa kwa kutumia uzoefu tuliopata kwenye suala hilo la ruzuku, lakini bahati mbaya niliambiwa pale sio mahali pake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nilikubali kwamba pale si mahali pake. Ninachotaka kusema ni kwamba kwa kweli Serikali imefanya jambo la maana sana kwa kuongeza ruzuku hii kwa ajili ya kuwasaidia wakulima. Tunajua ili wakulima na hasa wa mazao ya chakula waweze kufanikiwa suala la pembejeo, suala la masoko na suala zima la miundombinu mingine ya kilimo hayo ni mambo makubwa ambayo yanatakiwa kuangaliwa. Sasa suala la ruzuku limeangaliwa kwa kiasi cha kutosha na hasa ongezeko hilo kubwa.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ninakumbuka wakati tumeanza mpango huu wa ruzuku na hasa kwa ajili ya mbolea kwenye Mikoa ile inayozalisha chakula na hatimaye katika nchi nzima ya Tanzania, Serikali ilikuwa inataka kabisa kuona namna gani inajarabu kuwakomboa wakulima wa mazao ya chakula kama mahindi ili waweze kutengeneza ziada ya chakula kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya chakula katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Sasa namna ya kutumia ruzuku bado ni tatizo kubwa. Ni kweli kumeainishwa mipango mizuri sana katika hotuba hii, lakini mimi bado narudi pale pale katika mipango hiyo, hivi kwanini maana yake hii mipango yote tutaendelea kufanya majaribio. Tulianza awamu iliyopita tukaona kwamba tumekwama leo tumeingia na mipango mingine. Lakini kwanini Serikali haitaki kukubaliana na ushauri wangu wa kuona jaribio jingine liwe kutumia vyama vyetu vya Akiba na Mikopo. Mimi hilo bado kabisa nashindwa kuelewa kwanini Serikali haitaki kuona hilo ni kama jaribio jinginelo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kama inawezekana mniruhusu mimi kwenye Jimbo la Peramiho nimewaambieni nina *SACCOS* katika kila Kata. Hebu kwenye Jimbo langu mturuhusu tufanye majaribio ruzuku hii itumike kupitia vyama vya Akiba na Mikopo na si wale Mawakala. Miaka yote taarifa hizi, mikakati ya Mawakala na kadhalika kwenye vitabu inakuwa mizuri sana. Lakini utekelezaji hauonekani. Mimi naomba jamani hawa Mawakala tunategemea tutawapata wapya. Ni walewale waliozaliwa jana, juzi, wanaofanyakazi ni wale wale na mbinu zinabadilika kulingana na wakati. Kwa nini tusiamue jamani kutumia vyama vyetu vya Akiba na Mikopo. Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema anavielimisha ametoa fedha vitaimarishwa na kufundishwa, kwanini tusivitumie jamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi labda nisaidiwe kueleza katika hotuba hii, hiyo ruzuku ya shilingi bilioni 21, inarudi tena kusaidia ile asilimia 50 ya kusafirisha hiyo mbolea ama itapelekwa kupunguza bei moja kwa moja kwa mkulima kule kijijini? Mimi naomba hayo maelezo ndiyo tupewe basi, na kama itarudi tena katika kusaidia kupunguza asilimia 50 ya usafirishaji, hata tungekekaa vikao na malaika wakashuka kutoka mbinguni hapa pana shughuli. Kuna shughuli zito kabisa, labda sana sana kama ni wakala tuwatumie ndugu zetu wa *TFC* wasafirishe hiyo mbolea fedha hiyo itumike kama mkopo na ipelekwe kwenye vyama vya Akiba na Mikopo. Wananchi wapewe fedha mwaka mzima, fedha za kuwasaidia kukopa mbolea na hivyo wataweza kuzalisha vizuri zaidi, na tukizingatia suala la utalaam ukizingatia suala la masoko tutakuwa tumewakomboa wakulima wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri basi akubali kwenye Jimbo langu afanye majaribio ya kutumia vyama vya akiba na mikopo tukifanikiwa asambaze nchi nzima ya Tanzania. Nimesema kwamba ili kuendeleza kilimo ni suala pia jingine la msingi la kuangalia masoko. Sasa mimi nasema hivi, tunao huu mfuko huu wa stakabadhi za maghala, tumejifunza kwenye mradi wa Elimu ya Shule za Msingi MMEM. MMEM iliweza kusambazwa kwenye Halmashauri, kwenye Mashule huko vijiini na ikagusa kila kona ya nchi na tukafanya vizuri sana. Mradi huu bado uko katika maeneo machache, na sasa hivi tumesema tuko katika mkakati wa *Green Revolution*, tumesomewa hapa matrilioni ya fedha ambazo zitatumika kuboresha Kilimo nchini.

Kwanini tusiangalie suala hili stakabadhi tukaamua kutenga fedha kwa maksudi mazima zikapelekwa huko kwenye maeneo ya vijiji tukaimarisha maghala, tukaimarisha na mfumo huo wa stakabadhi za maghala ili kuwasaidia wakulima wetu kuuza mazao yao kwa bei inayotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani sasa ni wakati wa kuamua vitu hivi tuvifanyie utekelezaji, fedha tunazo na tumeona hapa mafedha tunayosomewa hapa yapo. Kwa hiyo, ni suala la kuamua kuwa na mpango ambao tuna uhakika utasambaa katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kule katika Jimbo langu Kata moja ya Mpitimbi imeingia katika mfumo huu wa stakabadhi za maghala. Mfumo ni mzuri sana, na tena sasa hivi mimi wameniletea homa kubwa kwenye Jimbo langu, kwa sababu wale walionufaika majirani wenzao wananiambia Mheshimiwa Mbunge umependelea. Kwanini ni Kata moja tu, sisi huku wengine tutafikiwa lini. Kwa hiyo, mimi nafikiri kwamba hebu tuangalie kwenye Serikali kwamba Serikali kwa mazao ya pamba na mazao ya korosho na mazao haya ya chakula tumbaku kahawa tuingie kwa nguvu kama mradi wa Shule za Msingi MMEM, tukafanya hilo katika nchi yetu nzima ya Tanzania, hiyo *Green Revolution* itaonekana.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini tukiendelea hivi kuamua kwa kusuasua bado tuna safari ndefu. Naendelea kusisitiza utekelezaji wa mipango hii ndiyo itakayowahamisha wakulima wetu kutoka katika suala zima la umaskini na kupiga hatua katika kuwaletea maendeleo endelevu ya suala zima la kilimo.Nakubali kabisa kwamba ajenda ya kilimo cha umwagiliaji ni ajenda ya kutiliwa mkazo sana katika nchi yetu ya Tanzania. Lakini mimi katika Mkoa wangu wa Ruvuma na niseme hususan katika Wilaya yangu ya Songea Vijijini Jimbo la Peramiho, tumekuwa na sifa za kuendelea kuongeza uzalishaji. Lakini mimi najiuliza, hivi kweli tunatakiwa kujisifia kwa kuongeza uzalishaji bila kujua hawa wanaozalisha wanazalishaje chakula kile. Hali bado ni ngumu wananchi wetu bado wanatumia jembe la mkono kila siku za maisha yao, na unapoona uzalishaji umeongezeka kuna watu wameumia na jasho limewatoka mpaka wametaka kufa kwa sababu ya kuongeza uzalishaji.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nafahamu kwamba tunayo mipango ya kilimo katika *DADP's* na mingine katika maeneo yetu. Lakini fedha zinazotengwa kwa mradi huo mmoja unaweza ukafunika miradi mingine mingi katika Halmashauri mmoja. Hebu tuamue tutenge Bajeti ya kubatilisha kilimo kile cha mkono tukiingize katika kilimo cha

matrekta na majembe ya kukokotwa na ng’ombe, na kipatiwe mpango maalum peke yake ukijitegemea. Serikali iamue kuweka mpango maalum katika nchi zima, usimame peke yake, ujitegemee ili ubadilishe kilimo hicho kutoka katika jembe la mkono kuingia katika jembe la kukokotwa na matrekta. Kweli kabisa inasikitisha nchi hii tutaendelea kuwa katika kilimo hicho cha jembe la mkono mpaka lini? (*Makofi*)

Suala la msingi ni mpango, kule Wilayani ni kweli tunaweza kujiwekea hiyo mipango lakini fedha zinazogawiwa kulingana na migawanyo hiyo ukisema uanzishe mpango huo kwa ajili la jembe la kukokotwa ua na trekta fedha ni nyingi itafunika miradi mingine. Kwa hiyo, wananchi wale hawatapata faida ya kupiga hatua katika maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mimi tayari tunao mpango wetu wa Wilaya wa kuhama kutoka kwenye jembe la mkono, lakini unahitaji fedha za kutosha. Mheshimiwa Waziri nitamwomba akubali nimkabidhi anisaidie kwenye hizo trilioni za fedha atusaidie hizo fedha tubadilike, halafu wengine waje wajifunze kutoka kwetu. Naona anafurahi pale nadhani amenikubalia na nitamkabidhi haraka sana jumatatu. Kwa hiyo, kwa kweli umuhimu wa kubadilisha suala zima la kilimo ni suala la msingi na ni suala ambalo tunatakiwa kwa kweli kulipa kipaumbele sana katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kabisa mimi niseme kwamba niiombe sana Wizara ione umuhimu wa kuimarisha vyama vyetu vya ushirika na hasa liko bado tatizo la mazao mchanganyiko kutokusimamiwa ipasavyo. Mazoa kama ya karanga, choroko, soya kwa kweli bado tuna matatizo makubwa sana. Kwa hiyo, tunaomba Wizara ione namna gani pia inaweza kutusaidia kusimamia mazao hayo ili yaweze kupatiwa masoko lakini yazalishwe kwa viwango vinavyotakiwa na yaweze kuwasaidia wananchi wetu kupata kipato na kuwasaidia kuongeza chakula na lishe katika nchi yetu ya Tanzania.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa kweli naomba nisisitize nimwombe Mheshimiwa Waziri apokee ule mpango wangu apokee na hiyo *proposal* ya wananchi wa Jimbo la Peramiho halafu atusaidie tuone namna gani tunaweza kuwa mfano wa kuhama kutoka jembe la mkono kuingia katika jembe la kukokotwa na ng’ombe na matrekta. Lakini vilevile namwomba sana akubali Jimbo letu la Peramiho kubadilisha huo utaratibu tutumie vyama vya akiba na mikopo ili pembejeo ziwafikie wakulima wote na tutalisha nchi nzima.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.(*Makofi*)

**MHE. MAGALLE JOHN SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kwanza kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili namimi niweze kuchangia katika Bajeti hii ya mwelekeo wa kazi za Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kutumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa juhudi mbalimbali alizofanya wakati wa kukabiliana na njaa wakati wa msimu uliopita ambapo Wilaya ya Maswa tulikuwa na

matatizo makubwa sana na namshukuru kwamba aliweza kufika Maswa pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu na kutambua shida na kutupatia msaada wa chakula. Nashukuru ahsante sana.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kutambua mchango wa Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa maoni mbalimbali waliyotoa ya kufaulisha kuundwa kwa Bajeti hii, nawapongeza sana. Vilevile napenda kuwapongeza wasaidizi wa Mheshimiwa Waziri kwa juhudi mbalimbali walizoshughulika hadi wakaweza kukamilisha Bajeti hii. Wahenga husema matofari hayajijengi bila ya kuwa na fundi mwashi. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itazame zao la pamba. Napongeza juhudi za Serikali na rai ya Serikali kwamba wakulima wa zao la pamba waongeze kilimo kutoka kilo 300 hadi kilo 1,000 ambazo zitakuwa ndiyo uwiano wa kilimo cha kisasa. Ili tuweze kuibua rai hiyo naomba Serikali itambue kwamba pana matatizo ambayo yanakwamisha motisha kwa wakulima wetu wa zao la pamba. Tatizo la kwanza ambalo linakabiliwa na wakulima wetu katika kujenga motisha ni mapunjo ya tofauti ya bei ya toka msimu wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itafute mkakati wowote ule wa kuwezesha wakulima walipwe mapunjo yao ya tofauti hizo, ni mamilioni ya pesa. Nasikitika kuiarifu Serikali kwamba wanunuzi wa zao la pamba walikuja Mkoa wa Shinyanga hususan Wilaya ya Maswa na ninauhakika hata Wilaya ya Bariadi kwa Mheshimiwa Andrew Chenge wako watu wanadai japo Mheshimiwa Chenge hawezi kusema kwa sababu ya itifaki. Nina uhakika Wilaya ya Kishapu, Meatu kwa ujumla niseme Wilaya zote za Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananunuzi wa zao la pamba, ilipoamuliwa na Serikali walipe ile tofauti ya mapunjo ya bei wanunuzi walipewa madai ya mapunjo ya tofauti ya bei. Mfano Maswa, kuna *SM Holdings* iliambiwa deni la malinganisho ni shilingi 4,627,885/-, ikaamua kulipa shilingi 1,480,085/-. *Jambo Oil mills* walikuwa wanadaiwa shilingi 62,605,810/-wamelipa shilingi 3,137,675/-. *Fresho Investment* shilingi 44,789,445/- wanalipa shillingi 2,305,725/- *Gaki Investment* wanadaiwa takriban shilingi 32,817,080/- wameamua kulipa shilingi 4,253,440/-. *Afrisian* wanadaiwa shilingi 52,848,070/- wanalipa shilingi 5,433,050/-, *Simon Agency* wanadaiwa shilingi 19,129,950/- wakaamua kulipa shilingi 1,718,600/- *S&C Ginning* wanadaiwa shilingi 2,731,231/- wakaamua kulipa shilingi 1,618,550/-, Hassanali Walji wanadaiwa shilingi 28,102,936/- akaamua kulipa shilingi 2,170,950/- na *CARGILL* wanadaiwa shilingi 89,103,345/- wameamua kulipa 26,071,050/- *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naiomba Serikali isimamie malipo. Malipo waliyoamua wanunuzi kulipa hayakusimamiwa katika malinganisho na Halmashauli ya Wilaya na hayakusimamiwa na Serikali ngazi ya Wilaya. Malinganisho wanunuzi wameamua wao wenyewe waamue wajilinganishie kulipa kiasi gani na hadi sasa imekuwa ni manung'uniko makubwa kwa wakulima. Tuna rai ya kuinua uzalishaji na uboreshaji wa

zao, lakini kero hii ni kubwa sana. Naiomba Serikali iingilie kati wakulima walipwe mapunjo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zao la pamba ni uti wa mgongo wa uchumi na ustawi kwa maendeleo ya wananchi wa Mkoa wa Shinyanga. Nasikitika sana pamoja na nia nzuri ya Serikali kuinua bei ya zao la pamba, nia hii nzuri sana imeondosha makato yaliyokuwa yanapelekwa kwenye Bodi ila yamebaki katika mfuko wa maendeleo wa zao la pamba. Naiomba Serikali ipitie upya uamuzi wake wa kutokatwa pesa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Elimu wa Mkoa wa Shinyanga. Ni kweli kwamba zao kuu la biashara katika Mkoa wa Shinyanga ni pamba, ni kweli kwamba jamii ya wananchi wa Mkoa wa Shinyanga kuna wafugaji, kuna wakulima na kuna wafanyakazi.

Lakini nia njema ya Serikali ingefaulu zaidi na zaidi iwapo utafiti ungekuwa umefanywa wa kina wa kushirikisha hata wakasikia sauti ya Madiwani ambao ni wawakilishi wa wananchi katika ngazi ya jamii. Je, wana mawazo gani?

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuja kuibua na kuzindua ari ya kujengwa mfumo wa elimu. Mkoa wa Shinyanga elimu ni duni. Mfuko wa Elimu wa wakulima katika Mkoa wa Shinyanga, umejenga sekondari 87. Nikirejea katika Wilaya yangu, katika miaka 45 toka tupate uhuru shule ya sekondari ya Serikali ni moja. Katika Mkoa mzima tuna sekondari 105. Juzi juzi tumeweza kujengwa sekondari 42 ambazo zimechangiwa na Mfuko wa Elimu wa wakulima. (*Makofi*)

Sasa kwa sababu mfuko huu umeondolewa, naiarifu Serikali. Pole haimwondolei mjane majonzi ya ukiwa wa ujane. Mtatupa pole sasa tutapata wapi mbadala? Naiomba Serikali itafakari kwa kina. Ushauri wangu kwa Serikali kuhusu suala hili naiomba Serikali kwa nia njema kabisa suala hili ilirejeshe kwa Wakuu wa Mikoa, ambako wakulima wanalima ili Wakuu wa Mikoa watafakari njia ipi itakuwa bora ya kupata mchango kutoka kwa wakulima. Tujadiliane na wakulima kwa uhuru wetu. Naiomba sana Serikali irejeshe hili ili tulifanyie *referendum*, twende vijijini tukashauriane na wakulima.

Mheshimiwa Spika, zao la pamba ninaweza kusema ni nishati ya kisiasa katika Mkoa wa Shinyanga. Zao la pamba na bei ya pamba inaweza ikatumika kwa maslahi ya kisiasa si kwa maslahi ya jamii, bali kwa kundi la watu. Kwa hiyo, naiomba Serikali ishirikiane na uongozi wa Mkoa wa Shinyanga, tutafakari jinsi gani ya kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, rai ya wakulima ni kuongeza kipato chao, kuongeza kipato cha kaya na rai ya wakulima ni kuhakikisha kwamba wanaondokana na adui ujinga, wanaondokana na matatizo ya maradhi. Serikali inahimiza wananchi wajichangie wao wenyewe. Tuna miradi ya *TASAF* ambayo jamii inapaswa kuchangia. Tuna utaratibu wa kuchangia pembejeo, tuna *passbook.* Ninaiomba Serikali itazame upya udhaifu na uzuri wa *passbook*. Azma ya *passbook* naiunga mkono kabisa na wakulima wanaiunga mkono.

Tatizo lililopo kila mwaka pana *passbook*, ajabu binadamu anapokwenda benki habadilishiwi *passbook* kwa sababu kaja leo, kesho aje na *passbook* mpya. Wakulima wanabadilishiwa *passbook*, *passbook* zinatengenezwa kwa gharama kubwa. Ninaomba Serikali itazame upya jinsi ya matumizi ya *passbook* na jinsi ya kufaulisha azma ya kuwa na *passbook* ili iboreshe, ihakikishe kwamba siyo mzigo wa kupoteza fedha za wakulima. *(Makofi*

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Serikali kwa kutoa ruzuku kwa mazao mbalimbali. Korosho wamepata ruzuku, kahawa wana *STABEX*, Chai wana *STABEX*. Je, wakulima wa pamba watapata ruzuku wapi sijaiona. Naiomba Serikali iwasaidie na kutambua jasho la mkulima wa pamba na matatizo mbalimbali waliyonayo hususan katika kipindi hiki cha kuboresha zao la pamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kupitia Bodi ya Pamba, wakague mizania za kununulia zao la pamba, udhalimu unaofanywa na soko huria ni mkubwa sana. Ninaomba washirikiane na Idara ya Vipimo na Mizani, wahakikishe wanapitia mizania. Wakulima wanaibiwa sana fedha katika mfumo wa soko huria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kuhusu suala la Ushirika. Naiomba Serikali pamoja na mkakati wa kutengeneza ushirika utakaoendana na mfumo mpya ambao ni wa azma ya Serikali ni vema wakafanya utafiti kupitia hata Halmashauri za kila Wilaya, wakaelezwa wananchi tuna maoni gani kuhusu matatizo ya Mfumo wa Ushirika uliopo.

Ushirika uliokuwa ni wa asilia wa *Victoria Federation* ulisimamia mambo mengi sana na uliundwa vizuri sana. Lakini baada ya Serikali kuvunja Ushirika wa *Victoria Federation* na kuanzisha Mfumo wa Nyanza pamoja na *SHIRECU* pana mapungufu ambayo sasa ni vema yakajulikana na pengo hilo likazibwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ishirikiane kufanya utafiti wa kupata maoni ya kitaaluma na vile vile maoni ya kijamii kwa kuzingatia mazingira ya kila mfumo wa ushirika unapo-*operate*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kifungu cha 50 ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni. Mheshimiwa Mbunge, aliyemaliza kuzungumza ameliambia Bunge hili kwamba Shinyanga tumejenga *Secondary Schools* kwa kutumia Mfuko wa Pamba. Huu ni uongo kabisa na ingefaa atoe uthibitisho huo.

Mheshimiwa Spika, tumewachangisha wananchi wa Bariadi na sehemu zingine na siyo kutumia Mfuko wa Pamba. Hela iliyoko ndani ya Mfuko wa Pamba inaliwa na watu ambao wasiojulikana na hili linajulikana ndani ya Serikali kwa hiyo, nilitaka hilo atoe uthibitisho au afute usemi wake.

**SPIKA:** Nitamwomba Mheshimiwa Mbunge, athibitishe, lakini na wewe pia itabidi uthibitishe usemi wako kwamba hela ya pamba inaliwa na watu. Mheshimiwa Magalle John Shibuda. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, nitaomba siku nifanye hivyo kwa sababu…

**SPIKA:** Kaa chini Mheshimiwa Mbunge. Unamsikiliza Spika na siyo kutafuta maslahi yako. Mheshimiwa Shibuda ebu thibitisha hilo.

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:**Mheshimiwa Spika, kama huna utafiti kweli, huna sababu ya kutoa hoja. Hapa nina taarifa ya kutoka *Shinyanga Regional Education Trust Board* ambayo inaelezea historia na mchango wa shule mbalimbali na ningependa nimwambie tu kwamba Upandagila maabara na bweni la wasichana lilijengwa kwa kuongezewa majengo mapya kutokana na Mfuko wa Bodi ya Wadhamini ya Elimu Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, ushahidi ninao hapa na shule zote nikiruhusiwa ninaweza nikazitaja, kwa ruhusa yako ili na yeye nimsaidie kuboresha uelewa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Bado unahitaji kuhoji Mheshimiwa Mbunge? Kwa sababu ipo karatasi ina orodha ya shule zote.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo ningependa niletewe ushahidi ulio kamili kabisa, unaoonyesha kwamba shule zote zilizojengwa katika mwaka huu zaidi baada ya juhudi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama zimejengwa kwa kutumia Mfuko wa Pamba. Mimi sikubali kwamba huo ni ukweli. Inaweza kuwa baadhi, lakini siyo alivyosema Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Subiri kwanza. Kwa kuwa kuna waraka ambao haujawekwa hapa mezani basi tutaomba suala hili tulimalize siku ya Jumatatu. Tutaomba vielelezo alivyonavyo Mheshimiwa Mbunge wa Maswa, vitufikie vitaweza kutoa mwanga wa jibu hili. Nadhani hili limekwisha. Hili la Mheshimiwa Cheyo kwamba hela za pamba zinaliwa na wajanja uthibitisho wake.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo kuhusu nini sasa, tunamaliza moja baada ya jingine wewe unataka mwongozo kuhusu nini? Spika amehoji kauli nzito sana ambayo imefika kwa wakulima wa Tanzania wote, kwamba fedha za Pamba Shinyanga zinaliwa na wajanja hatuwezi kuliacha hivi. Udhibitisho Mheshimiwa John Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, uthitibisho nitaomba nafasi, tuweze kuleta hapa matumizi ya Bodi ya Pamba ya Shinyanga, ambayo itaonyesha wazi kabisa hakuna uhusiano na yale yaliyosemwa na Mheshimiwa Mbunge.

La pili, kwa kuwa inaonyesha kwamba Mfuko huo mpaka leo hata Waziri Mkuu, anafahamu unahitaji kuangaliwa na kuchunguzwa kwa hali ya juu sana. Kwa hiyo, ni kitu ambacho ni kizito na itahitaji muda ili niweze kupata ushahidi wote. Lakini mpaka sasa hivi hisia ndivyo zilivyo. *(Makofi)*

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Msemaji alisema fedha zinaliwa na wajanja. Neno wajanja linawakilisha watu naomba awataje wajanja hao kwa maslahi ya wakulima kuwajua wezi wao ni akina nani? (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusiendeshe Mahakama hapa siyo utaratibu. Nitalifikisha suala hili kwa Kamati husika itachambua na itatupa ukweli uko wapi. Bunge halitasita kuchukua hatua kwa yeyote yule ambaye amediriki kuvunja Kanuni za Bunge kwa kusema uongo humu Bungeni. Tunaendelea.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 50 Mheshimiwa Mbunge, yeyote ambaye ana suala ambalo anataka kulidhibitisha anaweza akapewa muda wa kuweza kushughulikia suala hilo na kulileta Bungeni.

Kwa hiyo, nadhani ungempa muda Mheshimiwa John Cheyo na siyo kulipeleka kwenye Kamati husika. Baada ya kuwa ameleta uthibitisho wake na kama utakuwa hujaridhika na huo uthibitisho unaweza sasa ukatoa muda. Pili Mheshimiwa Shibuda katika uthibitisho wake amesema fedha za shule zimetoka *Shinyanga Education Trust Fund* na siyo kwenye Mfuko wa Pamba. Kwa hiyo, Mheshimiwa John Shibuda hajalithibitishia hili Bunge kwamba hizo fedha zimetoka katika Mfuko wa Pamba, bali zimetoka *Shinyanga Education Trust Fund*. Shinyanga *Education Trust Fund*

inachangiwa na watu mbalimbali *including private sector* kutokana na kodi na mambo kama hayo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Magalle Shibuda, hajalithibishia hili Bunge kwamba Mfuko wa Pamba, umejenga shule kwa mujibu wa juhudi za Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Nadhani taratibu kwamba Mbunge hawezi kuvunja uamuzi wako ambao umeshautoa sasa hivi. Mwongozo wako. (*Makofi*)

**SPIKA:** Tuendelee, nilikuwa nasimama, nimempa nafasi kwa sababu mtaona Spika, nanajaribu sana kuwasikiliza hawa Wapinzani, kwa sababu mara nyingi wanakuwa wepesi kulalamika kwamba wanaonewa.

Kwa hiyo, ni vizuri tukiwa tunawapa muda wa kutosha. Sasa kwenye hili mwongozo wangu ni tayari. Kwa kuwa mambo yote mawili yanayobishaniwa yanahusu Mkoa wa Shinyanga na kuna nyaraka ambazo zitaletwa, ni vizuri nyaraka hizo zifikishwe kwenye Kamati hiyo, ambayo nitaagiza ifanye kazi hiyo. Yote yatakuja hapa hapa halafu tutaona mwongo ni nani. Sasa tuendelee. Msemaji anayefuata, alikuwa bado Mheshimiwa Shibuda hajamaliza? Alikwishamaliza. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mbunge wa Vunjo CCM, atafuatiwa na Mheshimiwa Teddy Kasela – Bantu, CCM Bukene, wakati huo huo Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Viti Maalum Iringa, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie kwenye hoja ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Nianze kwa kuunga mkono hoja lakini nitazungumza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kupongeza Serikali ya Awamu ya Nne, kwa shughuli inayofanya kwa umakini. Nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kupata kura nyingi za kishindo, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, niwapongeze Mawaziri, niwapongeze Manaibu Waziri, niwapongeze Wabunge wenzangu kwa kupata kura nyingi za kishindo na kutuwezesha sisi kuwa hapa kwenye Bunge hili jipya lenye Ari mpya, Nguvu mpya na Kasi mpya. Vile vile niwapongeze wananchi wangu wa Vunjo kwa kuweza kunipa kura za kutosha nikawa sasa nawakilisha hapa Bungeni. Nawaahidi nitafanya kazi waliyonituma. (*Makofi*)

Pia niipongeze Serikali kwa hatua iliyochukua wakati mafuriko yaliyotokea Moshi Vijijini na Jimbo la Vunjo. Nampongeza sana Makamu wa Rais aliposikia kuna mafuriko alikuja kuwafariji wananchi na kutoa ahadi mbalimbali za misaada.

Nimpongeze vile vile Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa makini na kufuatilia aliweza kunipigia simu akaniuliza hali ya huko nikamwambia hali ni mbaya akaniambia Serikali imesikia na itachukua hatua na wakachukua kweli hatua. Walikuja Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Juma J. Akukweti, alikuja, pamoja na watendaji nashukuru sana kwa Serikali kuwa makini na kusaidia wakati wa maafa. (*Makofi*)

Pia niwashukuru wananchi kwa kuvumilia, pia nawashukuru Maaskofu wafuatao: Baba Askofu Amedeus Msalikie, kwa kutusaidia wakati wa mafuriko. Nimshukuru pia Baba Askofu Martin Shayo, wa Kanisa la KKKT, Dayosisi ya Kaskazini kwa kusaidia. Vile vile niwashukuru wafuatao: Karitasi walisaidia sana. Niwashukuru *Red Cross,* niwashukuru *TPC, UNDP, FAO* na wengine wote waliochangia kwenye maafa haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea kuchangia naomba kuzungumza yafuatayo. Jana wakati tunachangia hoja hii Mbunge wa Mbarali Mheshimiwa Estherina Kilasi alizungumza kwa machungu sana hapa. Mimi naomba niungane naye na hata Wabunge wenzangu jana nilikuwa nawaangalia walikuwa wanasikitika sana. Serikali vile vile niliona inatikisa kichwa kwa masikitiko.

Sasa kama tunaungana naye naomba kuzungumza yafuatayo. Mbarali yale mashamba nayafahamu. Serikali imetumia fedha nyingi kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji. Kuna nyumba za wafanyakazi, kuna magodauni, uchumi wa Mbarali ni yale mashamba.

Sasa kama Serikali imekwishakubali wananchi wauziwe ekari nne nne na ndiyo uchumi wa Mbarali, sijui imekuwaje. Serikali inageuka kinyumenyume na kwenda kuuzia watu binafsi. Kama watu binafsi wanataka kuanzisha mashamba mapori ni mengi waende kwenye mapori. Lakini Serikali kwa sababu inataka kusaidia wananchi wake iwauzie hayo mashamba kama tulivyokubaliana ekari nne, ili uchumi wa Mbarali uweze kukua kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. (*Makofi*)

Mimi naomba Serikali iwasikilize Wabunge, Wabunge wanawakilisha wananchi wao. Wabunge ni vipasa sauti vya wananchi. Wanapokuja hapa wanapotoa hoja Serikali iwe *serious* isikilize hoja za wananchi.

Mheshimiwa Spika, mimi nathubutu kusema kwamba pengine Serikali inapoingia mikataba na inaingia mikataba na wafanyabiashara huku inasema Serikali haifanyi biashara, lakini mikataba inaingia na wafanyabiashara, wafanyabiashara wanaingia mikataba ili wapate faida.

Tumeshuhudia Serikali ikiingia mkataba *IPTL*, imekuwa ni hasara, *Songas* imekuwa ni hasara, mikataba ya madini mingi imekuwa ni hasara, Meremeta hatari, *KADCO*, *Kilimanjaro Airport* wanalipa *US Dollars* 1000 kwa mwaka hasara. *TTCL* hasara. (*Makofi*)

Sasa Serikali ikubali kama kuna mahali imekosea tujisahihishe, wote ni binadamu. Tukikosea, tukubali tugeuke nyuma tufanye mikataba ambayo ina faida. Sasa hivi tunakodisha *TRC* naomba sasa Wabunge wa Bunge jipya, tuwe makini tuhoji hii mikataba Serikali yetu sasa hivi ambayo tunasema ni Serikali ya ari mpya, iwe makini tusije tukalalamika tena baadaye kama tulivyouza *ATCL*.

Sasa hivi wanatupa hasara, tunafidia, tunapeleka fedha za kuendesha *ATCL* hizi fedha ambazo tunapeleka *ATCL* sasa tungepeleka kwenye barabara. Ninaomba sana Serikali hii ya awamu mpya iwe makini namfahamu Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni mtu makini mambo haya yasirudiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba wakati wa majumuisho ya hoja hii ya Wizara ya Kilimo inategemea Serikali makini ambayo tunaifahamu itasema kwamba mashamba yale ya Mbarali yatauzwa kwa wananchi kila mmoja apate ekari nne nne na suala hili liishe wananchi wa Mbarali wafurahi wapende Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niendelee kuchangia kwenye masuala ya kahawa. Jimbo langu ni moja ya majimbo ambayo yanazalisha kahawa kwa wingi. Kahawa ni moja ya mazao ambayo yanatunisha mifuko yetu ya *foreign reserve*. Kwa hiyo, Serikali ina haki kabisa ya kuweka fedha nyingi kwenye haya mazao ambayo yanatuletea fedha nyngi za kigeni. *(Makofi)*

Sasa Serikali imeshaanza kwenye suala la kahawa, kuna miche mipya ya kahawa, kuna *Lyamungo Research Institute* ambayo inazalisha miche ya kahawa. Ningeomba Serikali itoe fedha za kutosha, ili taasisi ya utafiti iweze kuanzishwa katika kila kata, mashamba ambayo yatazalisha miche ambayo itagawiwa kwa wananchi ili waweze kuotesha hili zao la kahawa mpya ambayo hailiwi na wadudu na inazalishwa kwa wingi kwa kila ekari. (*Makofi*)

Vile vile niiombe Serikali itafute masoko mazuri ya kahawa na pia ijitahidi kuwaeleza wananchi watumie kahawa badala ya kuuza nje yote. Nchi zingine kama Ethiopia *90 percent* ya kawawa wanakunywa wenyewe. Sasa tuwaelimishe wananchi kwamba kahawa ni kinywaji kizuri tena kinywaji cha wapendanao, familia kama watakuwa na utaratibu wa kunywa kahawa, inawafanya wanafamilia wanakuwa karibu. Kwa hiyo, niwahimize Watanzania wenzangu tujifunze kunywa kahawa. (*Makofi*).

Suala lingine ni suala la ushirika. Ushirika nchi hii umekufa, ushirika umeingiliwa na mchwa. Mheshimiwa Rais alipokuwa anafungua Chuo Kikuu cha Ushirika na Biashara Moshi, tarehe 18 Machi, 2006 alisema kwa masikitiko makubwa kwamba

Ushirika umeingiliwa na mchwa, mchwa wana kawaida ya kula mbao, lakini alisema mchwa hawa walioko Ushirika wanakula mpaka bati. *(Makofi)*

Sasa Serikali kwa kupitia Wizara wamesema wanataka kukarabati Ushirika. Tuweke nguvu tuwe na ushirika wa kisasa ambao wananchi wanakuwa na imani na wao kuliko ushirika ambao umepita ambapo lazima tutafute dawa tupulize tuue hawa mchwa wote walioko kwenye ushirika sasa hivi. Tuanze upya tunahimiza *SACCOS, SACCOS* ni ushirika.

Sasa bila kuwatoa wananchi hofu kwamba tukiingia pia kwenye hizi *SACCOS* ushirika ule ule wenye mchwa wale wale. Sasa Serikali kwa kupitia Halmashauri itoe elimu na *seminars* kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kule kwangu tumeanza *SACCOS* za fedha na mazao. Unakopa kwenye *SACCOS* unakwenda kulima, ukilima ukivuna unapeleka magunia kama ni 10 unapeleka kwenye *SACCOS* wanakuwekea, wanakupa fedha kidogo unakwenda kutumia kama ni kupeleka watoto shule ada na matumizi mengine muhimu. Yale mazao yanabaki kwenye *SACCOS. (Makofi)*

Wakati bei imepanda wewe unarudi sasa kule kwenye *SACCOS,* kwamba naomba sasa muuze mazao yangu kwa bei kubwa sasa hivi. Wanauza mazao yale, wanaweka fedha zile kwenye *SACCOS* wanakata zile walizokupa. Kwa hiyo, sasa tuna- *encourage* Ushirika kwa njia ya *SACCOS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee pia kwenye kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji, kwenye jimbo langu tuna maeneo ambayo yanapatwa na mafuriko, lakini tungeweza tukafunga maji haya yakaingia kwenye mabwawa. *(Makofi)*

Tuna mito yenye mabonde makubwa kabisa. Kuna mto Wona, kuna mto mwingine unaitwa Muwe. Tukifunga yale mabonde tuka-*form* mabwawa baadaye tukajenga miundombinu ya kupeleka yale maji kwenye sehemu za tambarare kama Kahe Magharibi, Kahe Mashariki, Kirua Kusini, Kilema Kusini, tutazalisha mazao kila mwaka. Sasa hivi kwenye jimbo langu sasa hatuna njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**PIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge. Sasa Waheshimiwa Wabunge, namwita Mheshimiwa Teddy Kasela Bantu, CCM Bukene, atafuatiwa na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, CCM Viti Maalum, Mkoa wa Iringa.

Wakati huo huo Mheshimiwa Mgana Msindai, ambaye simwoni hapa, basi tutaendelea Mheshimiwa Mgana Msindai, kama hayupo Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, ajiandae.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu taarifa. Naomba nitoe taarifa kwamba hili linalozungumzwa kuhusu

mashamba ya Mbarali kwamba Serikali ilifanya uamuzi kwamba Serikali itagawa ekari nne nne kwa kila mwananchi katika Wilaya ya Mbarali, si kweli uamuzi huo haujafanywa hilo la kwanza. *(Makofi)*

Lakini la pili, tunakubaliana kabisa kwamba sekta ya Kilimo ili ipate mapinduzi yanayostahili lazima pawepo na wakulima wakubwa ndiyo maana Serikali kuna sehemu nyingine katika nchi yetu pamoja na Mbarali mashamba yale makubwa wameuziwa wakulima wakubwa ili kuweza kuchochea kilimo chetu nchini. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeruhusu hilo kwa msingi wa Kanuni zetu kwamba ni taarifa. Bahati tu ni kwamba alikuwa msemaji amekwishakaa.

Lakini ingewezekana kabisa ninaruhusiwa kwa Kanuni kusimama kutoa taarifa ingawa Kanuni inasema pia anayeongea wakati huo inabidi akubali hiyo taarifa itolewe. Lakini kwa kuwa alikuwa ameshakuwa ameketi basi nimeruhusu.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi nichangie hoja iliyopo mbele yetu yaWaziri wa Kilimo Chakula na Ushirika. Awali ya yote, napenda kuwapongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa jinsi inavyokwenda kwa Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ukitazama hotuba ya Waziri inayoeleza kilimo na inatupeleka kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM inayosema kwamba lazima twende katika kilimo cha kisasa ili tupate uchumi wa kisasa. Moja kwa moja hawajachelewa Awamu ya Nne wameanza kutekeleza. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nilikuwa nasikia uchungu sana ninapoangalia maji yanaelea ovyo ovyo na hakuna mtu anayeyavuna. Ukitazama kutoka hapa hapa Dodoma, nikiwa nakwenda kule nyumbani kwangu Bukene, unaanza hapa hapa Bahi, pana maji yanaelea hovyo hovyo, hakuna anayeyavuna. *(Makofi)*

Ukienda kule mbele mpaka utakuta Wembele, maji yanaelea hovyo hovyo, Mbuga ni nzuri sana.

Mheshimiwa Sika, ukifika kule kwenye Jimbo langu ndio usiulize! Mbuga ni nzuri! Maji ni mengi, tulikuwa tunashindwa kuyavuna na hata mimi mwenyewe nimeshapeleka watu kusoma pale *Sokoine University* kwa kuwa *Training of Trainers* ili waweze kuvuna maji ya mvua. *(Makofi)*

Lakini, kwa sababu walikuwa wakulima wa kawaida wamejua, wanashindwa kujiwezesha kwenda kufundisha watu wengine.

Kwa hiyo, ninaposikia tunaanza kuingia kwenye uvunaji wa maji ya mvua na tunakwenda kwenye kilimo cha umwagiliaji, kwa kweli nasikia furaha sana, maana mbuga zote unapopita zinakuita, zinakwambia njoo unilime. Kwa hiyo, ninafurahi na nawapongeza kwa kufikia hapo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijakwenda mbali, naomba nizame zaidi katika Jimbo langu la Bukene. Kwa bahati nzuri, nina mabwawa mengi yaliyoachwa na Wakoloni. Mabwawa haya, hata juzi nilipokuwa nazungumza kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, nimeyazungumza, lakini na sasa naomba nijikite katika kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mabwawa haya kama yatakarabatiwa kama wananchi wa Bukene walivyonituma niseme, kweli nina uhakika kwamba Bukene hatutakuwa na shida ya chakula na hatutakuwa na shida ya mazao ya biashara.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi tutajikwamua kwa kilimo cha kisasa na tutakwenda kwenye uchumi wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, naomba niyataje hayo mabwawa tena kwa utaratibu nakueleza hapa na pale kile kinachotakiwa. Nikianza kutokea Nzega kuingia katika Kata ya Shigamba, kuna bwawa pale Kagongwa naomba walikarabati kwani litawasaidia watu wa Kagongwa na wa Karitu kufanya kazi ya kilimo. *(Makofi)*

Vile vile, lipo bwawa lingine pale Itobo, naomba nalo pia likarabatiwe, liweze kufika katika hali ya kufanya kilimo cha umwagiliaji pale.

Kuna mabwawa kule Mwangoye ambako ndio hasa mpunga unalimwa zaidi mpaka Sigiri, naomba mabwawa yale yakarabatiwe na vile vile naomba mtaro wa Sigiri utengenezwe kwa sababu mtaro ule umewekwa na unasukumwa, *designer* anasema alimaliza kazi yake ikachekiwa na ikakubalika. *Contractor* naye anasema ametengeneza ule mtaro kufuatana na *design* aliyochorewa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, pale unakuta wananchi hawanufaiki na mtaro ule maji hayatemi kwenye mashamba. Kwa hiyo, tukiendelea na hii ya kuvuta kamba hapa na pale tunasukumana, *designer* na *contractor* na pesa zimeshachukuliwa, wameshalipwa watu, kwa hiyo, inafika mahali ambapo hatuwasaidii wananchi. Kwa hiyo, naomba Serikali itusaidie kutengeneza mtaro ule uweze kumwaga maji kwa wananchi ili waweze kulima mpunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile niende taratibu kutoka Sigiri kuja Igusule. Pale Igusule pana bwawa ambalo limekauka na halileti faida. Lakini karibu na *Igusule Railway Station*, pale Magharibi tukichimbiwa bwawa jipya, naamini kabisa tutapiga ndege wawili kwa jiwe moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lile bwawa la Igusule kama litajengwa au kuchimbwa litawasaidia watu wa Mwakata ambao wapo katika Jimbo la Uchaguzi la Msalala la Mheshimiwa Maige na vile vile litawasaidia watu wa Jimbo langu pale Ilalo, Sojo na Igusule yenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba bwawa hili lijengwe pale ili liweze kusaidia Majimbo mawili na hapo ndio sehemu yote hii ninayozungumza ya walimaji wa mpunga na hata sasa hivi ninapozungumza mpunga wote unaosikia unatoka kule kwetu Tabora, maana yake unatoka katika sehemu hiyo na katika Jimbo langu la Bukene. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukienda mbele kidogo, tena pale tunaingia Kata nyingine, kuna mtaro wa Malolo ambao Naibu Waziri alikwenda akauona tukauangalia wote pamoja ambao vile vile una walimaji wa mpunga. *(Makofi)*

Ukija mpaka Kisasiga, kuna bwawa lingine lipopale Itindwa limeharibika. Kwa hiyo, nalo linahitaji kukarabatiwa ili sehemu yote hiyo iweze kuwasaidia wakulima wa vitunguu na mpunga na vile vile kama tukiweza kupata kilimo cha umwagiliaji, maana yake tutalima mara mbili. Kwa hiyo, kama tukilima mara mbili, tuna uhakika wa chakula cha kaya na mazao ya biashara ya kuuza nje.

Mheshimiwa Spika, tukitoka hapo, tunakuja tena Uduka na Suti katika Kata ya Isagehe, kuna maji yanaelea ovyo ovyo. Hizi mbuga zote zikiweza kuwekewa mabwawa, naamini kabisa Bukene itakuwa sehemu ya amani, yenye neema na vile vile tutakuwa tuna chakula cha kutosha kwenye kaya na vile vile tutakuwa na mazao ya kutosha kuuza ili twende sambamba na ile falsafa ya kwetu ya kusema kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya, wakulima wapo na kama unavyojua mzigo mzito mpe Mnyamwezi, kwa hiyo, *no problem* tutalima. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza kueleza hayo, nataka kueleza faida ya mabwawa haya. Maana yake, tukishapata mabwawa haya, tutafanya kilimo cha umwagiliaji na kama tutafanya kilimo cha umwagiliaji tutalima mara mbili nimesema. Tutalima mahindi kwa ajili ya chakula chetu sisi wenyewe na tutalima mpunga na matunda kwa ajili ya kuuza.

Baada ya kupata mazao yote haya tunahitaji kitu kingine ambacho ni barabara ya kutoa mazao yetu kupeleka sokoni. Kwa hiyo naomba vile vile zile barabara zinazozunguka pale Mwalolo katika *irrigation,* Sigiri na hapa niliposema, Itobo, Itingwa,

Uduka na Suti nataka yawe mabwawa mapya. Kwa hiyo, katika sehemu hizi zote, barabara zitengenezwe tuweze kupeleka mazao yetu Tabora au Shinyanga na Mwanza na vile vile tupitishe Isaka kwa ajili ya kupeleka Burundi na Rwanda na hapo kweli tutakuwa tumeshajikwamua kiuchumi na tutakuwa tumeweka maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, tunalima, lakini tunahitaji mbegu bora vile vile. Kwa hiyo, naomba tuletewe mbegu bora na pembejeo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nafurahi ku-*support* wazo alilolitoa Mheshimiwa Monica Mbega jana tarehe 5 Julai,2006 kwamba*TFA* zifufuke. *TFA* yaani *Tanganyika Farmers Association*,zilikuwa zinafanyika katika sehemu kubwa zaidi kwamba zinakwenda Iringa,Njombe,Arusha na Moshi. Sasa naomba *TFA* zije mpaka kwetu ziweze kufika hata katika Wilaya kwa mfano Wilaya ya Nzega ziweze kuleta mbolea, mbegu bora, matrekta, maana yake sisi sasa tunalima na ng'ombe au jembe la mkono. Kwa hiyo, walete *idea* ya matrekta ili watu waweze kulima mazao mengi zaidi.

Kwa hiyo, naomba *TFA* zije pale na vilevile watuletee dawa ya kuzuia wadudu waharibifu (dumuzi) kwenye mahindi. Kwa hiyo, tukishaweza kuweka dawa yale mahindi yetu, naamini kabisa tutakuwa na chakula cha kaya na sisi ni mahodari kwa kuweka vyakula vikavu. Kwa hiyo, tutaweka vizuri. Vile vile, tuna ma-*godown* mengi sana na ushirika wetu wa Igembensabo.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze Igembensabo maana yake nini. Igembensabo ni jina la Kinyamwezi. Kwa Kiswahili, ni jembe ni mali. Kwa hiyo, naomba ushirika huo. Ushirika huo umeanza kufufuka, lakini naomba upewe msaada wa hali na mali ili uweze kununua mazao na kuweka katika ma-*godown*. Tunayo ma-*godown* mengi sana pale Bukene tuna ma-*godown* karibu kila Kata kwa ajili ya kuweka pamba na tumbaku na vile vile mazao mengine ya mchele na kadhalika. Kwa hiyo, Igembensabo naomba isaidiwe kwa hali na mali ili iweze ku-*take off* vizuri na kuwasaidia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba basi wale Maafisa Ushirika wasikae pale Ofisini Nzega tu, waje vile vile kwenye Majimbo kama ya kwetu watusaidie kufanya *SACCOS*. Watu wanataka *SACCOS*! Kuna watu wamewafuata pale Ushirika, kila mara huwaomba waje wawasadie kufanya *SACCOS,* lakini wanakuta hawaendi. Sijui kwa nini!

Kwa hiyo, naomba ushirika uje pale utusaidie tufanye *SACCOS* ili tuweze kupata mikopo ya Kuweka na Kukopa katika ushirika huu, tusaidiane na Igembensabo kuweza kununua mazao na kupeleka Dar es salaam, Mwanza, Burundi na Rwanda. Naomba yote haya tuyapate.

Mheshimiwa Spika, nafikiri nimemaliza. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Naanza kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kuweza kuandaa hotuba hii ambayo imeelezwa kwa kina. Nawapongeza Naibu Waziri wote, Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na Maafisa Kilimo wenzangu waliopo Vijijini wakifanya kazi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niipongeze Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara hii jinsi walivyoshughulikia tatizo la upungufu wa chakula uliojitokeza nchini na hususan maeneo mbalimbali katika Mkoa wa Iringa. Wananchi waliweza kupata chakula na kwa kweli Serikali iliahidi kwamba hakuna Mtanzania atakayekufa kwa njaa na kweli hakuna Mtanzania aliyekufa kwa njaa. Nawapongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, nikianza kuchangia, nianze kwa kukumbusha kwamba Mkoa wa Iringa ni mmojawapo ya Mikoa minne inayoitwa *the big four* katika uzalishaji wa chakula na kuweza kulisha nchi hii ukiwemo Mkoa wa Ruvuma, Rukwa na Mbeya. Kwa maana hiyo, Mikoa hii inahitaji kupatiwa pembejeo nyingi za kilimo. Tunaishukuru Serikali kwa jitihada ambazo wamekuwa wanafanya, lakini kwa kutegemea na mahitaji, bado tunahitaji kupata mbolea na pembejeo za kilimo kwa wakati. Sasa hivi karibu mwezi wa Nane unafika, pembejeo hizi hazijafika na zilitakiwa ziwe zimeshaanza kufika katika Mikoa yetu na kuanza kusambazwa.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Iringa ni mmojawapo kati ya Mikoa minne ya uzalishaji uliokuwa unafanywa na wananchi kwa kilimo cha jembe la mkono. Nafikiri kwa sasa kilimo hiki hakifai tena tunahitaji kulima kilimo cha kisasa, tunahitaji kulima kwa matrekta. Tunahitaji kulima kwa maksai, lakini yako wapi matrekta ambayo yatatuwezesha sisi kulima?

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na Vijiji katika Mkoa wa Iringa, naomba nivitaje. Kijiji cha Magulilwa kilichokuwa Kijiji bora kwa kilimo, Kijiji cha Lulanzi Wilaya ya Kilolo, Kijiji cha Makoga Wilaya ya Njombe ambavyo viliweza kulima kilimo cha kisasa na kuweza kuzalisha mahindi kwa wingi. Sasa ni wakati muafaka tuanze kufufua kilimo hiki na tujue kwa nini kilimo hiki kilikufa. Tujiulize, kwa nini Vijiji hivi sasa havizalishi kwa wingi? Tatizo ni pembejeo za kilimo!

Sasa tuna mabonde mengi katika Mkoa wa Iringa. Bado Mkoa wa Iringa unaweza kuendelea kuwa Mkoa wa uzalishaji wa zao la chakula kama tutazingatia kilimo cha umwagiliaji. Tunayo mabonde mengi, tunao Mto Lukosi ulioko katika Wilaya ya Kilolo ambao maji yake hatujayatumia vizuri.

Pia, kuna mradi ule wa *Traditional Irrigation Program (TIP)* iliyoko katika eneo la Mbuyuni, tunazalisha vitunguu kwa njia hii. Mradi huu pia unahitaji kuimarishwa ukiwemo na mradi wa umwagiliaji wa Nyanzwa katika Wilaya ya Kilolo.

Mheshimiwa Spika, tuna mabonde mengi katika Wilaya ya Mufindi ambayo kama tutayatumia kwa umwagiliaji, yanaweza kutusaidia. Tuna Mto Lugoda, njia panda ya kwenda Sadan. Kama eneo hili litaimarishwa, Vijiji vya Igombalano na Isalavanu

vinaweza kulima kwa umwagiliaji na ni hekta nyingi sana zinaweza kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Tuna maeneo ya mto Twagi, Mufindi ambao pia unaweza kusaidia Vijiji vya Kasanga kuweza kulima kwa umwagiliaji. Tunalo bonde la Manda kule Ludewa, nina uhakika kwamba Wizara ya Kilimo imeshaliangalia lile bonde.

Mheshimiwa Spika, lakini, nina uhakika kama tutazingatia maeneo haya kuweza kulima kilimo cha umwagiliaji, pembejeo kufika haraka, kujenga mabwawa, mabwawa haya yanaweza kutusaidia kuweza kupata samaki ili kuboresha lishe na tukaweza kujitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Spika, tuna mvua nyingi sana katika Wilaya ya Makete, karibu miezi saba au nane mvua inanyesha. Haya maji tunayatunza wapi? Kama tungeweza kujenga mabwawa kwenye maeneo kama haya na kutumia vyanzo vya maji kama nilivyoeleza jana, ku-*generate* umeme, tungeweza kuwa na viwanda vingi Vijijini na kuweza kuanzisha miradi ya kiuchumi ikiwemo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la usindikaji, nafikiri sasa wakati umefika, wakulima wakubwa Mikoa ambayo ni *the big four* sasa tuuze unga badala ya kuuza mahindi. Tuwe na mashine za kusaga Vijijini kwenye maeneo unakopatikana umeme, tusindike ili tupate bei nzuri na nafikiri tunaweza kufikiriwa kuuza vyakula katika Taasisi hizo zinazoanzishwa katika maeneo yetu tukaweza kuuza na kuweza kupata bei nzuri badala ya mahindi tunayolanguliwa, gunia linawekwa lumbesa. Lumbesa ni gunia moja ambalo limejazwa karibu yanakuwa magunia mawili na wananchi wanapunjwa bei. Sasa tunataka kuwa na kilimo cha kisasa, tusindike mazao sisi wenyewe, tuuze unga, badala ya kuuza mahindi.

Mheshimiwa Spika, hili pia naomba nitoe ushauri kwa chakula hiki ambacho tunatoa, ni vizuri pia tukaweza kutoa unga kwa sababu wakati mwingine unaipa familia kilo kumi za mahindi na Kijijini pale hakuna mashine. Kwa hiyo, hili nalo kama tutakuwa tunatoa chakula kilichosindikwa itaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya ugani, elimu hii haijawafikia wananchi wote. Wizara imekiri kwamba kuna upungufu wa wataalam wa kilimo, lakini mimi najiuliza kwamba mbona kila mwaka kuna wanafunzi wanaomaliza Chuo Kikuu cha *SUA* na hawana ajira? Kwa nini hatuwaajiri hawa wakafidia huu upungufu? Tuna upungufu wa wataalam wa kilimo, lakini tuna wataalam waliomaliza mafunzo hawajaajiriwa. Kuna hawa wengine waliokwenda Vyuo vya Kilimo wakapata Stashahada na Shahada kwa kujitegemea na wenyewe hawana ajira. Kwa nini hatuwaajiri hawa wataalam wakafidia huo upungufu?

Naomba Wizara ya Kilimo iliangalie hilo pia, lakini pia iwaangalie hawa watumishi wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Wataalam wa kilimo wapo katika mazingira magumu, wanafanya kazi na Vijiji wengine hawana hata nyumba za kuishi.

Kwa *package* hii nzuri niliyoiona humu ndani, sina uhakika kama na nyumba za wataalam wa kilimo waliopo Vijijini kama zimewekwa. Itakuwa ni motisha kama mtaalam akifika Kijijini kwenye ngazi ya Kata au kwenye Kijiji akiwa na nyumba apate mahali pa kujihifadhi. Hili nalo napenda Wizara iliangalie na pia kuwaangalia wale wanaofanya kazi katika mazingira magumu katika Wilaya ambazo zina mazingira magumu au maeneo ya Vijiji yaliyo na mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, tunaelewa kwamba wakati mwingine wanakuja kupata mishahara yao wanatoka Vijijini wanakaa pale kwenye Wilaya hawana posho wala kitu kingine cha kuwasaidia, hebu tuangalie hiyo *package* iendane na kuwamotisha hawa wataalam ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nishauri kwamba pembejeo hizi za kilimo zipitie kwenye *SACCOS* zilizoko huko kwenye maeneo yetu na tumesema hivyo na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamelizungumzia kwa kina. Utaalam wa kilimo pia uwakute hawa watu kwenye *SACCOS* zao, kwa sababu itakuwa rahisi Afisa kilimo kuwakuta wananchi wengi walioko kwenye *SACCOS* kuliko kumwendea mkulima mmoja mmoja. Tunaomba hizi nafasi zilizoko zitumike. Tutumie pia vikundi vya vijana, vikundi vya wanawake kupata elimu ili waweze kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Spika, nimekiangalia hiki kitabu chote, nikaona kwamba suala la jinsia hapa halikuzungumzwa kwa sababu limezungumziwa tu vikundi vya wakulima, lakini kuna wakulima wanawake, kuna wakulima vijana hawa, tunawapata wapi kama siyo kwenye vikundi vyao ambavyo ni rahisi kuweza kuwapatia utalaam? Tupewe pembejeo mapema kwenye vikundi na elimu pia iende kwenye vikundi vyetu. Elimu hii iendane pia na tafiti mbalimbali zinazotolewa. Wana Vijiji wengi hawajui hata mazao hayo yaliyofanyiwa utafiti, hawayaelewi ni mazao gani mapya. Tuelimishwe tuyajue ili tuweze kulima kilimo cha kisasa ambacho mazao hayo yatakuwa yana soko na kuweza kuondokana na umaskini ili kuhakikisha maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, zao la pareto ni zao mkombozi lililokuwa zao zuri katika Mikoa yetu, hasa Wilaya ya Makete. Zao hili ukiliangalia ni kwamba kilimo hiki kitafufuliwa. Tunaomba kilimo hiki kifufuliwe, pembejeo zitolewe mapema wananchi waweze kulima. Lakini pia wahakikishiwe soko lao kwa sababu pareto zao hazikuuzwa, wengine wanazo majumbani mpaka leo na wengi wao walikata tamaa.

Kwa hiyo, tunahitaji kuanza upya kufufua hili zao, kuwaelimisha wananchi na kuwahakikishia kwamba pareto yao itauzwa na bei nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie sasa suala la kuboresha mazao mapya ambayo yamezungumzwa katika kitabu hiki. Tumezungumzia mazao kama *vanilla* na tumesikia kwamba yanalimwa kwenye maeneo ya baridi. Tungependa kufahamu kama kwenye maeneo yetu wananchi wanaweza kulima. Kuna maeneo ambayo Mkoa wa Iringa, Wilaya ya Njombe, eneo la Uwemba maua yanalimwa na nimeona humu kwamba kuna kuboresha kilimo cha maua.

Ningependa sana Wilaya ya Njombe eneo la Uwemba kilimo hiki kiboreshwe. Nina uhakika Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba eneo la Uwemba linatoa maua mengi. Kama tutaimarisha kilimo cha maua katika Wilaya ya Njombe, ina maana pia tunahitaji kuimarisha Kiwanja cha Ndege kilichopo Njombe Mjini ili kiweze kutumika kusafirisha maua kwenda kwenye maeneo ambayo yanahitajika. Hili litakuwa ni ukombozi kwa wananchi kuweza kuhakikisha kwamba maua yao yanalimwa wakati mwingine yanakauka hayana soko. Hebu tuangalie kama tunaweza kuboresha kilimo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna Vituo vingi vya kilimo Mkoani Iringa. Tuna Kituo cha Kilimo cha Utafiti kilichoko Isimani, tuna Kituo cha utafiti kilichopo Njombe, viko viwili kule na tuna kituo cha kilimo cha utafiti kilichopo Ipogoro Iringa Mjini. Vituo hivi vimetelekezwa. Sasa vitafufuliwa lini? Tunaomba vifufuliwe vitumike kutoa mafunzo kwa ajili ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliongelea suala la Chuo cha Uyole kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha *SUA*. Nina uhakika kwa vile Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyosema, Mawaziri wanaohusika watatujibu, mimi nilipenda kupata majibu kwa vile Vhuo cha Kilimo Uyole ni Chuo kikubwa na kilikuwa kinazalisha mazao kwa wingi na Chuo hiki mimi nafikiri kama tukikigeuza kuwa Chuo Kikuu kinaweza kusaidia kuongeza wanafunzi wengi wanaosomea masuala ya kilimo na kufanya vijana wengi waweze kusoma na kujiendeleza na kupata shahada zao katika nyanja ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, eneo hili sasa hivi mashamba yale makubwa yanakodishwa kwa watu. Lakini kulikuwa kunazalishwa mahindi mengi sana katika eneo lile ambalo lina ekari nyingi. Ninaomba Wizara iliangalie hili eneo kama linaweza kuwekwa pia kwenye eneo la umwagiliaji tukaweza kupata mazao mengi ambayo kuna ekari nyingi pale zimelala tu, wakati tunakosa chakula. Ninaomba hili eneo liangaliwe, lakini pia uwezekano wa hiki Chuo kugeuzwa kuwa Chuo Kikuu pia liangaliwe kwa undani zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina uhakika kama tutayazingatia haya kuhakikisha kwamba *SACCOS* zinazoundwa, zinapata pembejeo na uzuri Wizara imeshatamka kwamba watawapa wakulima mikataba pembejeo na mbegu na kuwahakikishia mazao yao, mimi nina uhakika kama haya yatazingatiwa kilimo bora kitafikiwa, tutajitosheleza kwa chakula na maisha bora yataboreshwa. Pia, wale ambao hawana uwezo naomba waangaliwe ili waweze kupata pembejeo. Kuna familia ambazo haziwezi kununua pembejeo. Kuna familia za watoto ambao wanaojilea wenyewe, wapewe pembejeo waweze kulima na kuzalisha chakula cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Namwomba radhi Mheshimiwa Manyinyi, ile nafasi ya Mheshimiwa Mgana Msindai nampa sasa Mheshimiwa Fares K. Kabuye, Mbunge wa Biharamulo Magharibi (*TLP)*. Wote mtapata nafasi, lakini mtiririko umekuwa wa Wabunge CCM, nikaona ni vizuri hapa katikati aingie mmoja wa kambi ya Upinzani.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuongelea kilimo.

Mheshimiwa Spika, watu wanasema kilimo hawakijui. Kilimo wanaimba kilimo, lakini kilimo ni kazi ngumu sana. Ni kazi ngumu na kazi nzito na kazi ya kudharauliwa. Watu wengi wanaokwenda kwenye kilimo ni wale ambao wamekosa kazi, anaona hana la kufanya, anakwenda kwenye kilimo. Kilimo ni kazi ngumu sana!

Mheshimiwa Spika, naomba niwape mfano mmoja. Ukitaka kujua ugumu wa kilimo, nenda ukanunue jembe la mkono jipya uende kwa nguvu yako yote ukate, pale ulipokata uchukue futi upime sentimeta ngapi, utengeneze *square* sentimeta halafu uchukue ekari uibadili ziwe sentimeta, ugawie sentimeta ulizokatua, ujue mkulima kumaliza ekari atakuwa amepiga chini jembe mara ngapi. Hoi!

Mheshimiwa Spika, mimi watu niliozaliwa nao wakaenda kwenye kilimo, ukiwaona utafikiri ni baba zangu. Kilimo, hoi! Kilimo kweli ni kitu chenye heshima, ndicho kinacho-*support* maisha ya watu, lakini kilimo na waliolima wenyewe, wanadharaulika. Mtu mwenye shida duniani katika nchi zinazoendelea ni mkulima.

Lakini kilimo na wanaolima wenyewe wanadharaulika. Mtu mwenye shida duniani, katika nchi zinazoendelea ni mkulima. Wakulima pamoja na kudharauliwa katika Tanzania ndiyo wanaobeba mizigo mikubwa sana. Nenda kwenye hizi shule zinazojengwa, nenda kwenye kazi zote za kujitolea, wanaoshiriki ni wakulima. *DC* haendi kubeba mawe, Mkurugenzi habebi mawe, Mwalimu habebi mawe, Mganga habebi mawe, wanaobeba mawe kichwani na mchanga ni wakulima. Wanapoteza kazi zao kwa sababu tunafikiri kwamba kazi ya mkulima haina thamani. *(Makofi)*

Hivi mtumishi wa Serikali afanye kazi siku tano bila kulipwa ataweza? Kazi yako imelala! Huwezi kufanyiwa hivyo! Kila mara tunapiga kelele mishahara midogo, mishahara midogo! Lakini mkulima pamoja na kutokuwa na mshahara na siku zake nyingi anazozipoteza, hakuna anayemlipa! Kwa hiyo, wakulima tuna taabu! Bwana Shamba wanadharauliwa kama wakulima wanavyodharauliwa. Hawana heshima Mabwana Shamba Kijijini na mimi ni Mwalimu. Vijana wachache wanaochagua Ubwana Shamba kwa sababu wanaangalia Ubwana Shamba hauna heshima, kilimo chenyewe kwa kweli tumekitupa.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie kilimo na wanaolima waheshimiwe na wale wanaowatumikia Waheshimiwe na halafu wote tushirikiane. Hivi, kazi ya kujenga nchi Tanzania ni ya mkulima tu! *DC* hawezi kujenga nchi! Mwalimu hawezi kujenga nchi! Mkulima tu, ndiye mwananchi, wengine siyo wananchi! Hili tuliangalie. Kama ni kazi za kujitolea, mimi nafahamu Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, katika kujitolea ndiye alikuwa wa kwanza kukamata koleo na wengine wanafuata. Lakini sasa hivi mambo ya kujitolea yamebaki ya mkulima ambaye ni maskini.

Mheheshimiwa Spika, mkulima hana *ED*. Akilala, basi mambo yamelala. Mkulima hana pensheni, lakini huyo huyo ndio kwa kweli anayebeba mizigo ya kujenga Taifa hili. Naomba sasa niseme kwamba hivi kweli Tanzania tunalima na tunafanya kazi! Mshukuru mfumo wa nchi yetu, kama tungelikuwa na Majimbo kuna Majimbo mengine, yangelia. Tunakuja hapa kulilia kugawana sawa, lakini *contribution* yetu ni sawa? Chukulia Mkoa wa Kagera, utukufu wa Kagera kabla ya uhuru sisi tunauelewa. Lakini baada ya uhuru kile kilichozalishwa kwa kweli hakikwenda kusaidia wana-Kagera. Kwa mfumo wetu sio Kagera tu wala wazalishaji wote kwa kuwa tulikuwa tunaweka kwenye chungu kimoja, basi yule mgawa keki ndiye aliyekuwa anaamua agawie nani bila kujali wale wanaolima. Matokeo yake sasa hivi sisi watu wa Kagera tuko hoi.

Mheshimiwa Spika, mkoloni alikuwa ameacha lami kutoka Bukoba mpaka Chetema, ilifika mahali pa kukwanguliwa. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Magufuli na Serikali iliyopita kwa kutusaidia kwamba sasa tunaanza kupata lami. Mtu alikuwa anazaliwa mpaka anazeeka hajaona lami, alikuwa anasikia tu. Leo hii tunapata lami, lakini ungehesabu pesa ambayo imezalishwa na Kagera, unaweza ukaona kwamba kweli wana-Kagera kama sio kudhulumiwa, basi Mwenyezi Mungu anajua.

Mheshimiwa Spika, Kagera hatuna Hospitali ya Wilaya hata moja. Kagera shule tulizonazo ni zile zile zilizoachwa na Mkoloni. Labda Mungu bariki hizi shule ambazo ndiyo watu wanaziita shule za siasa. Ni watu wa kuhurumiwa tu! Wazalishaji wakubwa, lakini tulichokizalisha hatukukifaidi. Tunaomba tuangalie na hili. Watu wanasema Kagera wako juu, Kilimanjaro wako juu; hawakuwekwa juu na Serikali, ni juhudi zao wenyewe. Fanyeni hivyo Iringa, fanyeni hivyo Mtwara. Hakuna aliyewapa watu wa Kilimanjaro hayo waliyonayo, hakuna aliyewapa watu wa Kagera, ni juhudi zao.

Mheshimiwa Spika, niwachekeshe. Watu wa Kusini samahani, hili jembe la kilo tatu wanaita ngwamba. Hawawezi kulinyanyua. Sasa sisi tumenyanyua ngwamba, tumefika mahali sasa mnaona gere. Nanyi nyanyueni ngwamba, tushirikiane kuzalisha na tushirikiane kuendeleza nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli baada ya uhuru tulijitahidi kufanya maendeleo ya nchi yetu. Vyama vya Ushirika vilivyokuwa imara sana Kagera nakumbuka, Chama cha Ushirika cha Shinyanga kilikuwa cha kwanza katika *East Africa*. Sisi watu wa Kagera kama sikusahau tulianzisha Vyama tangu mwaka 1927 vika-*survive* mpaka tumepata uhuru. Lakini kwa sababu ambazo mimi siwezi kuzijua, tulipopata uhuru Vyama vyote vikawa vimesimama. Zile Halmashauri zilizokuwa zinajitegemea na ni Halmashauri kabisa, zikasimama.

Mheshimiwa Spika, kilichozaliwa baadaye ikawa ni Vyama vya Ushirika vya kutengenezwa na Serikali. Chama cha Ushirika hakitengenezwa na Serikali, kinatokana na uchungu wa unyonyaji wa wakulima wanaozalisha. Hakitengenezwi, tulivianzisha kwa uchungu wa Wahindi waliokuwa wanatunyonya. Lakini hivi Vyama vya kutengenezwa vinakufa. Unatengeneza Chama kwenye mikopo. Serikali inabidi itoe pesa kwa sababu imetengeneza hicho Chama na wananchi hawakuvithamini. Walivijua

ni vya Serikali. Halmashauri tulizonazo, hazina *autonomy*. Ni Halmashauri gani inategemea kupewa na Serikali?

Hivi kweli mbona tunalalamika kwamba tumekuwa tegemezi wakati pengine tunapewa madeni?! Sasa Halmashauri zinazoitwa Serikali zinategemea kumegewa na Serikali Kuu! Hizi siyo Halmashauri, ni Idara za Serikali, haziwezi kutusaidia kilimo. Haziwezi kusaidia!

Halafu juzi, mmeona Mikoa yetu inapitana kwa ukubwa na kwa uwingi wa watu. Lakini milioni 500 kila Mkoa! Kitu gani tunafanya, tunaogopa watu! Kama wewe Mkoa wako ni mdogo, chukua kidogo. Mkoa mkubwa upewe kikubwa! Hivi tunaogopana, fulani atanung'unika, hanung'uniki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Mikoa *giant* sitaki kuitaja imepata Shilingi milioni 500, kamkoa kadogo, sitaki kuutaja, Shilingi milioni 500, tunafanya vitu gani? Kwa nini tusiende kufuatana na hali ilivyo? Tumetoka huko tukajifunza, kweli kilimo tukakipa heshima.

Mheshimiwa Spika, tumeanzisha mashamba *NAFCO*, tumeanzisha *National Milling*, kwa kweli Watanzania tukawa na chakula na tuliheshimiwa. Maghala yakajengwa ya ajabu, yote yakajaa vyakula, Wilayani na kila Kijiji kukawa na maghala. Kwa kweli nchi yetu ikaneemeka!

Mheshimiwa Spika, tulifika mahali, ujamaa nao ulikuwa mzuri. Kila kitu kina faida na hasara. Baada ya ujamaa kufa, sasa wale waliokuwa wanasema jamaa damu damu, mimi nafikiri walimwogopa Marehemu hawakuwa wajamaa.

Mheshimiwa Spika, hao hao baada ya kusema sasa tunarudi kwenye ubepari, yamezuka ndugu yangu ni hatari kabisa, kama yale manyang'au ya Kenya yaliyokuwa yanasemwa na Mtukufu Rais Mwalimu Nyerere. Sasa unajiula wale waliokuwa wanasema ni wajamaa damu damu wako wapi? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *NAFCO* imekufa, *National Milling* imekufa, masirika yote yaliyotengenezwa na wananchi wa nchi hii yamekufa. Sasa tunatafuta wawekezaji waje tuwagawie na watakuapisha tu. Kuja kuwekeza, tunawapa! Tumekwenda Ulaya kwa wakubwa wa uwekezaji. Sisi tuliapishwa! Mzungu anasema ninyi Watanzania mtatutengenezea umaskini mpaka lini? Watu wetu wamekuja na pesa wamewekeza wamekuwa matajiri, mmewanyang'anya kila kitu, ndiyo maskini wanaoombaomba. Mnataka tena tuwaletee watu wawekeze mje muwanyang'anye tena. *(Kicheko/Makofi)*

Mwingine alikuwa Arusha nikakutana naye akasema ninyi wabaya, mlitaifisha mpaka na shanga za mke wangu. Nikamwambia, wewe Mzungu, shanga zilitaifishwaje? Akasema nilikuwa Nairobi nafanya *picknick* na mke wangu, kurudi nyumbani, nyumba imezingirwa na Askari na mashamba. Bwana Kabuye niliingia ndani kuchukua changu! Nikampa pole. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ndugu zangu naomba Serikali chini ya ndugu yetu Waziri wa Kilimo, mimi ninamfahamu sana, jamani mfanye kazi kwa sababu tunawafahamu. Mzembe tunamjua, mchapakazi amepewa tunamjua. Kwa hiyo, fanyeni kazi kwa bidii, maana wewe Kabuye kama ulikuwa Waziri miaka 10, tunajua huwezi, ukajigeuza, lakini tunataka na wewe ujitahidi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tumaini siku moja, Rais Mstaafu Mkapa, alisema, mimi nimeingia sasa nataka Shilingi moja inunue kitu. Maskini ametoka sio shilingi moja isiyonunua kitu, hata Sh.20/= hazinunui kitu. Sasa mnaposema tumebarikiwa, fulani ni Rais, nasema aah! Tuangalie kwanza kwa sababu tunawaelewa mlikuwepo na Kabuye alikuwepo, sasa nitajizaa!! Tulikuwemo, kwa hiyo, tunataka tuwaelewe kwa matendo na wala sio kwa sura na kujitapatapa. Mfanye kazi wananchi watawasifu. Fanyeni kazi na mtu anayetaka kufanya, hasemi. Kenya wamefika huko, mlishasikia kuna MKUKUTA Kenya. *(Kicheko)*

Kaa chini sema, waone matendo. Lakini MKUKUTA, MKUKUTA. Mnajua MKUKUTA kwetu KUKUKUTA ni kula kwa ulafi. Kwa hiyo, hii MKUKUTA, hizi pesa Shilingi milioni 500, ngapi huko watazikukuta na Watanzania tutabaki hivi hivi. Kwa hiyo, nawashukuru sana, fanyeni kazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ndugu yangu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo sina tatizo naye. Kwa hiyo, ni haya niliyotaka kuzungumza. kwamba waheshimuni wakulima, ndiyo watu walio hoi kabisa. Hawana *ED*, hawana pensheni, wakiugua, kwisha! Wakifa, kwisha! Wanachanika nyayo haki ya Mungu na tetenasi haiingii. Safura, nyayo zinachanika, Mtanzania! Uhuru miaka 45, mnayo kazi Waziri Mkuu. Anayo kazi Mheshimiwa Rais, mnayo kazi Waheshimiwa Mawaziri na wala siyo maneno ya MKUKUTA na MKURABITA. Fanyeni kazi watu waone.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, nakushukuru sana. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge, Spika anapenda kuchanganya, maana yake ni lazima tusikie na upande mwingine. Namwita sasa Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini CCM, atafuatiwa na Mheshimiwa Adam Kigoma Ali Malima, Mbunge wa Mkuranga CCM, wakati huo huo Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbeya Mjini CCM ajiandae.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hii Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Waziri wa Kilimo kwa hotuba yake nzuri ambayo kwa kweli kwa yeyote anayeweza kusoma kitabu hiki ni hotuba inayoonyesha au inayoashiria matumaini makubwa katika mapinduzi ya

kilimo. Kusema kweli yamezungumzwa mambo mengi ya msingi na hotuba hii imejikita zaidi katika utekelezaji wa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi mazuri ambayo yamezungumzwa na hii hotuba imesisitiza kwamba kilimo cha kisasa ndiyo msingi wa uchumi wa kisasa. Lakini vile vile tumeweza kuangalia katika hotuba hii kwamba kuna mambo mengi na makubwa ambayo yanategemea kufanyika katika huu mwaka wa fedha 2006/2007. Kwanza ruzuku ya mbegu pamoja na mbolea kutoka Shilingi bilioni saba hadi Shilingi bilioni 21. Lakini vile vile mbolea inaongezeka toka tani 63,000 mpaka tani 129,000. Programu ya kilimo katika kipindi cha miaka saba imetengewa Shilingi trilioni 2.5. Kuna suala la mageuzi ya ushirika kwa mwaka huu tu zimetengwa fedha Shilingi bilioni 4.7.

Mheshimiwa Spika, haya yote ni mambo mazuri ambayo yanayoonekana katika hii hotuba ya Waziri wa Kilimo na kwa kusema kweli sio mwaka huu tu, lakini hata katika miaka mingine mambo haya yamekuwa yakionekana. Lakini tuna jukumu, sisi kama Watanzania tujiulize hivi ni kweli mipango hii mizuri ambayo imezungumzwa katika muda mfupi wa mwaka na kuendelea tunaweza kuyaona matokeo yake? Nadhani hilo ni swali la msingi ambalo tunahitaji kujiuliza sisi kama Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia tu, mfano wa mwaka 2005 katika hotuba hii tumeona zaidi ya Shilingi bilioni 30 zimeelekezwa katika maendeleo ya kilimo. Lakini pamoja na fedha hizi kuelekezwa huko, bado *impact* yake katika Taifa haikuonekani na tatizo la kilimo limeendelea kuwa kubwa kwa maana ya tatizo la chakula mwaka hadi mwaka. Katika hali hiyo, sasa mwaka huu zimetengwa hizo fedha kwenye maendeleo ya kilimo sio chini ya Shilingi bilioni 45.

Mheshimiwa Spika, ombi langu basi ni kuiomba Serikali sasa iweze kuangalia fedha zaidi safari hii ziende kule chini kwa mkulima. Maana fedha zinaweza zikawa zimetengwa lakini hizi fedha zinaishia huku juu Maofisini. Kwa hiyo matokeo yake ni kwamba hata ile *impact* sio rahisi sana ikaonekana. Kwa hiyo, itakuwa ni watu wa kuzungumza kila siku lakini pasipokuwa na matokeo yoyote. Ni vizuri sasa tuendelee kama ambavyo tunasema kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo kwa kweli kinachohitaji kuonekana ni matokeo.

Mheshimiwa Spika, tafiti nyingi zimefanyika na inawezekana hata fedha nyingi zinaishia kwenye masuala ya upembuzi yakinifu na matokeo yake fedha kiasi kidogo sana kinaweza kuwafikia wale wakulima wetu. Niombe basi hasa kwa kutumia hawa wataalam wetu, pamoja na sisi wenyewe kama viongozi, ni vizuri basi hizi tafsiri na utaalam wa kilimo sasa uendane na hali halisi ya mazingira yetu tunayoishi. Maana siku hizi utaalam mwingi umekuja, watu wanaingia kwenye *internet*, ukimwambia akutengenezee *feasibility study* anaingia kule anakuletea, lakini unakuta ukienda kwenye hali halisi ya mazingira yetu ni vitu viwili tofauti. Ndiyo maana mwaka hadi mwaka bado matokeo yake hayaonekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ushauri wangu sasa kwamba kati ya mambo ambayo tunahitaji kuyafanya ni vizuri tufahamu hili kwamba mchango wa Wataalam unahitajika sana katika kuendeleza na kuboresha kilimo. Lakini vile vile na sisi kama Viongozi ni

vizuri tukatumia nafasi zetu hasa katika maamuzi kwa maana kama wanahitaji wafanye kazi yao ya kutushauri. Lakini pale tunapofika katika maamuzi, basi ni vizuri tukatumia busara zetu zaidi kuamua. Nami ninachoweza kusema hapa ni kwamba nimeona maamuzi mengi yetu sisi hasa wanasiasa kwa kweli wakati mwingine yamekuwa yakileta zaidi maendeleo haya ambayo tunayazungumza kuliko pale tunapochukua ule uamuzi au ushauri wa kitaalam na huo huo ndiyo tutaendelea nao mpaka mwisho bila kuongezea nafasi zetu, basi tunajikuta mambo mengi yanabaki kama yalivyo.

Mheshimiwa Spika, labda ni vizuri nikatoa baadhi ya mifano michache ambayo uamuzi wetu wa kisiasa wakati mwingine wenzetu wamekuwa wakiuona sio mzuri sana, lakini umetusaidia hasa katika nchi changa kama hii ya Tanzania.

Nakumbuka mwaka jana kwa maana ya mwaka huu mwanzoni tumepata hili baa la njaa. Hili baa la njaa naamini kwamba tulifika tu mahali wakaona kwamba hatuna jinsi, lazima tuamue sasa kuhakikisha kwamba chakula kitafutwe watu wetu waweze kupata chakula ili wasife na njaa.

Mheshimiwa Spika, lakini ninaamini, laiti kama tungewapa nafasi kwamba hebu watushauri, hadi leo watu wangekuwa wanakufa na chakula kingekuwa bado hakijatafutwa. Lakini sio hilo tu, hata zoezi lenyewe la ugawaji wa chakula naamini na sisi wote ni mashahidi, Waziri Mkuu aliamka akatembea kila mahali.

Katika ile Mikoa yote ambayo hicho chakula kimekuwa kikienda baada ya utafiti wao kuja na Serikali nayo ikaamka na baada ya uamuzi huo kuwa umechukuliwa, lile zoezi la kupeleka chakula haraka katika yale maeneo husika limekwenda kwa wakati. Hali hiyo basi ikaweza kunusuru Watanzania wengi ambao sasa walikuwa wanaelekea katika hali mbaya ya kimaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sio hilo tu, hata huu uamuzi aliouchukua Mheshimiwa Rais wa kujenga Chuo Kikuu katika Mkoa huu wa Dodoma, mimi naamini laiti kama angelisema tu kwamba sasa tunataka kujenga Chuo Kikuu, kwanza huu utafiti, huu upembuzi yakinifu, ungechukua miaka mitano mpaka Chuo Kikuu kijengwe. Lakini kwa kuwa Rais alisema tunataka Chuo Kikuu kijengwe na mwisho akasema hiki Chuo Kikuu kijengwe Dodoma, basi zoezi limekwenda haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naamini sio hivyo tu, baada ya kuwa amesema, naamini vile vile amewashirikisha viongozi wa kisiasa wa Mkoa huu, akiwemo na Mkuu wa Mkoa kwamba tunahitaji kiwanja na ndiyo maana haukupita hata mwezi tayari tukaambiwa kiwanja hiki kinahitaji kujengwa Chuo Kikuu.

Kwa hiyo, hivyo ndivyo na mimi nawashukuru ndugu zetu wanasiasa na sisi kama viongozi, hebu basi pamoja na ushauri mzuri wa wataalam, wakati mwingine na sisi tuchukue nafasi zetu baada ya kuwa tumepata zile *inputs* zao tuweze kuamua ili mambo yaweze kwenda kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nitoe mfano mwingine wa pili. Wakati matokeo ya Darasa la Saba yametoka, sisi wote ni mashahidi, karibu asilimia 45 peke yake ya wanafunzi ndio waliokuwa wamechaguliwa kuingia Sekondari. Mheshimiwa Waziri Mkuu akasimama akasema hebu tuhakikishe watoto wote wanakwenda Sekondari. Kwa muda mfupi, zoezi hilo kwa kuchukua huu uamuzi wetu ambao wenzetu wanauita wa kisiasa, leo sio chini ya asilimia 70 ya watoto wetu wako Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunachokifanya sasa ni kurekebisha yale mapungufu yaliyopo. Nami niwahakikishieni ninyi ndugu zangu, leo tukikubaliana hata tukachukua Shilingi bilioni mbili tukawapa tu hawa wataalam kwamba hebu anzisheni shamba la mfano hapa na shamba hili sasa liwe linajiendesha lenyewe, tukianzisha mashamba kama hayo 10 zaidi mashamba yatakayoendelea ni mawili au ikiwezekana moja, mengine yote yatakufa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndiyo maana nahitaji kuwapa tu changamoto hiyo kwamba kumbe basi uamuzi wetu ni uamzi ambao unatakiwa sana. Ni vizuri sasa tukawa na utaratibu wa mashamba ya mifano, mashamba haya angalau yakawepo hata katika Kanda hata kimkoa, kwamba, basi haya mashamba yatengewe kiasi cha fedha kama ni Shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Spika, hii inakupa nafasi hata Mheshimiwa Waziri Mkuu anajua anaweza kumbana Mkuu wa Mkoa anambana *DC* pamoja na wale wataalam ili waweze kuonyesha mfano. Maana tatizo kubwa ambalo limekuwa likijitokeza linaonekana kumbe hiki kilimo sasa ni kama cha kufikirika hivi. Kwa sababu hakuna mahali ambapo tunaweza kwenda leo tukashuhudia hiki kilimo kwamba kweli mahali fulani kilimo cha mfano kipo na hata haya mashamba ya mifano yanayotolewa ni yale ambayo kila mwaka yanapewa ruzuku.

Mheshimiwa Spika, tunachohitaji ni kwamba litengwe eneo ambalo, hilo shamba likishaanza liweze kujiendesha lenyewe. Hivyo ndivyo watu wetu wengi wanaweza wakaenda na wakajifunza kutoka huko.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni vizuri sasa tungewashirikisha wananchi, kwanza kwa kuwatafutia zana bora za kilimo. Leo Waziri Mkuu akitafuta matrekta au Serikali ikitafuta matrekta wakaja wakawahusisha wananchi kwa maana ya wakulima, hata wakichanga Shilingi laki tano, wakulima ishirini wanapata Shilingi milioni kumi. Serikali inawakopesha Shilingi milioni kumi nyingine, milioni 20 tayari trekta. Tunaweza kupata matrekta mengi kwa kadri tuwezavyo na haya matrekta yakawasaidia hata wale wakulima wa chini wakaweza kulimiwa. Lakini tofauti na hapo kwa kweli hatutaweza kukidhi hili tatizo la wakulima ambalo kwa kweli linaonekana kuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni vizuri sana hii ruzuku ya pembejeo ikawa na utaratibu mzuri, ikaelekezwa katika maeneo yote. Maana leo kwa Mikoa kama ya Kanda ya Ziwa, Mkoa kama wa Mara, nisemee Mkoa ambao ni wangu, hizi ruzuku za pembejeo ni ruzuku tu wanazozisikia wala hawajawahi kuziona, wala hata hawaelewi zinatolewaje. Kwa hiyo, ni vizuri hasa upande wa mbolea, basi kile kitengo chetu aidha kianzishwe

kitengo maalum ambacho kitakuwa kinasambaza hizi mbolea kuliko zinavyouzwa na watu kiasi ambacho hata bei inakuwa ni kubwa, ambayo kwa kweli hakuna anayeweza kuimudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikushukuru kwa hayo, lakini niombe basi Serikali ni vizuri zaidi sisi Watendaji kwa maana ya sisi viongozi tukatumia nafasi zetu kwa maana ya maamuzi kuliko pale tutakapochukua ushauri kama ulivyo na huo ushauri tukaupeleka kwenye *implementation* kwamba hatutaweza kukidhi hii tija ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kusema tena katika Bunge lako Tukufu na naomba niungane na wenzangu kuwapongeza Mheshimiwa Mjomba wangu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Joseph Mungai na Manaibu wake, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje na Mheshimiwa Christopher Chiza.

Mheshimiwa Spika, pia naomba katika maandalizi ya hotuba hii niwapongeze Katibu Mkuu, Peniel Lyimo na Watendaji na wahusika wote wa Kilimo nchi nzima kusema kweli kazi ni kubwa wanayotakiwa kuifanya na lazima tutambue hivyo.

Mheshimiwa Spika, sijui kama ndivyo ilivyo au ndiyo mipango ya kila siku, lakini miundombinu na kilimo ndiyo vitu ambavyo kusema kweli ndiyo *most visible indicators* ya tunatoka wapi na tunakwenda wapi kwa mwananchi wa kawaida. Ndiyo vitu anavyoweza kujitambulisha navyo kwa namna ya moja kwa moja. Kusema kweli Chama changu, Chama cha Mapinduzi kimeshaweka katika Ilani ya Uchaguzi ambayo iko kamili kabisa. na ambayo ni mwongozo tosha kwa Watanzania wote kuifuata na katika hilo nakumbuka ile kauli ya watu wa Nabii Musa alipoletewa Msahafu mbadala, wakasema tunataka Msahafu mbadala wa nini wakati Msahafu wa Musa unatutosha?

Sasa na mimi katika hilo nataka niseme naamini kabisa kwamba tukijifunga katika Ilani ya Uchaguzi na Chama cha Mapinduzi na Serikali na Watendaji wakijifunga katika hilo na malengo na mwelekeo uliowekwa katika Sekta za kilimo na miundombinu na tukafanya jitihada ya pamoja, *everybody* kusema kweli, mimi naamini kwamba tutakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili, naamini kabisa kwamba sisi ni Wabunge na Wabunge wa Chama chetu na Chama chetu kinatuma na wananchi wetu wametutuma, kwa hiyo pamoja na maneno mazuri ya pongezi yaliyosemwa na wenzangu wote lakini mimi naomba niseme maneno machache na kusema kweli mimi naamini kwamba pamoja na uzuri wa *document* hii, mimi naamini kabisa *it could be better*. Naamini kabisa kwamba tunaweza tukapata nzuri zaidi, sio kama haiko kamili lakini ingeweza kuboreshwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, nasema hili kwa sababu kama nilivyosema kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu, tulisema Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya, ni kitu ambacho tunataka sisi wote tuone mabadiliko katika sehemu zote. Kwa hiyo, hata katika hili la taarifa na hotuba ya Waziri mimi nilikuwa natarajia kwamba nilipolinganisha ile ya mwaka 2005na hii nimeona *some slide difference* lakini nafikiri *it could be better.* Nalisema hili kwa sababu bado naamini kwamba kazi ni kubwa lakini kwa uwezo wa kihistoria na wakitaalam tuliokuwa nao tungeweza kutengeneza *document* nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu katika mambo ya kilimo ambayo tunasema 78 *percent* ya Watanzania wote wako huko. Sasa lazima tujiwekee malengo ambayo tunajua kabisa yanaathiri maisha ya Watanzania wote (*everyday)*, kila siku ya Mungu na lazima tukubaliane na *demands* ambazo wanatuletea.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa nafsi yangu, napenda niseme kwamba na matarajio makubwa ya Wizara ya Kilimo ni Miundombinu, katika kutuvusha katika hili. Katika hotuba ya Waziri sehemu ya pili kuna *indicators* ambazo Mheshimiwa Waziri amezizungumzia ambazo zinatupa nafasi ya kujua *how serious this situation is.*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika alisema, asilimia 70 ya wakulima wetu bado ni wakulima wa jembe la mkono ambao wanalima *between 0.2, to 2 hectors* ambazo ni ndogo sana tena sana. Anasema upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno ni *up to 40%* sasa kama *production* yetu iko hapa ilivyo, *imagine* kwamba *that is the level,* tukiwa na 40% ya *loss* tuna uharibifu wa mazingira ambao tunausemea kila siku na sasa itabidi tuutengenezee mikakati ya kuukabili *otherwise we will be in trouble.*

Mheshimiwa Spika, mpaka leo tunazungumza katika *statistics* walizoleta, ardhi inayofaa kulimwa ni hekta milioni 44, zinazolimwa ni asilimia 25, *ten million hectors*. Hekta zinazofaa kufanyiwa *irrigation*, ni hekta milioni 2.3, zinazolimwa ni asilimia 11, utumiaji wa mbolea kilo nane *per hector* au tani 121,000 *the ideal target should be 50 kilos per hector,* kulingana na *standard* zetu za *Sub Saharan Africa*. Halafu mwisho unajua lazima tufikie tani 700,000 mwaka 2010 kama walivyofanya wenzetu wa India, Pakistani, China katika *page* namba 16.

Mheshimiwa Spika, sasa tuwe *realistic about this,* kweli tutafikia hii. Kuna *investment* inayotakiwa kufanywa kwenye teknolojia *now,* kuna *investment* inayotakiwa kufanywa katika mambo ya *irrigation* ya mabwawa ili tuweze *targets* hizi na pia tuwe na *substantial gradual increment* ya *production* yetu. Kwa hiyo, tutasema mwaka huu tuko kwenye laki mbili, mwaka kesho tuko kwenye laki mbili na nusu, tuwe kwenye laki tatu na nusu ifikapo mwaka 2008. Hayo ndio maelezo ambayo mimi nilikuwa natarajia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ingeniambia.

Mheshimiwa Spika, labda niseme hili kwa sababu ili tufanikiwe lazima tuwe tayari kuumia na lazima tuwe na *political will,* tukija hapa kama Wabunge tukasikia maneno mazuri ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, *I promise you* tutakuwa hapa hapa, 2010 tunajiandaa kurudi kwenye majimbo na huenda tusirudi lakini *these should*

*be the questions* watu watauliza. Watanzania wanajifunza kuuliza maswali haya mlituambia mwaka 2005 hivi, mwaka 2010 leo tuko hivi, tutaomba msamaha wakati tunataka tuwe kama India, Pakistani, China. Leo nilikuwa tazama *TVT* asubuhi walikuwa wanaonesha programu moja ya China sijui jimbo moja la Purdon.

Mheshimiwa Spika, *25 years ago* ilikuwa ni *arid country*, wamekuja wakasema *we need this land for agriculture, we need this land for development, everybody pull up your socks*, atakayekaa nje, kwaheri. *That is why we call it a revolution,* sasa tunasema Tanzania tunataka kufanya *a green revolution* Kanda ya Ziwa, ambayo mimi namshukuru Mwenyezi Mungu nimepitapita huko Kagera nimekwenda, Mwanza nimekwenda, Musoma, Ukerewe, *the land is fertile,* wana mashamba kumi ya mfano, *total 36 hectors. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wadogo wadogo humu ndani kama Mheshimiwa Vita Kawawa na Mheshimiwa Juma Njwayo, tukikaa tunaweza kulima *36 hectors*. Sasa mashamba ya mfano ya Serikali ambayo tunataka ndio uwe mfano wa kilimo cha matunda Kanda ya Ziwa nzima kwa kutumia *Lake Victoria, 36 hectors*. Halafu tunaweka kwenye *document* hii kama *something of pride, this is a disaster, we should have 10,000 hectors* za mfano maana yake tuna mfano tunataka mtu tumwambie huu ndio tunataka uige. Sasa tunamwambia mama Mushashu akawaambie nini watu wa Kagera *36 hectors* vikundi kumi kanda nzima ya ziwa yaani tunataka mfano nini pale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema katika haya mabilioni ambayo tunaidhinisha, *we need* mifano ya mashamba ya wakulima, ili mkulima mimi nikienda kama Mbunge niseme lima vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa tahadhari ya upungufu wa chakula *page 32. I think this is a very important position*, kwa sababu anatuambia kwamba *we are going to have a problem*. Sasa badala ya kuwa ile *document* amefinywa pale, ningeomba labda wangefanyia *dissemination* ya *media* kabisa ili Watanzania na maeneo yote wajue kwamba, *we might have a problem* kwa hiyo, tuchukue njia kadhaa na mimi nafikiri kuuma na kupulizia ndio misingi ya muungwana. *This is an indication of responsible governme*nt. Naomba niwapongeze Serikali kwa tahadhari hii ambayo imezingatia ukweli na ukame na njaa uliopita na hali inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, aliyezungumzia suala la mazao haya mapya ya *vanilla,* maua mengi yaliyotajwa hapa sio mapya, pilipili, hiliki, ukienda Kariakoo utakuta watu kila siku ya Mungu wanatoka Dubai kuja kununua haya mazao sio mapya. Ni kwamba hatuna *market strategies* wala hatuna *drove strategies* za kumwambia mtu anayelima pilipili manga, Matombo au anayelima hiliki, Mvomero - Turiani alime zaidi, *so far* analima tu kwa sababu tangu babu yake wakati wa ukoloni alikuwa analima. Sasa sio mapya, ni kwamba sisi tumechelewa kuyatambua kama mazao yanayoweza kumpelekea Mtanzania mazao mbadala.

Mheshimiwa Spika, katika hili kuna sekta mbili ambazo nimeshindwa kuzitofautisha, kuna idara ya utafiti wa mazao, imeelezewa maelezo mazuri tu halafu kuna idara ya maendeleo ya mazao. Sasa nimeona kama maelezo yake yanafanana lakini nikiri tu kwamba ningependa kunukuu lakini sasa kengele ya kwanza imeshanigongea na mimi nataka niseme maneno kidogo hapa mengine. Kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba kuna maelezo mengine ambayo kama nilivyosema hayatoshelezi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naomba nilizungumze nashukuru kwamba Waziri wa Fedha, yuko hapa ni suala la upatikanaji wa mbegu bora. *Total* ya mbegu bora zilizozalishwa *10.5 thousand tones*, 1.5 mashamba ya Serikali mbegu bora, *3.5 production* ya makampuni binafsi, 5.2 mbegu bora zimeagizwa nje. Sasa tunaomba tuambiwe Serikali ya Tanzania inafanya mikakati gani ili hii 3.5 ya sekta binafsi ianyozalishwa Tanzania iwe ni kitu ambacho sasa Watanzania wanahamasishwa kuingia katika *production* za mbegu bora kuondoa *pressure* tunayoweka kwenye ku-*import* haya mambo. *If we can produce it locally,* basi *let us promote this production* zaidi, *to expand* kitu ambacho tayari tunaweza kufanya, *we are already producing three thousand tones,* tuzalishe tani elfu kumi. Lakini nadhani hili ni watu wa Wizara ya Fedha, watuambie kama wanaweza kuwasaidia watu wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwenye kuwapa *measures*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme lingine ni hili suala la programu kwenye kilimo, haki ya Mungu kwenye hiki kitabu kila *page* ina programu moja. Kwa haraka haraka kuna *District strategic investment*, kuna *PADEP*, *DADP*, kuna programu karibu 20 humu ndani hakuna popote tulipoambiwa kwamba patafanywa *coordination* ya hizi *programs* ili *programs* ziwe na *visible effect* kwa mwananchi Mtanzania wa kawaida. Hizi ni *programs* ambazo tunawapa watu wanakwenda wanakaa, *they make programs, we give them money and then how we benefit from these programs?*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba labda kwamba pamoja na uzuri lakini tupate maelezo ya kwamba Serikali, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, itaji-*commit* ili programu hizi sasa ziwe *a direct visible effect* kwa Watanzania 80 ambayo ndio walikulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Serikali kwa kutambua matatizo yaliyopo katika kutoa ruzuku ya mbolea. Tulikaa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, sisi wazalishaji wa korosho na kweli *we have a problem* lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu, niseme tu kwamba pamoja na maelekezo mazuri sana uliyotoa, bado huu mgao wa pesa zile ambazo tumepata wakulima wetu wamechangia. Mimi wakulima wa Mkuranga wamezalisha tani 10,000 za korosho, kwa hiyo, tani 80,000 zinazozalishwa, Tanzania nzima, Wilaya nne ama tano tunazalisha *fifty thousand tones*.

Sasa tuangalie basi sisi ili tukuleteeni tani laki moja na nusu mwakani, lakini kama alivyosema Mheshimiwa mmoja kwamba huwezi ukasema tu hii ni kitu kama unatoa tu alisema Mzee Jackson Makwetta kama *holly communion, we must have economic targets* ambazo zinasema hawa kwa sababu ni mabingwa wa korosho watazalisha laki moja na nusu, hawa kwa sababu ni mabingwa wa mahindi tunawapa tani laki tatu, *that is the way forward* na nina hakika hiyo ndio *zone economic analysis*

ambayo alikuwa anaizungumzia Mheshimiwa Mzee Kingunge Ngombale-Mwiru, juzi wakati wa bajeti ya miundombinu. Bila hii tukifanya tu kwa kubahatisha bahatisha *we will be in trouble*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho nasema haraka haraka ni suala la muhogo, mwezi wa nne Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, alizungumzia suala la mihogo ni kweli kuna soko Antatu milioni tano *in Europe*, sisi wakulima wa Mtwara, Lindi na Mkuranga, sisi ni wakulima wa muhogo tunaandaliwa vipi ili tuweze kuingia kwa *access*. Tunaambiwa mbegu tu zitapandwa, lakini jamani *we have to be more specific* tukitaka kilimo chetu kitutoe *from one place to another* lazima tuwe na *targets* ambazo zinajieleza zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spik,a niseme usalama wa chakula amezungumzia Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi kwa mara nyingine tena niweze kuchangia katika hotuba hii kwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitangulize kusema Mungu wetu mwema ametupa ardhi, maji na hewa ili tuweze kuvitumia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niwapongeze tu Waziri wa Kilimo na Manaibu wake wote wawili. Mheshimiwa Joseph Mungai, yeye tunamfahamu sana sisi majirani zake kama ni moja ya mifano ya wakulima waliofanikiwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, ndugu yangu ni moja kati wana ushirika wakereketwa, Naibu Waziri Mheshimiwa Christopher Chiza, tunamfahamu ni mtaalamu wa kilimo. Kazi imewapata wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umbile la bajeti hii ni nzuri sana malengo yaliyoko ndani ya bajeti hii ni mazuri sana. Wasi wasi wangu kama wengi tulivyochangia ni utekelezaji kiasi gani itatekelezwa kwa kasi mpya na ari mpya. *(Makofi)*

Mimi naomba nitoe ushauri tu kwa kuanzia kwamba pengine ni vizuri tumeamua kwamba ardhi, kilimo ndio uti wa uchumi wa nchi yetu. Tunaomba basi tuige utaratibu wa kufanya kazi wa viongozi wetu wawili Rais wetu na Waziri Mkuu, wao wana falsafa inayosema *no issue is a small issue.* Ninawaombeni sana hawa ukiona jambo limetokea mahali utasikia wamekimbia wameona, wameshuhudia wenyewe wamehakikisha wametelekeza. Tunataka tufanye *modernization* katika kilimo, lakini tukae kwenye viti haitatusaidia, lazima tuwe karibu na matatizo ya wakulima tuwasaidie na mimi nalizungumza hili kwa uchungu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi wa pili mimi niliomba nipewe mbolea ya ruzuku niongezewe. Jimbo langu la Mbeya Mjini lina kata 36, lakini kata 24 ziko *peripherals*

ndio wanaolisha mjini, wale ni *peasants* wala hawajafikia *stage* ya kuwa *farmers* ni *peasants*. Niliomba hilo kwa kujua kwamba katika mwezi Februari, hata wataalam wa kilimo wanajua, ndio kipindi ambacho mazao ya mahindi yanahitaji mbolea ya mwisho ya kuufanya mmea ubebe na uzae na upate kinachotakiwa.

Lakini majibu niliyopewa hapa ni kwamba msimu umepita, wananchi wangu wamesikitika sana katika hilo. Lakini baada ya wiki mbili, mwenzangu Mheshimiwa Vita Kawawa, akauliza swali lile na wenzangu hawa kuweza kustuka kwamba kulikoni? Kwa sababu sisi tulibaki kama ndio eneo pekee yake katika nchi lililobahatika kupata mvua, nilifikiri Serikali ingekuwa imeelekeza upande wa Nyanda za Juu Kusini, ili tuweze kulisha wenzetu ambao hawakubahatika kupata mvua. Kwa sababu si mapenzi yao ni mapenzi ya Mungu, lakini tukapewa majibu ambayo kwa kweli watu wangu wamesikitika na kusononeka sana kwa sababu wakati huo mbolea hii ya ruzuku tulikuwa hatuioni, tulikuwa hatujaipata na kipindi cha *tasoliny* ukikosa kuweka mbolea pale, huna mhindi wa kuvuna, nilisikitika sana. Lakini kama Mheshimiwa Waziri angemtuma Naibu Waziri au yeye mwenyewe akaone hali halisi, nafikiri hili lingekuwa limetatuliwa.

MheshimiwaSpika, mwenzangu Mheshimiwa Vita Kawawa, baada ya kufuatilia kwa njia nyingine alipewa tani 1,000 kutoka pale Makambako, zikaenda kuwasaidia ndugu zangu wale watani zangu. Lakini bado hii *inconsistence* katika maamuzi inatuweka pabaya, mimi nikafikiri kwamba Mheshimiwa Vita Kawawa ameogopwa kwa sababu ya neno Vita na mimi nibadilishe jina nijiite *BM 52*, labda ndio nitaeleweka. Kwa sababu kama sisi sote tunakuja hapa tunaomba vitu, tunaomba basi na Serikali iwe na *consistent* sisi wote ni wa Taifa hili tunataka tutendewe haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, ilipaswa kuona kwamba hili ambalo ameliomba Mheshimiwa Vita Kawawa ndio aliloomba Mbunge wa Mbeya Mjini, kwa hiyo, wangesema tani 1000 ziende kwa Mheshimiwa Vita Kawawa na 1000 zije kwangu. Nafikiri hapa mimi ningeweza kuwaelewa, sasa maamuzi haya ndio yanayotuletea wakati mwingine kuwe na malalamiko na mang'uniko ambayo si sahihi, na wala hayaitajiki.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo, hayo yamepita hii ndio bajeti ya kwanza ya Serikali hii, naomba nitangulize tu kwamba naunga mkono hoja iliyoko mbele yangu kwa asilimia 100, ushauri naomba muubebe, wapo watu ambao wangetoa ushauri kama wa kwangu huu wangejiita ma-*consultant* wangelipwa pesa. Mimi naomba niseme tu kwamba natoa ushauri wa bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye eneo la pili juu ya *pillars* nne za kuufanya *modernization* ya kilimo, mimi nitagusa eneo moja tu la utafiti katika *bio technology*, kama tunafanya mageuzi katika kilimo *(green revolution)* tukiacha sehemu ya utafiti haitatusaidia, utafiti tunauweka mbele, halafu mambo mengi ndio yanafuata. Huduma za ugani zinakuja baada ya utafiti, kutangulia, katika hili ninaomba kwa dhati ya moyo wangu ni wapongeze sana wafanyakazi wa kituo cha utafiti pale Uyole, wakiongozwa na Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana ya kuhakikisha Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wanapata mazao ambayo yanatakiwa, na

kwa njia ya pekee kabisa naomba nimpongeze Dr. Lyimo, yeye ndio Mtanzania wa kwanza aliyevumbua mbegu ya *hybrid 6303* ambayo mavuno yake ni tani saba kwa hekta moja na mimi mwenyewe nimejitahidi katika ekari moja nimepata magunia 32 kwa mbegu hii ambayo imetolewa na Mtanzania mwezetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wale wanafanya kazi nzuri sana pale Uyole na naomba niwaambie ndugu zangu pale pana taasisi mbili, kipo Chuo cha Kilimo Uyole na kipo Kituo cha Utafiti Uyole. Kwa hiyo, ninaomba wenzangu pengine ni vizuri tukafanya utafiti ili ukajua kwamba hali ikoje. Yale maeneo yote ya shamba ni mali ya Kituo cha Utafiti na yanatumika kikamilifu na wanafanya utafiti wa hali ya juu sana, tujaribu sana kuwaenzi watalaam wetu ambao ni wazalendo wanakereketwa na nchi hii Kituo kile cha Utafiti cha Uyole kimenisaidia sana kubadilisha maisha ya wananchi wa Mbeya kwa ujumla pamoja na maeneo yanayozunguka Chuo kile cha Uyole. Lakini wana matatizo mengi, na ninaamini kabisa matatizo haya kama yangepatiwa ufumbuzi wangefanya kazi nzuri sana katika nchi hii.

La kwanza hela ya utafiti haitoshi, si mara moja, mara mbili nazungumza katika hili, walipokuwepo wale wenzetu wa Finland wakitusaidia hela ya utafiti, ilikuwa inatolewa milioni 100 waliweza kufanya kazi nzuri sana. Lakini baada ya kulalamika mwaka 2005, yaani kipindi kilichopita, ziliongezwa pesa kutoka milioni mbili kwenda milioni sita, lakini mahitaji halisi ya utafiti watu wale kama wangepatiwa milioni 300, kazi ambayo ingefanyika ile katika programu hii basi ingekuwa ya kulikomboa Taifa hili.

Mimi naomba tujenge mawazo ya kuzilinda zaidi fedha zetu za kigeni, hatuna sababu sisi kama Taifa sasa hivi kuagiza nje ya nchi tani 30,000 kama tungekuwa tunayatumia vizuri mazingira haya na wataalam hawa, uwezo tunao wa kuzalisha. Naomba tuwepe nyenzo wale wenzetu wakamilishe utafiti wao, milioni 300 zingewasidia katika utafiti ule.

Mheshimiwa Spika, lakini lipo lingine watumishi wale wanaonekana kwamba wana manung'uniko mengi, la kwanza *promotion* zao, hawapati *promotion* kwa wakati unaotakiwa na lau kama akibahatika kupata *promotion* ile nyongeza ya mshahara mpaka leo hawajalipwa. Lakini vile vile alikuwa ni *Diploma Holder* amekwenda amechukua shahada ya kwanza, amechukua shahada ya uzamili hakuna mabadiliko katika mshahara wake. Ninaomba kwa  kasi mpya na ari mpya, ninaomba jicho lile tuliangalie vizuri wale ndio habu ya uchumi wa nchi hii katika utafiti. *(Makofi)*

Lakini lingine ambalo nafikiri linaweza likatatuliwa, ni nauli na malimbikizo wanapokwenda likizo. Huwezi uka-*compromise* na mtu ambaye ni *frustrated*, hawezi kukufanyia utafiti unaotosha mtu ambaye ni *frustrated* tena anakuwa *frustrated* kwa vitu vidogo vidogo. Ninaomba Serikali ilipe uzito hili.

Mheshimiwa Spika, ninaomba na mimi nizungumze juu ya mbolea ya ruzuku. Amezungumza sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, amelalamika na ameeleza, tumeshazungumza kama washauri kwamba mbolea, hii ruzuku kwanza naipongeza Serikali kutoa Shilingi bilioni saba mpaka sasa Shilingi bilioni 21.  Ni uamuzi makini na

uamuzi unaoonyesha kwamba Serikali hii kwa kweli imedhamiria kuwakomboa wananchi. Lakini kinachotuumiza ni maamuzi mabaya katika utekelezaji wa suala zima hili.

Mbolea hii ya ruzuku imekuwa haifiki kwa walengwa, inaishia kwa wafanyabiashara wajanja na sisi tumependekeza njia sahihi, kama mimi mkiwapatia watu wa *UWAMU SACCOS* pale Uyole mtaona mabadiliko, kwanza ni *advantage* kwa Serikali. Tutaufanya mfuko huu uwe *revolving,* wale watakusanya zile fedha na bado fedha ya Serikali haitapotea, tunaomba tuaminiane, nchi hii ni ya kwetu sote, tunapowapa ushauri, basi mkubali, kwa sababu hizi zinazotolewa zinakwenda zinapotea na hii fedha tuliyopata ya *World Bank,* yataulizwa hata makaburi yetu. Ziko wapi fedha zetu?

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza tunaomba mtusaidie tuzipitishe kule kwenye *SACCOS* ambazo ni imara. Mheshimiwa Chibulunje, wewe unazijua *SACCOS* za Mbeya Mjini zinaongoza katika nchi hii kwa ubora lakini inayowasaidia wakulima zaidi ni *UWAMU SACCOS* ya pale Uyole. Lakini tukifanya hivyo, fedha hizi Mheshimiwa Mungai zitakurudia tena kwa ajili ya mwaka unaofuata. *(Makofi)*

Pili, nilikuwa naomba hawa watu wa *TFC* Shirika la Mbolea ndio waliofanya kazi nzuri mwaka 2005, kuliko mawakala wote mliowapa pembejeo. Niseme tu, *they were so transparent,* mbolea yote iliyokuja waliipeleka, kwa hiyo, naomba hawa ndio wapewe uwakala wa kusambaza kupitia kwenye hizo *SACCOS*. Walifanya kazi nzuri sana mwaka 2005 hatuwezi kuwabeza hata kidogo. Ninawapa changamoto wenzangu wa kilimo. Ukisoma Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Rais ameahidi kufufua viwanda vilivyoko Mbeya Mjini. Unapofufua Viwanda hivyo, lazima uwe na malighafi ya kuvilisha viwanda ambavyo vinafufuliwa, kwa ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, niliwaomba ndugu zangu wa kilimo wanipe maelezo, kwa nini mmezuia kilimo cha pamba Chunya, pamba ambayo ndio ilikuwa inakilisha kiwanda cha *New Mbeya Textile*? Kiwanda hiki kilikuwa kinatoa ajira kwa zaidi ya vijana 2,500, sasa wanaoajiriwa ni 500 tu. Pamba ambayo ilikuwa ndio malighafi ya Mbeya *Industries* imekufa, mashine zimeng’olewa na mimi niliomba mnipe maelezo na Serikali iliahidi kwamba mtakuwa na mashamba ya mfano kule Chunya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JUMA SULEIMAN N’HUNGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kwanza nichuku nafasi hii kukushukuru kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo na Chakula. Lakini pia nichukue nafasi hii kwa heshima kubwa kukupongeza kwa dhati kabisa kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Spika wa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuchagua sio kwa kubahatisha, wengi tunakujua ujasiri wako, wengi tunakujua jinsi ulivyokuwa *back bencher* na jinsi ulivyokuwa Waziri na sasa hicho Kiti ulichokaa umeenea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina hakika sana siku uliyochaguliwa ulikuwa mwoga, lakini Mwenyezi Mungu anasema hakupi mzigo akakunyima kata, atakupa busara na maelewano na *inshallah* utaongoza vizuri na Mwenyezi Mungu atakusaidia.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ile. Kwa bahati nzuri, Waziri wa Kilimo mwenyewe ni mkulima, tena wa jadi wa kuzaliwa. Ninazo habari za uhakika kwamba baba yake alikuwa dereva wa trekta kule Iringa. Kwa hiyo, ni mkulima wa kuzaliwa. Ni mtu ambaye ana uchungu na kilimo. Kwa hiyo, matumaini yetu Watanzania ni kwamba, mabadiliko na mapinduzi ya kilimo katika kipindi hiki yatachukuliwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo nitalizungumzia, tuna Sera ya Chama cha Mapinduzi inayohusu kilimo. Lakini Sera ya Chama cha Mapinduzi inayohusu kilimo haikuanza leo. Nadhani Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba pale Iringa ndipo lilipoanzia Azimio la Kilimo, "Siasa ni Kilimo," miaka hiyo iliyopita. Kama utalichukua Azimio hilo la Siasa ni Kilimo la wakati huo ukalichambua vizuri na kama utalitekeleza lilivyo, basi unaweza ukaona mengi ambayo tunazungumza sasa hivi yamo mle kwa mfano kilimo cha kisasa, mbegu nzuri, utafiti, matrekta, kuondoka katika jembe la mkono kuja katika vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Waziri na hotuba yake ni nzuri kweli na mimi namjua Mheshimiwa Mungai ukimpeleka Mahakamani atakushinda tu, ana uwezo mzuri sana wa kujieleza. Mheshimiwa Mungai alipokuwa *backbencher* alikuwa *backbencher* mzuri sana. Akikaa kwenye Wizara ni mzuri sana, lakini bahati nzuri Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Mungai nyie nyote mlikaa Bungeni wakati mmoja, mkiwa *backbenchers* na mmeshika nafasi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, umerudi kama Spika, Mheshimiwa Mungai amebahatika kurudia tena Wizara ya Kilimo ambayo miaka ya nyuma aliwahi kuishika akaporonyoka kwa mambo mengine. Sasa tunategemea safari hii itasimamiwa vizuri zaidi kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachokusudia kukizungumza katika suala la kilimo, Watanzania wote tunaelewa kwamba kilimo ndio uti wa mgongo wa Taifa letu. Maelezo katika hotuba ni mazuri, viwango vya fedha vilivyopangwa ni vizuri, lakini je, nilitaka nielewe, hivi tafsiri ya siasa ni kilimo, lile Azimio la Iringa limekufa au lipo? Utekelezaji wake ukoje?

Nimeona mambo mengi na fedha nyingi zimetengwa kwa mabilioni, usimamizi wake ukoje? Ama mwaka huu utamalizika na mwaka mwingine atakuja Mheshimiwa Mungai ataleta maneno mazuri, safi.

Mheshimiwa Spika, leo hii tumeambiwa hapa maneno mengi sana na siku za nyuma ilifikia kiwango tukaelezwa hapa na wakubwa kwamba *DC* yeyote atakayetamka

kwamba kwake kuna njaa, basi kajifukuza kazi. Matokeo yake ma-*DC* na ma-*RC* wote wakasema katika maeneo yao hakuna njaa, matokeo yake njaa leo imetukumba miaka mitatu mfululizo kwa sababu ukweli walikuwa wanauficha. Sasa hatutaki tufike huko.

Mheshimiwa Spika, tunachotaka sasa hivi, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pamoja na mkakati huu, lakini usimamizi wa Bajeti hii na fedha hizi uwe wa uwazi zaidi na uwe wa ukweli zaidi na tufaidike sote Watazania. Usiwe usimamizi wa kuficha majipu, maana ukificha jipu lazima utaadhirika. Usimamizi wa *undugunazation*, usimamizi wa urafiki, usimamizi wa kuoneana haya, hatuwezi tukaenda!

Mheshimiwa Spika, nayazungumza haya kwa sababu naona aibu sana Tanzania kama Tanzania Waziri kama Mungai anasimama na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Meghji na Waziri Mkuu, anaomba chakula katika nchi yenye hekta milioni 40. Ni aibu sana! Sijui hili tutakwenda nalo wapi na mpaka lini! Nchi zinazotupa msaada, sisi tuna eneo kubwa zaidi la ardhi kuliko wenyewe, ni kwa sababu masharti ya kilimo bado hatujayafuata. Wataalam wa kilimo waliobobea hawaendi Vijijini, wako Mijini zaidi kuliko Vijijini. Wamefunga tai vizuri, makoti mazuri, kila kitu, Ofisi zenye viyoyozi, hawaendi kulima. Mheshimiwa Mungai atusaidie sasa watalaam hawa waende Vijijini, waende wakakae na wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka Mwalimu Nyerere aliwahi kusema kwamba kiongozi bora katika Kijiji ni yule ambaye ana shamba la mfano. Sasa tukiulizana hapa, Wabunge wenye shamba la mfano wangapi na nani anayakagua mashamba hayo, hao wataalam wanakwenda kiasi gani? Mwenzangu hapa amesema kwamba kuna mbegu ya maharagwe unapata mavuno mazuri kiasi gani, imesambazwa mbegu hiyo? Sasa tunataka tuone kwamba suala la njaa katika nchi hii kwa wakati huu Mheshimiwa Waziri Mungai na timu yake linakomeshwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika nchi hii mpaka leo bado kuna utapiamlo. Mbegu nzuri kama za kina Msindai ni chache tu, lakini wengine tuliobaki sisi ndio hivyo. Eeh, ni hali, maziwa hamna, ufugaji sio mzuri, chakula kidogo tatizo moja kwa moja, milo ya kawaida haipo. Ndio maana nadhani Mheshimiwa Rais ameamua kuanzisha Wizara ya Kilimo na Chakula. Mheshimiwa Mungai pamoja na kujibu kwa Rais, lakini na kwa Mwenyezi Mungu utakwenda kuulizwa kwa nini watu wanaendelea kuombaomba hawana chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la mashindano ya siasa ni kilimo ni vyema yale mashindano ya siasa ni kilimo yakaangaliwa na yakaboreshwa, badala pengine kushindana kwa Mikoa, Wilaya, sasa yaende mpaka katika Vijiji yawaguse wakulima mmoja mmoja na yale mashindano yawekwe kila Mkoa, Wilaya na kila Kijiji ili kuwe na motisha ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa na maelezo mengi, nimeona kwamba Serikali imeweka mkazo mkubwa katika suala zima la ruzuku ya mbolea. Sio sahihi kwamba Tanzania nzima watu wanalima kwa kutegemea mbolea. Kuna maeneo hayahitaji mbolea, lakini yanahitaji ruzuku ya kilimo, yanahitaji mbegu bora. Nchi zote

duniani kubwa kubwa kama Marekani, Uingereza, Japan zinatoa ruzuku kubwa kwa wakulima wao, lakini leo Tanzania kwa mfano bei ya dizeli ambayo ndio mafuta, yanatumika katika matrekta, malori ya kusombea mazao kwa wakulima, lakini imepanda karibu sawa na petroli.  Mkulima wa kawaida bado anabanwa, motisha iko wapi? Naomba kuwepo na ruzuku maalum kwa sababu ya mbegu na hawa wakulima.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nitalizungumza katika nchi zote zilizoendelea katika kilimo zina benki maalum ya wakulima. Tanzania leo toka Uhuru mpaka sasa tuna miaka zaidi ya 40 hatuna benki ya wakulima tunababaishana. Kuna benki ya wafanyabiashara, kuna benki sijui ya nani lakini hakuna benki ya wakulima. Nadhani sasa hivi wakati umefika Serikali kuanzisha kwa haraka zaidi benki ya wakulima. Benki ya wakulima lazima inakwenda sambamba na bima ya wakulima. Watu wa benki wanaogopa kuwakopesha wakulima kwa sababu wakulima hawana *insurance* lakini lazima kunakuwa na *insurance* maalum kazi yake kusimamia wakulima. Kwa hiyo, hili ni jambo la kufanyiwa kazi na Serikali. Ni vema Serikali ianzishe Benki ya wakulima na kuwepo na *insurance* ya kudhamini wakulima ili kilimo chenyewe kiende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini unaweza ukashangaa kuona kwamba katika nchi yetu bado kuna benki ya wafanyabiashara, *CRDB* na mambo mengine tunahimiza kilimo, tunaondoka, hatuelewani, wakulima wanazalisha lakini wanakula hasara, hakuna anayewafidia, naomba sana jambo hili lisimamiwe. Tena suala la benki ya wakulima naomba lizingatiwe kwa haraka iwezekenavyo ndio jambo linaloweza kuwakomboa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la ardhi. Tanzania kuna ardhi nzuri na kubwa. Sasa hivi tumeingia kwa wingi tu kwa mfano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, *COMESA* na mambo mengine mengi. Wenzetu wengi waliokuwepo huko katika nchi zao hawana ardhi. Watakachokimbilia kikubwa Tanzania ni kutafuta ardhi na wakija hapa ardhi ya Watanzania wataichukua kwa bei rahisi tu wengine watawadanganya danganya Watanzania watapata ardhi na watakuwa ma-*settler* katika nchi yetu.

Naiomba Serikali iangalie kwa mtu yeyote ambaye si Mtanzania asiwe na kibali cha kumiliki ardhi Tanzania kwa vyovyote vile. Ardhi ya Watanzania imilikiwe na Watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naiomba Serikali ardhi iliyokuwepo ikafanyiwe utafiti wa kutosha. Itengwe ardhi kwa madhumuni ya kilimo tu iwe inalimwa, itengwe ardhi sehemu ya wafugaji na itengwe ardhi ya akiba. Wezee wetu waliokuwa wanalima wakati huo walikuwa na mashamba makubwa, lakini shamba moja analima miaka miwili akiona limepungua kidogo mbolea, analilaza hilo shamba analima miaka miwili mingine. Kwa hiyo,  Watanzania tukiweka ardhi ya akiba baada ya miaka 50 au 100 itakuja iwafae watoto katika suala la kilimo. Kwa hiyo, suala la njaa katika Taifa letu litakuwa halipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa heshima na taadhima sipendi kupoteza muda au kupigiwa kengele ya pili naomba nitamke kwamba naunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi hii ili nami nichangie Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, ambayo tunaiita uti wa mgongo hapa nchini lakini kwa kweli sio uti wa mgongo sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na watumishi wa Wizara ya Kilimo walioko kwenye Kata. Hawa watu wana taabu sana, wengi bado hawajapanda vyeo toka mwaka 1991. Wakati Wizara ya Kilimo iko na Mifugo watumishi wote wa Mifugo na Kilimo walikuwa na shida ya namna hii lakini zilipogawanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati ule akawa Waziri wa Mifugo na Maji, aliwasaidia wenzetu wa mifugo wote wakapanda vyeo sasa hawa wenzetu wa kilimo mpaka leo bado. Kwa kweli ni aibu kwa Serikali na hii ndio inayosababisha hawa watu wasifanye kazi ipasavyo. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa makusudi kabisa afanye kama Waziri wa Mifugo alivyofanya wakati ule wote wakapanda vyeo. Sasa hivi hatutafika kama tutaendelea na watu ambao kila siku wana manung'uniko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili hawa hawa watumishi walioko kwenye Kata, Kata zetu ni kubwa mno tumeomba zigawanywe. Hawa watu hawana usafiri. Kwa hiyo, waangaliwe wapewe usafiri, walipwe posho zao na wapewe nyezo za kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni juu ya mbegu. Sasa hivi tuna matatizo ya mbegu. Halmashauri zetu hazishughuliki kutafuta mbegu kwa wakati unaotakiwa. Kisingizio kwamba hawana fedha. Sasa hizi fedha nyingi zilizokwenda Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, zisaidie kununua mbegu na kusogeza karibu na wakulima kabla ya msimu wa mvua. Hiyo itatusaidia sana kufanya wakulima wetu waweze kulima kwa kutumia mbegu zinazotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nizungumzie juu ya Mikoa kame. Mwaka 2000 tuliambiwa Mikoa kame ambayo ni Dodoma, Singida, Shinyanga, Tabora itasaidiwa lakini mpaka sasa bado haijapata msaada. Tuliambiwa tumetafutiwa fedha kwa ajili ya mradi wa kusaidia wakulima wetu juu ya kupata mbegu, matrekta, bei nzuri na kutengeneza barabara za vijijini lakini mpaka leo bado. Mimi naomba Waziri akifunga hoja yake atueleze ana mpango gani na Mikoa hii kame ya Dodoma, Singida, Shinyanga na Tabora ili tujue tunaelekea wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo juu ya umwagiliaji. Tanzania tuna makorongo mengi sana ambayo yanajaa maji wakati wa mvua. Tukiweza kuyazuia hayo kwa kweli hatutakuwa na shida ya chakula. Nayo tuliambiwa mkakati maalum unafanywa ili makorongo yetu yazuiwe wananachi wetu waweze kulima lakini hakuna kinachofanyika. Hata hao watu wa umwagiliaji kule mimi sijui wanafanya kazi gani.

Mimi nitakupa mfano Meshimiwa Waziri wa skimu zangu mbili za umwagiliaji. Moja iko Mwangeza na nyingine Msingi tena hizo fedha nilitafuta mimi mwenyewe kwa wafadhili, shilingi milioni 125 kila bwawa lakini mabwawa yale yamejengwa hata maji hakuna mle ndani, miundombinu imeshabomoka. Naomba Mheshimiwa Waziri na wataalam wako mfuatilie mjue kuna nini. Wananchi wetu wanalalamika sana sasa hivi mpunga waliokuwa wamelima umekauka kwa sababu mabanio yamebomoka. Kwa hiyo, naomba sana mfuatilie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee juu ya kupeleka fedha katika Halmashauri. Tunajua Serikali imepeleka fedha nyingi kwenye Halmashauri zetu lakini Halmashauri nyingi usimamizi bado mbovu. Kwa hiyo, ni juu ya Serikali kuhakikisha kwamba hizo fedha zinafika kwa walengwa. Kuna fedha ambazo wananchi wanataka wakopeshwe, kwa nini hizi fedha msipeleke kwenye Kata? Tuna *SACCOS* kila Kata sasa hivi.

Kwanza pale uangalizi utakuwa mzuri sana. Sasa hivi wananchi wetu wanakopeshana kule kutoka kwenye *SACCOS* zao na fedha wakikopa wanarudisha vizuri sana. *(Makofi)*

Mimi naomba hizi fedha za kuwakopesha wakulima zisiishie Wilayani wala Wizarani, ziende kwenye Kata, kwenye *SACCOS* zetu ili wananchi waweze kuzipata kwa urahisi na kuzitumia kwa wakati unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia bado naona kuna umuhimu wa bei za mazao ya kilimo kurudi Wizara ya Kilimo. Hawa ndio wanajua haya mambo, kuhamisha usimamizi wa bei kupeleka Wizara nyingine ni kosa kubwa. Kule lilikokwenda watu hawashughuliki na kilimo.

Naomba hizo shughuli za bei za mazao zirudishwe Wizara ya Kilimo. Tena hii irudi sasa, isingoje wakati mwingine. Sasa hivi wakulima wetu wanavuna mazao, ilitakiwa Wizara ya Kilimo iwe imeshaangalia bei, wapi bei nzuri ili wakulima waweze kuuza.

Kwa hiyo, hebu tusiwayumbishe wakulima wetu kutoka Wizara moja hadi nyingine, wao wanajua Wizara ya Kilimo na ni jukumu lenu msikwepe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matrekta tumeimba kila mwaka, matrekta yanunuliwe, yapelekwe kwenye Kata, huko usimamizi ni mzuri kabisa. Kuna watu tuna matrekta kule kwenye Kata yanakwenda yanajiendesha na yanajilipa. Kwa hiyo, Serikali msituletee huo mpango eti mnaweka mahali yawe yanatoka yanakwenda kwenye Kata, pelekeni kwenye Kata, Kata ziwajibike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia kusema tuige mfano wa wenzetu wa Uganda, pesa zinakwenda kwenye Kata, vifaa vinakwenda kwenye Kata, sasa hivi mambo mazuri kwa nini tusiige, hatujafanya majaribio sisi tunang'aka tu kule hakuna wasimamizi, wapelekeeni si mnao wasomi waende kwenye Kata, *TASAF* ipo mpaka vijijini, kwenye vitongoji na kazi zinakwenda, itakuwa nyie watu wa kilimo?

Mimi nashauri kabisa haya mambo yafanyike kule kwenye Kata tuachane na haya ya kukaa makao makuu tunaangaliana na matrekta mkinunua yanakaa makao makuu au Mkoa au Wilayani yaande kwa walengwa. Sasa hivi ukienda vijijini kwetu kuna watu wameshaanzisha shirika zao, wamenunua matrekta na yako kule yanafanya kazi. Kwa hiyo, tunaomba na Serikali tuondokane na aibu ya kila mwaka kuwa na njaa, wapelekeeni wakulima vyombo vya kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila siku tunasikia Bodi ya Kahawa, Bodi ya Pamba, Bodi ya Tumbaku hivi Bodi ya Alizeti itakuja kuanzishwa lini? Afadhali basi haya mazao mchanganyiko alizeti, karanga, ufuta, soya nayo yaundiwe bodi au hayo mnayadharau kwamba sio mazao?

Mimi ninawashauri na kwa kweli sio kuwashauri ni kuwataka na sisi tuwe na bodi kwa mazao tunayolima hayo ndiyo yanafanya sisi tunanyanyaswa na wanunuzi. Sasa hivi nasikia vikao vinakaa kila siku kufuta kodi ya mafuta ghafi kutoka nje. Sasa na sisi tumejiandaa kupambana na nyie mlituambia kodi ipo na kodi iendelee iwepo ili wananchi wetu wauze mazao wanayolima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine mwaka huu nina imani maeneo mengi watapata mazao ya kuridhisha lakini maeneo hayana ma-*godown* ya kuhifadhia mazao haya. Hamuwezi kusema kila kitu wananchi wawe wanajitolea ma-*godown* ni kazi ya Serikali. Jengeni ma-*godown* ili tuweke akiba ya chakula. Sasa hivi kama hatuna mahali pa kuweka chakula wananchi hawatakubali mazao yao yanyeshewe, watauza halafu tuje kuhangaika tena.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri utaratibu wa ma-*godown* uende kama tulivyofanya *MMEM* na *MMES* tuwe na *operation* maalum kwa ajili ya kujenga vitu hivi tutaondokana na tatizo la uhaba wa chakula. Nimesikia kuna mpango wa kununua sijui tani milioni moja lakini hizo bado ni chache kama tuna ma-*godown* mengi wananchi wenyewe wataweka akiba yao. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri nakuomba sana ujitahidi.

Mheshimiwa Spika, halafu barabara za vijijini, kuna barabara zinalimwa kwa ajili ya kusafirisha mazao, siku hizi zimekufa lakini tukisoma kwenye hotuba tunaambiwa pesa zimetengwa kwa ajili ya miradi ya kilimo ikiwa ni pamoja na kutengeneza barabara, kuwasaidia wakulima hizi huwa hatuzioni. Tunaomba safari hii unapojumuisha uzungumzie hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nilikuwa na hayo tu ya kuzungumza leo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hautoshi kumpa nafasi mchangia hoja yeyote kwa muda ule tuliokubaliana. Utaratibu wa jioni ni kama ifuatavyo, itawezekana Waheshimiwa Wabunge wanne tu kuchangia nao kwa mpangilio ni Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi na Mheshimiwa Felister Bura. Hiyo itatufikisha saa 12.00 jioni na

itabidi wakati huo niite Naibu Mawaziri mmoja baada ya mwingine kwa hiyo saa 12.00 jioni hadi saa 12.15 jioni mmoja, saa 12:15 jioni mpaka 12.30 jioni mmoja, halafu ataingia mtoa hoja Mheshimiwa Waziri kuanzia saa 12.30 jioni mpaka 1.00 usiku.

Waheshimiwa Wabunge, saa 1.00 usiku Bunge litaingia katika Kamati ya Matumizi ili kupitisha au vinginevyo Makadirio ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, huo ndio utakuwa utaratibu. *(Makofi)*

Kabla sijasitisha shughuli za Bunge kwa asubuhi hii kulikuwa na hoja ya kuhusu utaratibu ambayo nataka niitolee maamuzi.

Kwanza napenda kuwapongeza sana vijana wetu wa *Hansard* wameniletea yote yaliyosemwa na Mheshimiwa John Shibuda na Mheshimiwa John Cheyo, haya hapa, dakika hizi hizi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa John Shibuda alichosema ni kwamba, ninanukuu: “Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuja kuibua na kuzindua ari ya kujengwa mfumo wa elimu. Mkoa wa Shinyanga elimu ni duni. Mfuko wa Elimu wa Wakulima katika Mkoa wa Shinyanga umejenga sekondari 87. Akaendelea akasema na juzi juzi zimejengwa sekondari 42 ambazo zimechangiwa na Mfuko wa Elimu wa Wakulima.

Baadaye akasema Mheshimiwa Spika, zao la pamba ni uti wa mgongo wa uchumi. Nasikitika sana pamoja na nia nzuri ya Serikali kuinua bei ya zao la pamba, nia nzuri sana imeondosha makato yaliyokuwa yanapelekwa kwenye bodi, yamebaki katika mfuko wa maendeleo ya zao la pamba. Naiomba Serikali ipitie upya uamuzi wake.”

Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyokuwa mmenisikia, hakuna wakati wowote Mheshimiwa John Shibuda, alitamka kwamba Shinyanga tumejenga sekondari juzi kwa kutumia Mfuko wa Pamba. Haya ni maneno amebambikiziwa na Mhesheshimiwa John Cheyo, hayamo katika *Hansard. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ila yeye sasa akaendelea sasa na kusema hela iliyopo ndani ya mfuko wa pamba au ninukuu yote: “Mheshimiwa Spika, kifungu cha 50 ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni. Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza kuzungumza ameliambia Bunge hili kwamba Shinyanga tumejenga juzi *secondary schools* kwa kutumia mfuko wa pamba ambalo halikusemwa. Huu ni uongo kabisa na ingefaa atoe uthibitisho huo. Tumewachangisha wananchi wa Bariadi na sehemu nyingine na sio kutumia Mfuko wa Pamba ingawa mapato ya pamba kutoka zao la pamba yalikuwa yanaingia katika Mfuko wa Bodi ya Elimu ya Shinyanga. Hela iliyopo ndani ya mfuko wa Pamba inaliwa na watu wasiojulikana na hili linajulikana ndani ya Serikali na kadhalika.”

Kwa hiyo, sasa kwa kuwa Mheshimiwa John Shibuda imethibitika hakusema uongo wowote ila kuna tuhuma zilizotolewa katika kujaribu kujenga hoja ya utaratibu na

Mheshimiwa John Cheyo yeye ndio akasema kwamba Mfuko wa Pamba fedha zinaliwa na watu wasiojulikana.

Nimeamua sasa hakuna wajibu wowote kwa Mheshimiwa John Shibuda kutoa uthibitisho wowote kwa sababu hauhitajiki kwa sababu hakusema ila amesingiziwa na badala yake ni kwamba Mheshimiwa John Cheyo ambaye yeye sasa ndio ametoa tuhuma kwamba hata Serikali inajua, Waheshimiwa Wabunge hili ni *serious* kwa sababu anachosema hapa Serikali inawajua hao watu wanaokula fedha za wakulima wa pamba na hakuna chochote kinachofanyika.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maana hiyo sasa yeye atatakiwa atoe uthibitisho huo na nimeamua kwamba aulete Bungeni uthibitisho huo siku ya Jumanne tarehe 11 Julai, 2006 kumpa nafasi ya kutosha. *(Makofi)*

Baada ya kusema hivyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Kwa upande wa Serikali, basi labda Mheshimiwa Waziri wa Kilimo mwenyewe ndiye kiongozi wa shughuli kwa sasa.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema wakati tunasitisha shughuli zetu hapa asubuhi, tunao wasemaji wanne tutaanza na Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka wa Morogoro Mjini lakini Mheshimiwa Dr. Festus Limbu yeye ni wa Magu Mjini, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi na Mheshimiwa Felister Bura atafunga orodha ya wachangia hoja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Dr. Festus Limbu. *(Makofi)*

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nyingine ili na mimi niweze kulihutubia Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kupongeza Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, nikianzia na Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa bajeti nzuri ambayo naamini imeandaliwa vizuri na imekidhi matarajio kwenye karatasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo hotuba ya Waziri inaeleza kwenye ukurasa wa tisa hali ya kilimo chetu ni duni sana, kama ni mgonjwa ukilinganisha na nchi nyingine zilizondelea ukilinganisha na nchi kama Afrika Kusini, India, Amerika kilimo chetu ni kama mgonjwa yupo kwenye dripu lakini ukilinganisha na nchi nyingine kama Uholanzi basi kilimo chetu kipo *ICU*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kazi tunayo kubwa ya kufanya lakini naamini kwamba wana matumaini makubwa sana kama walivyo Watanzania wote kwamba viongozi waliopewa dhamana ya kuendesha ama kuongoza Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika wataleta *value for money* (thamani ya fedha) inayokwenda kwenye sekta hii itaonekana kwa maana ya kwamba tutapata matokeo mazuri kwa fedha ambazo zinaingia kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri ameomba shilingi bilioni 123 katika kutekeleza miradi mbalimbali na shughuli mbalimbali ndani ya Wizara lakini naamini kwamba chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri Joseph Mungai ambaye namfahamu ni mchapakazi, Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Naibu Waziri na yeye namfahamu vizuri ni chapakazi na Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Christopher Kajoro Chiza, namfahamu ni mchapakazi mzuri na Katibu Mkuu Ndugu Peniel Lyimo, namfahamu kama ni mchapakazi kwa hiyo, nina imani kwamba *value for money* ambayo Waziri anaomba au thamani ya fedha ambayo wanaomba shilingi bilioni 123 itaonekana na hatimaye Watanzania waone kilimo chetu kinaanza kuinuka na kutoka *ICU* pole pole.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza na maombi ambayo nimeletewa na wapiga kura wangu ambao ni wafanyakazi wa Idara ya Kilimo Halmashauri ya Wilaya ya Magu ambao toka wamehamishiwa Halmashauri kutoka Wizara ya Kilimo miaka ya 1970 mpaka leo *promotions* zao hazitekelezwi, hawajapata *promotions*, hawajarekebishiwa mishahara na mimi mwenyewe baada ya kuniletea malalamiko hayo kama Mbunge wao nilimwandikia barua Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo nikamweleza kero hii na akaahidi kwamba ataishughulikia, akanijibu kwa barua. Lakini bado mpaka leo hii wanasema mambo yamekwama Wizara ya Utumishi, sasa naomba hali hii ishughulikiwe haraka kama ambavyo wasemaji wenzangu wameshasema Mheshimiwa Mgana Msindai, amesema hilo kwa uchungu na mimi naomba na nazidi kurudia kwamba Wizara ichambue takwimu zake ili watumishi wa Idara hii nyeti waweze kutendewa haki na hatimaye waweze kufanya kazi kwa *morale* inayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye umwagiliaji ukurasa wa 33 Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima, alinisaidia kwa kushangaa kwamba ukanda wa Ziwa Victoria ukurasa wa 33 kuna vikundi 10 ambavyo vimefanyiwa majaribio kwenye mashamba ya hekta 36.

Mheshimiwa Spika, najua kuna bajeti kubwa sana kwenye umwagiliaji naamini inakwenda kwenye maeneo mengine ambako pengine labda kuna *potential* kubwa lakini bado naamini kwamba eneo la Ziwa Victoria lina *potential* kubwa sana la kulisha maeneo hayo kwa sababu ukisema kwamba fedha za umwagiliaji ziende Ifakara peke yake, Madibila peke yake ukaacha maeneo mengine bado utagharamika kusomba chakula kukitoa Madibila kukipelekwa Mwanza lakini kama Mwanza, Magu, Sengerema, Misungwi kuna maeneo ambayo yanaweza yakaimarishwa yakapata fedha za umwagiliaji utakuwa umepunguza tatizo Kitaifa siyo kuwapa sehemu kubwa ya bajeti watu wa eneo moja. Kwa hiyo, mimi nadhani kwamba juhudi haijafanyika kiasi cha kutosha katika kuimarisha na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika ukanda wa Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, kuna mabonde mazuri tu nikitolea mfano kwenye Wilaya yangu ya Magu, kuna eneo la Chabula, Kata ya Kongolo, Kata ya Magu Mjini kuna Sawenge, kuna mradi wa Ilungu, Shinembo na kuna mradi wa Kalemela na bado ukienda Sengerema kuna Katunguru na Misungwi kuna Bugharika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi hii iko tayari kwa ajili ya kuzalisha ni kiasi cha kuweka hela kidogo na hatimaye wananchi waliopo pale na vijana ambao hawana ajira wataweza kujipatia ajira na hatimaye kujiondolea umaskini. Mradi wa Shinembo pale Kahangara umefadhiliwa na *UNDP* lakini mkandarasi aliyekuwa amepewa hajaonekana na baadhi ya vifaa vimeanza kuibiwa pale. Naomba sana Wizara tukitoka hapa tufuatilie kujua kwamba kulikoni? Siyo fedha zimetolewa kama ni za Serikali ama ni za wafadhili lakini mbona mambo hayaendi? Wananchi wanasubiri, vijana wanasubiri wana njaa hawana fedha lakini miradi haiendelei na kuna watu wachache wamefanya makosa.

Mheshimiwa Spika, mimi nazungumza haya kwa uchungu kidogo na kuna eneo ambalo nimeshawahi kwenda mimi pamoja na Mheshimiwa *Engineer* Christopher Kajoro Chiza, kwenye eneo la Kayanza ambako mimi nina shamba pale, ndiyo. Nina shamba la ekari 20 pale nilikwenda na Mheshimiwa Naibu Waziri nikamwonyesha, nikamwambia angalia hapa ni kama *Eden,* watu wanavuna mwaka mzima lakini hakuna msaada wowote wa Serikali wa kuwasaidia, nitaomba sasa nimpeleke na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika mwenyewe Mheshimiwa Joseph Mungai, ili akaone jinsi gani eneo hilo na maeneo mengine katika Ziwa Victoria ambayo kwa kweli huhitaji kuagiza chakula kutoka Mbarali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo hilo la Kayanza limesaidia sana watu katika kipindi hiki cha njaa kwa sababu kuna ndizi muda wote, kuna mahindi muda wote, kuna maharage muda wote na hivi sasa ninavyoongea watu wanakula mahindi mabichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba hilo tuliangalie na tusaidie katika kuhamasisha, naomba Wizara watoke kule juu warudi chini kwa wananchi huku waangalie kinachoendelea, Mheshimiwa Waziri naomba tukitoka hapa mvae mabuti, muondoe tai, mvae pama mwende mashambani. Wananchi wanawasubiri kule mkawahimize na watu wale wa ugani waende vijijini, ndiyo! Vijana wengi ambao mimi nawafahamu wamepata ajira kwenye eneo hili wanakwenda kule lakini kwa sababu wanakosa *support* wakati mwingine wanakata tamaa kwa msaada ambao ungeletwa na Serikali kidogo wangeweza kuendelea kwa haraka zaidi na kuendeleza kilimo na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, hili la umwagiliaji katika maeneo haya naomba nisisitie lakini pia nitumie fursa hii kumpongeza mkulima mmoja katika Jimbo langu anayeitwa Cosmas Chenyenge, yeye analima katika kijiji cha Lubugu, amelima ekari zaidi ya 100 za mpunga na amemwagilia, amechimba lambo lake mwenyewe na anavuna kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, Wizara yako imtembelee ione jinsi anavyofanya kazi na huyu anaweza kuwa mfano kwa wakulima wengine wa eneo

hili badala ya zile ekari 36 ambazo mnasema ziko pale kwenye Bonde la Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana mkulima huyu Ndugu Cosmas Chenyenge, naomba Mungu aendelee kumbariki na aweze kuwa mfano na ninaamini watu wa kata ile na wa Wilaya ya Magu hawezi kufa njaa kwa sababu mpunga atakaoivisha utatusaidia, nampongeza sana mkulima huyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye barabara vijijini. Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilayani *(DADPS)* tumesema kwamba ndiyo zinaanza na wananchi washirikishwe lakini nina mashaka kwamba kama mpango huu utakwenda kwa kasi inayotakiwa tayari na mpango wa *TASAF* ambayo wananchi wanashirikishwa, kuna mpango wa *MMEM* ambao wananchi wanashirikishwa pia, kuna mpango wa *MMES* pia wananchi wanashirikishwa na huu tena unakuja.

Mheshimiwa Spika, sasa bila kuwasaidia wakulima, bila kuongeza kasi katika kuwasaidia wakulima mipango hii inaweza ikachukua muda mrefu na inaweza ikachukua miaka miwili au mitatu hatimaye iweze kuanza. Kwa hiyo, mimi naomba kwamba Wizara ijipange vizuri katika kuhakikisha kwamba mipango hii ya Maendeleo ya Wilaya inaanza haraka na bila kuwa na matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna barabara nyingi vijijini ambapo nina mashaka kama mipango hii itaweza pia kutatua matatizo ya usafiri vijijini ili wakulima waweze kusafirisha mazao yao. Kwa mfano katika Jimbo langu barabara ya kwenda Bugatu, Salama, Nombola, Nyasato, Mwamanga, Nyamahanga, Buhumbi, Salong'we, Igekemaja hakuna barabara kule, watalima lakini watasafirishaje? Je, *component* ya *DADPS* itatengeneza barabara hizo ambazo haziko kwenye bajeti ya Wizara, hayako kwenye bajeti ya Wizara, *TANROADS*, hayako kwenye bajeti ya Wilaya? Hizo barabara je, zitaingia kwenye mpango wa Wilaya? Naomba pia hilo nielezwe kama hilo litakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei ya pamba. Bei ya pamba inaendana kwa namna moja ama nyingine na Bodi ya Pamba pamoja na Chama cha Ushirika cha Nyanza *(NCU)*. Niungane na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mheshimiwa Dr. James Alex Msekela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila ushirika madhubuti masoko ya mazao ya wakulima yatayumba, bila ushirika imara masoko ya wakulima yatayumba, naomba chonde chonde Serikali ifanye juhudi ya kufufua ushirika, juhudi zilizopo nyingine zinaelekea kama ni za kuvunja ushirika lakini juhudi zifanyike za kufufua Nyanza ifufuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbolea, Serikali imetenga shilingi bilioni 21 kutoka shilingi bilioni saba, wakulima wa pamba watapata mbolea hii kwa namna gani? Wakulima wa pamba kwa kawaida mbolea hawatumii sana lakini kikubwa wanachotumia ni dawa za kuua wadudu kwa nini Serikali isitenge katika hizi bilioni 14 zilizoongezeka hizo shilingi bilioni saba zilizokuwepo waendelee kupata lakini katika hizi shilingi bilioni 14 zilizoongezeka wakulima wa pamba wapate angalau shilingi bilioni nne au tatu basi

lakini ziende kwenye madawa, ziende kwenye dawa za kuua wadudu. Zinapokwenda kwenye maeneo yanayolima mazao mengine kama mahindi wanaweka mbolea ili mazao yapatikane lakini kwenye pamba unanyunyizia wadudu ili pamba ipatikane.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali iangalie uwezekano wa kutenga sehemu kwa utaratibu wowote itakaouona ili basi kiasi cha sehemu hiki iweze kwenda kufidia gharama za dawa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la *improved varieties,* vituo vyetu vya utafiti nchini vimetoa mbegu bora na zimeshakuwa *certified* lakini bado ziko kwenye *shelves*, Wizara ifanye juhudi ya kufukisha mbegu hizi kwa wakulima kwa bei ndogo. Ukienda Seriani, Lyamungo, Ilonga kuna mbegu ambazo ziko kwenye *shelves* hazijawafikia wakulima bajeti hii iwafikishie wakulima hizo mbegu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utegemezi wa fedha za nje katika kuendeleza Kilimo. Bajeti yetu ni tegemezi kwa 81.8% bajeti yetu ya maendeleo ya kilimo 81.8% bado tunafanya makosa yaleyale tuliyoyafanya kwenye Miundombinu na ndiyo maana tuliamua kusema kwamba 1.8 bilioni kila mwezi ziende kwenye barabara kwa nini tusiseme hili pia tupeleke fedha nyingi zetu? Tukiendelea kutegemea wafadhili sijui kama tutaendeleza kilimo kwa kuwategemea wafadhili wa nje.

Mheshimiwa Spika, mwisho kilimo chetu ni cha *small holders* 80% ni wakulima wadogo wadogo hivi mchango wa *commercial farming* kwenye nchi yetu ni asilimia ngapi? Kwa nini tusianze na taratibu za makusudi? Kuna *graduates* wengi sana waliomaliza *Ph.D, Masters* kwa nini tusiwawezeshe kwa makusudi tuwapeleke maeneo ambayo hayana watu, wakopeshwe zana, utaalam wanao wapelekwe *exposure* kule ambako watu wamefanikiwa waweze kuanzisha kilimo katika mashamba hayo. Tunamwagilia 11% hatuna *potential area* na *high potential area 11%* ndiyo tunamwagilia, kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR M. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, lakini kabla sijachangia naomba nichukue nafasi hii nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ndugu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake na wanachama wa Chama cha Mapunduzi kwa kura nyingi na za kishindo ili kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, chama dume, dume la mbegu na dume bora.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa niwapongeze Mheshimiwa Yusuf Makamba, kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapunduzi lakini pia nichukue nafasi hiyo hiyo nimpongeze pia Ndugu yetu Mheshimiwa Jaka Mwambi, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi pia nimpongeze Ndugu yetu Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba niwapongeze wote waliochaguliwa kwenye Sekretarieti ya Chama cha Mapinduzi lakini pamoja na hayo naomba nikupongeze wewe mwenyewe, nimpongeze Naibu Spika, Wenyeviti wetu wawili lakini pia nimpongeze na Waziri Mkuu, pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa jinsi mnavyoliendesha Bunge hili kwa umakini na umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa pongezi hizo sasa naomba niende kwenye *agenda*. Nchi hii ya Tanzania ni nchi ya wakulima, wafanyakazi na wafanyabiashara. 80% ya Watanzania ni wakulima na ambao wako vijijini lakini wananchi hawa 80% ambao ni wengi bado kulima kwao kunategemea kilimo cha jembe la mkono kwa asilimia 70% lakini kwa sehemu zile ambazo kuna wafugaji kama 20% hivi wanatumia jembo la kukokotwa na ng’ombe lakini asilimia iliyobaki 10% ndiyo sehemu ambayo wanatumia matrekta. Hata hii 10% ambayo wananchi hawa wanatumia matrekta hii 10% inafika tu kwa sababu ya kuboreshwa na hao wafanyabiashara na wafanyakazi kwa sababu kuna wafanyabiashara pia wanalima lakini pia kuna wafanyakazi wenye uwezo pia wanalima ndiyo walioongeza hii 10% ya kulima na matrekta kwa maana hiyo ingekuwa si hivyo asilimia ya wakulima wanaolima kwa matrekta ingekuwa ndogo zaidi ya 10%.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuzungumza ni kwamba nataka kuishauri nchi hii au Serikali kwa maana Serikali ijitume kwenye kilimo kwa maana ya kupeleka nguvu zake kwenye kilimo ili angalau nchi hii iweze kuondokana na njaa na umaskini. Ninachotaka kuzungumza ni kwamba sasa inabidi tubadilike kwamba tumesema kwamba wakulima wa jembe la mkono ni 70% sasa tunataka 70% hii ibadilike badala ya kutumia jembe la mkono iwe sasa kwa kutumia trekta na 20% kwa wanyamakazi na 10% sasa iwe kwa ajili ya jembe la mkono ili angalau hatimaye nchi yetu ifikie mahali ambapo tunategemea kufika.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ni hotuba nzuri yenye mtazamo wa kuwakomboa Watanzania kwenye nyanja ya kilimo, lakini kama hayo yote yaliyozungumzwa humo yatakuwa yamesimamiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni nchi yenye neema, baadhi ya mikoa mingi ina rutuba nzuri na inapata mvua ya kutosha na maeneo mazuri ya kulima sasa ninachotaka kuzungumza ili tuweze kuondokana na tatizo hili la njaa na umaskini uliokuwepo katika nchi yetu kilimo ndiyo mkombozi mkubwa na kilimo tunachokizungumza ni kilimo cha umwagiliaji maji kwa maana ya kutumia mifereji ya mito, visima sehemu nyingine na wakati mwingine malambo kwa sehemu zile ambazo wanaweza kuchimba malambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi hii inaweza ikafanyika vizuri tu chini ya wataalam wetu wa kilimo au hawa tunawaita maafisa ugani kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi wetu katika sehemu za vijijini ili angalau waweze kufikia katika kilimo hiki. Lakini tatizo nililoliona hapa ni kwamba hawa maafisa ugani wana umuhimu wao katika kuboresha kilimo cha Watanzania lakini kwa bahati mbaya na sisi au Serikali haijawatambua vizuri

kwa maana kwamba, hatujawawekea mazingira mazuri katika kufanya kazi zao kwa mfano maafisa ugani wengi wao ni kwamba wanakaa katika miji au manispaa au jiji.

Lakini sehemu ambazo kilimo kinafanyika ni sehemu za mashambani au vijijini ambapo hawa ndiyo wanatakiwa waende wakatoe elimu kule sasa inakuwa vigumu kwa afisa ugani huyu akae mjini leo hii awe anasafiri kila siku awe anaenda mashambani kwenda kuwapa elimu wakulima na yeye hana usafiri wa aina yoyote hana gari wala pikipiki sasa sioni kama hapa kama ni Serikali inachukua umuhimu kwa ajili ya kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningefikiria kwamba hawa maafisa ugani na sisi tungewajengea maisha bora kwamba wawe na nyumba za kuishi kule kule vijijini lakini pia tuwapatie usafiri kama pikipiki hata baiskeli katika sehemu zile ambazo zinaweza kufikika kwa urahisi ili angalau waweze kufanya kazi zao vizuri vinginevyo tunatwanga maji kwenye kinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hawa wananchi ambao tunasema kwamba na wenyewe wapate elimu ya kutosha ili waweze kulima kilimo cha kisasa, kilimo cha umwagiliaji pia wakulima hawa na wenyewe pia tuwawezeshe kwa maana ya kuwapatia pembejeo kwa maana ya mbolea, madawa na vifaa vya kufanyia kazi na jinsi ya kupata vifaa hivi kwanza, tuwawezeshe kwa maana ya kwamba ikiwezekana tuwapangie utaratibu wa kuweza kupata mikopo katika mabenki yetu ili waweze nao kuingia katika suala hili la kilimo waweze kujikwamua na umaskini huu uliowajaa Watanzania walio wengi ambao ni 80% ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila ya kuweka mikakati ya makusudi kwa ajili ya kukopesha wakulima ili angalau wawe na uwezo wa kununua mbolea na vitu vingine kazi hii itakuwa ni kazi ya bure kwani hawataweza kufika popote kwa vile kila kitu kinategemea pesa.

Kwa mfano, niliposoma tu kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha iliyopita, nashukuru kidogo alizungumzia masuala ya kuongezewa ruzuku ya mbolea kwa wakulima, hata mimi imenipa changamoto kidogo ya kuweza angalau niwahamasishe wananchi wangu sasa waweze kulima mazao ya chakula na ya biashara ili angalau waweze kujikwamua na matatizo waliyokuwa nayo.

Kwa mfano, Morogoro kule tunavyo viwanda vya kusindika mbegu na vya kukamua mafuta kwa hiyo nafikiri na mimi itakuwa ni jukumu langu sasa kuwaambia waweze kulima mazao kama pamba, alizeti, karanga na ufuta ili angalau waweze kujikwamua na shida hii ya umaskini waliokuwa nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi ambalo nataka nizungumze hapa ni kwamba ningeomba pia Serikali sasa iamue kuwekeza katika upande huu wa kilimo katika mikoa ile ambayo ni *fertile,* ninapozungumza kuwekeza ni kwamba aidha, Serikali yenyewe lakini pia wale watu ambao wana uwezo wa kuwekeza aidha, kutoka ndani ya nchi hii au nje ya nchi waweze kuwekeza katika mikoa ambayo ina mabonde mazuri na maeneo

mazuri kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapata chakula cha kutosha kwa ajili ya Watanzania na kingine cha kuuza nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mfano mmoja katika Mkoa wangu wa Morogoro, Mkoa wa Morogoro ni mkoa wenye neema naweza kusema ni mkoa wenye neema kuliko mikoa yote ya Tanzania. Mkoa wa Morogoro ni wa pili kwa ukubwa katika mikoa ya Tanzania lakini pia mkoa huu una milima na mabonde makubwa, milima hii inatiririsha maji mwaka mzima na mabonde tuliyokuwa nayo ni mabonde mazuri tu utakuta hata ndugu zangu Wasukuma ukienda kule utawakuta wamejaa katika mabonde yetu kwa sababu ya kupeleka ng'ombe wao ili waweze kuchungia kwa sababu tunayo ardhi ya kutosha na ardhi yenye mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa huu wa Morogoro umejaliwa pia kuwa na mito 148, mito mikubwa ambayo haikauki kwa mwaka mzima kwa hiyo, pia kuna mabonde 148 ambayo ni ya uhakika. Lakini kama haitoshi Mkoa huu wa Morogoro tunavyo vyuo vya kilimo, tunacho Chuo Kikuu cha Sokoine pale Morogoro, Chuo cha Liti ambacho kinatoa *Diploma* lakini pia tunacho Chuo cha Utafiti wa Mbegu kule Ilonga, Kilosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tukiamua kuwekeza katika Mkoa huu wa Morogoro nafikiri kwanza Watanzania wote wanaweza kupata chakula kutoka Morogoro, lakini pia tukapata chakula cha ziada kuuza nje ya nchi na tukaondokana na hili suala la umaskini. Kama tunataka tuwe *serious* kwanza Morogoro uzuri wake ukiondoa hizo baraka zilizokuwepo za kuwa na mito mingi, mabonde mengi na milima ambayo inatoa maji ya kutosha lakini pia ina hali ya hewa nzuri ambayo tunapata mvua ya kutosha kwa mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama haitoshi Morogoro ni njia panda karibu ya robo tatu ya mikoa yote ya Tanzania kwamba mikoa yote ni lazima upitie Morogoro kwa hiyo, njia ya usafiri ya kupeleka mazao yetu ni kwamba ni rahisi mno kwenda kwenye Jiji letu la Dar es Salaam ambapo pia ipo bandari lakini pia ni mji wa biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia Morogoro ipo karibu na Makao Makuu ya Dodoma, Makao Makuu ya nchi ambayo ni Dodoma sasa tunatafuta nini zaidi ya Mkoa kama huu wenye neema ya kila hali? Kwa hiyo, ningefikiri Serikali huu ushauri ninaoutoa ni ushauri ambao kwanza, sihitaji malipo ni ushauri wa bure, kwa hiyo, ningemwomba Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, achukue ushauri wangu, anaweza akapata sifa ya kutosha yeye na Wizara yake wakiamua tu kuwekeza katika Mkoa wa Morogoro ambao kwanza hakuna gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, karibu kila Wilaya ina barabara ambayo angalau inaweza kupitika kwa ajili ya kusafirisha mazao kilichobaki ni kuboresha tu miundombinu kidogo tu katika sehemu ambazo barabara siyo nzuri sana ili angalau mazao haya yatakayolimwa katika mkoa wa Morogoro yaweze kupelekwa bandarini au kupelekwa Dar es Salaam ambako pia usafiri wa ndege, kiwanja kikubwa cha ndege pia kipo Dar es Salaam ambapo ni karibu kabisa na Morogoro na nafikiri ndugu zangu Wabunge watakubaliana na mimi kwamba Morogoro hakuna shida ya usafiri. Sisi Morogoro yanapita mabasi

karibu 200 kwa siku kwa sababu pale Morogoro peke yake yanatoka mabasi siyo chini ya 100 ya kutoka Dar eslaam kwenda Morogoro, ukichanganya na mabasi mengine yanayotoka labda Dodoma, Mwanza, Singida Mbeya, Iringa na wapi, mabasi ni mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia malori ni mengi, kwa hiyo, hakuna shida ya usafiri. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali kwa makusudi ijikite kwenye kilimo hasa hasa katika Mkoa wa Morogoro ambao hauhitaji kuwa na gharama kubwa katika kuwekeza kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri wangu huu mfupi lakini ni wa muhimu, naomba Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, itilie maanani katika jambo hili ili angalau sasa tusiwe tunalia lia katika masuala ya njaa na umaskini, kwa sababu wanasema utajiri tumeukalia wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja katika Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, naomba nami nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe yangu machache kuhusu Wizara hii.

Kwanza kabisa nimeshatoa pongezi kwa viongozi wengi waliochaguliwa ikiwa ni pamoja na Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Edward Lowassa. Lakini naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Spika kwa jinsi anavyoliendesha Bunge hili kwa umahiri mkubwa na nafikiri kila Mbunge aliyemo humu anaamini kwamba sasa kiti cha Spika kimepata mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nampongeza Mheshimiwa Naibu Spika, akikaa pale kila mmoja anaridhika kwamba tunaye mwanamke mahiri na mwenye uwezo mkubwa. Mheshimiwa Jenista Mhagama naye vile vile nampongeza kwa kazi nzuri, akikaa pale utafikiri amekuwa akikaa pale muda wote na ndugu yangu Mheshimiwa Job Ndugai, naye akikaa pale kwa kweli wote tunaridhika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ofisi yako inafanya kazi nzuri, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwapongeze wapiga kura wangu kwa kunichagua tena kuingia humu ndani ya Bunge kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Imani yao kwangu imekuwa nzuri na imekuwa kubwa na mimi najiona ni mdogo sana kwa sababu hata nguvu zangu za kuweza kuwasaidia na kuwatetea kwa yale wanayoyahitaji pengine najiona sitoshi, lakini wao wanaponiangalia wanaona natosha, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuzungumzia hoja ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwanza naunga mkono hoja. Pia nawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, pamoja na Manaibu wake wawili pamoja na Katibu Mkuu na wasaidizi wake katika Wizara hii. Ziko dalili za *improvement* katika utendaji wao wa kazi hivi sasa tunavyoangalia *speech* hii kuliko ile tuliyoiona miaka michache iliyopita, kwa kweli mimi nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niseme kwamba mapungufu tunayoyaona sasa hivi ni kwa sababu mipango yetu si sahihi, kuna *policy constrains* katika mipango yetu tuliyonayo. Kama mipango yetu ingekuwa mizuri pengine ingekuwepo dira sahihi na salama kuhakikisha nchi hii haiombi chakula hata siku moja katika maisha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, *priorities* zetu haziko *right* kwamba tunapanga kilimo, tunasema *investment* kwenye sekta ya kilimo *will depend on eighty percent of foreign finances, this is wrong*. Kwa sababu wakikataa utafanya nini? Ina maana hiyo mipango yako haiendi, utakwenda kuomba chakula. Kinachoweza kutufanya sisi tuwe *self sufficient* katika chakula ni mipango mizuri na mwelekeo sahihi.

Mheshimiwa Spika, nilivyokuwa nachangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nilizungumzia kilimo cha umwagiliaji kwamba hivi sasa kama sisi Watanzania tungekuwa na *selective programs* za ku-*develop irrigation schemes* katika nchi hii hata tatu, nne au tano kubwa, hizi tunazozungumza sio *irrigation schemes,* mimi kule kwangu labda ninazo *irrigation* kama mbili, tatu hivi. Iko moja ya Tilye kule Kasulu, iko moja ya Msambara, iko nyingine ya Rungwe mpya, hizi *schemes* zote ni ndogo, kila mwaka milioni kumi au ishirini haziishi wala hazianzi kufanya kazi. Kuna moja imemaliza karibu miaka kumi na haijaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tuanzishe *schemes* sahihi ambazo zinaweza kuchukua mabonde makubwa kama Mto Lwiche, Mto Malagarasi na Mto Rufiji, hizi zitakuwa ni *schemes* za umwagiliaji mkubwa kama zile za Misri na sisi tuache kuendesha uchumi kwa unyonge, hatutafika mbali. Tutawasubiri *IMF* wanakuja, kisha watuambie kwamba jamani umaskini wa Tanzania sasa unapungua na sisi tunakwenda tunaringa tunasema umaskini wa Tanzania unapungua kumbe tunadanganywa tu umaskini unapungua wapi! Sisi wote tunatoka vijijini, hakuna asiyetoka kijijini hapa, tunakwenda kule tuna-*witness* umaskini unavyoongezeka, leo tunadanganywa kwamba umaskini unapungua, unapungua wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiambiwa uchumi unakua, *fine* unakuwa lakini kuna *dynamics* za *growth economics* ambazo hizo tunahitaji kuzielewa vizuri zaidi. *Growth* ya uchumi kuwe na *impact* kwenye *poverty reduction* lazima ifikie *level* fulani ikishafikia *level* ile ndipo itakapoanza ku-*impact on the poor*. Lakini hivi sasa haiwezekani kabisa ika-*impact on the poor* kwa sababu mazingira yetu kule hayajabadilika na kwa sababu hayajabadilika umaskini wa watu wetu umeendelea kukua hivyo hivyo na watu wetu wanaendelea kuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mawaziri wetu walitambue hili, waelewe kwamba umaskini unakua vijijini, wala haupungui na haiwezekani ukapungua, umaskini katika nchi za Afrika karibu zote umekuwa unaongezeka. Katika Tanzania *capital flight* ipo *rated at sixty percent* katika nchi za Afrika *compared to six percent* ya *East Asia, South East Asia four percent*, sisi *sixty percent* mpaka *forty*, nchi zingine umaskini umepungua, umefikia mpaka *forty percent*, kwa hiyo, haiwezekani uchumi ukakua kwa utaratibu ambao utaweza ku-*trickle down to the poor* na kupunguza umaskini kwa kiwango tunachohitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ambalo lina-*qualify* hili ni mipango yetu ndani ya Taifa hili. Katika Kamati ya Fedha na Uchumi tumekuwa tunaishauri Serikali kwamba njia rahisi ya kuweza kusaidia uchumi wa nchi hii ni kufanya Wizara ya Mipango isiwe Wizara ya Mipango, iwe ni *think tank* ya kupanga mipango ya nchi hii, kupanga kila sekta ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunaendelea na *business as usual* wale wanapanga, mimi nilikwishasema katika Bunge hili *it is impossible for the Planning Ministry to plan without a budget function, it is practically impossible,* hawana *budget function,* wanapanga kitu gani? *Dynamics* za *plan* katika nchi hii *must change* pengine tuwape *budget function* warudi wakapange kama wanavyotakiwa kupanga. Lakini hivi sasa tunataka *Planning Commission* iwe ndio *think tank* ya nchi hii sio *Planning Ministry,* wenzetu wanapoona hazifanyi kazi zote wanazi-*abandon* watupangie kilimo, waeleze mipango inavyohusiana na barabara, waeleze inavyohusiana na Wizara zingine, wafanye kazi vizuri, afya, elimu na vitu kama hivyo. Wenzetu wameendelea kwa sababu elimu imechukuliwa kama msingi wa kuendeleza kila sekta ya nchi. Watu wetu afya hawana, zahanati zetu hazina dawa, unategemea kilimo, sisi tunakaa hapa tunajiridhisha, kipo kilimo cha kuleta maendeleo katika Taifa, hakuna kilimo cha kuleta maendeleo katika Taifa hili mpaka tuwe tumepanga sahihi kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayasema haya kwa sababu ni mambo muhimu, kama tunataka ku-*prioritize* uchumi wa nchi yetu *we must change fundamentally* mipango yetu, *radically* tuibadilishe, kisha tupange vizuri twende mbele tutakuwa na mafanikio ya maendeleo katika Taifa letu. *As of now,* kwa kweli mimi nakata tamaa, maendeleo yatakuwa magumu kupatikana.

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa nazungumzia habari ya mafuta na nimezungumzia habari ya michikichi, lakini nikaeleza tuna-*import* mafuta, wale wanaoleta mafuta wanasema tunaleta *crude oil,* hakuna anayeleta *crude oil* kutoka Asia, hakuna hata mmoja. Kodi sasa imepanda, nimecheki hesabu zangu, imepanda kutoka asilimia thelathini imefika asilimia arobaini, kodi kutoka Malaysia, tukikupa wewe mafuta ambayo ni *crude* watu wetu hawana kazi. Sisi tunakwenda kuwapa kazi wale tunasema wakulima wetu wa mbegu wafilie huko huko na watu wetu wasipate kazi, *one million jobs* tutazipata wapi? Kumbe *the avenues* za kufanya hayo tuliyokusudia kuyafanya zipo, kesho hatutapata lakini uwezo upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mengi yamezungumzwa katika Bunge hili, pale mashamba ya Mbarali inaonyesha jinsi gani tunavyojikanyaga kanyaga katika *policy stance* za nchi yetu. Mimi niliona huruma sana Mheshimiwa Mbunge wa Mbarali alipokuwa anazungumza. Haya mashamba alikuja mtu akatoa pesa nyingi, mimi bahati nzuri nilipokuwa *UNDP* nilisaidia kupeleka pesa mbalimbali za *Micro Finance Operation,* nafahamu wale wakulima wadogo wadogo wa Mbarali, Madibira na Kapunga wameendelea zaidi kuliko sehemu nyingine yoyote na wamejitosheleza, walikuwa wanapata *support loans* kutoka benki kama *CRDB,* leo unawaambia ondokeni, tena walio-*tender* mara ya kwanza walitoa pesa nyingi bilioni sijui ngapi, baadaye sijui kulitokea matatizo gani Serikali ikaamua impelekee yule aliyetoa ya chini kabisa, aibu kabisa. Tunatoaje mashamba kama yale yanayosaidia watu wengi tumpe mtu mmoja na sisi tunasema sera yetu bado ni sera ya ujamaa, lakini tunaona hawa watu hawana maana wanyang'anyeni, wapeni walio na maana kwa sababu wana hela. Hapana hii *policy* ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie *specific area* ya watu wanaotaka kusaidia kilimo, tunahitaji kitu kinaitwa *public private partnership* katika nchi hii. Watu wajishirikishe katika kilimo ili wasaidie kukiendeleza. Leo mimi nataka kuagiza mbolea kutoka Ulaya siwezi kuruhusiwa, naambiwa usilete mbolea, sisi ndio tutaleta kwa taratibu zetu hata kama *the other fundamentals are interesting,* hivi tunakwenda wapi. Waruhusuni wenye uwezo na pesa zao walete mbolea kwenye nchi hii, nchi hii ni kubwa, mimi nimefanya *research* ya mbolea nchi nzima, kule wanakotumia mbolea nyingi yaani Rukwa, Mbeya, Iringa na Songea, kote kwa sababu ya *intensive use of ammonia* udongo ule umechoka hauwezi kuzalisha kwa wingi, *yield per acre* imekwenda chini, tunahitaji sasa kupeleka hizo sehemu zingine ambazo hazijaathirika wakati wale wanapumzisha udongo wao, watapumzisha tu mashamba fulani fulani ili zitumike sehemu zingine. Kigoma na Tabora ni *sleeping giant,* mabonde yako mengi, naomba tuyatumie ili yaweze kusaidia kuzalisha chakula kingi katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutembee, watu wamesema tutembee, Waziri wa Kilimo na watu wake watembee, *this country* ina *potential* kubwa, tunapolia hatuna chakula, kwanza wanatushangaa, wanasema *is it because of our genes or what is it* kwamba Watanzania hata chakula hawawezi kujitosheleza kwa sababu gani, wanakaa wanazungumza. Mimi nimekutana na wengine wanakaa wanazungumza kwa nini hatupangi? Ukimwambia ukweli ahaa, huyu bwana hafai, hii nchi ni nchi yetu wote, hakuna mtu aliye na hisa zaidi ya mwingine katika Taifa hili, *we all have an interest in the development of this country*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwenye hotuba yake amesema, wale wasioweza watuachie jahazi letu liende vizuri, tunataka jahazi hili liende, wakati wa mchezo umekwisha, sasa ni wakati wa kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya. Hii ari lazima ionekane ikitendeka, watu wafanye kazi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, mimi nakushukuru sana.

**MBUNGE FULANI:** Unga mkono hoja.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Michikichi inahitajika, kule Kigoma tunaweza kulisha nchi hii na tukazalisha dizeli kwa kutumia michikichi peke yake. Tuna kilimo cha kahawa, tunahitaji mashine ndogo ndogo za kukobolea kahawa kule vijijini, watu wanazihitaji. Ili ardhi ile iweze kufanya kazi tuleteeni hivi vitu tunavihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe. Kwa haya machache niliyosema, nina imani tutakwenda, nina imani hotuba hii ni mwanzo tu wa Serikali ya Awamu ya Nne, kazi nzuri wataendelea kuifanya na najua mwaka ujao tutapata hotuba nzuri yenye mwelekeo sahihi wa kubadilisha kilimo cha Taifa hili maana hii michango yote itasaidia Taifa hili kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Serikali na kuwa mchangiaji wa mwisho katika hotuba hii. Mtoto wa mwisho anaweza kuwa na faida au hasara, kwa sababu wenzake wamenyonya sana anaweza kupata maziwa kidogo, lakini pamoja na kupata maziwa kidogo nitanyonya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika pamoja na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji ambao wapo katika Wizara ile kwa kazi nzuri waliyoifanya na wakaileta mbele yetu.

Mimi naleta kilio cha watu wa Dodoma mezani kwa Serikali. Mkoa wa Dodoma ni Mkoa wenye ukame kama unavyoeleweka na mara chache sana kwa mwaka tunapata chakula cha kutosha. Pamoja na kukosa chakula kama inavyotakiwa hatuna zao la biashara. Katika miaka ya nyuma tulikuwa na zao la biashara la zabibu, tulikuwa tunalima sana zabibu lakini baada ya kiwanda cha *DOWICO* kufa na sisi tukafa na tumebaki maskini. Tulipokuwa na kiwanda cha *DOWICO* wananchi walikuwa na uwezo wa kulima zabibu na kuuza *DOWICO* na kujipatia mahitaji ya lazima. *(Makofi)*

Katika kipindi hicho wananchi wengi walikuwa na maisha angalau ya kuridhisha lakini tangu kiwanda cha *DOWICO* kife wananchi wameacha kulima zabibu kwa sababu hawana pa kuuzia. Mahitaji yao ya lazima hawana namna ya kuyapata kwa sababu hawana zao la biashara, wenzetu mikoa mingine wanatafuta pembejeo kwa ajili ya korosho, pamba, tumbaku, lakini sisi hatuna zao la biashara na hatuna zao la biashara kwa sababu hatuna pa kuuzia, sio kwamba hatutaki kulima, tunapenda kulima lakini tutauza wapi, wale wachache wanaolima, wanawauzia wale wafanyabiashara wadogo wadogo wanaouza sokoni na kwenye *stand* ya mabasi.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha kutegemea wauzaji wadogo wadogo kama vile Wamachinga, kwa kweli sio kilimo cha kuinua hali za wananchi, sio kilimo ambacho

kitamfanya mwananchi wa Dodoma awe na maisha bora, naomba ahadi ya Serikali kwamba kama itawezekana basi tupate kiwanda cha mvinyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipo kiwanda pale Hombolo ambacho kilifunguliwa mwaka jana, lakini yule mwenye kiwanda ana mashamba yake, sitegemei kwamba ataweza kununua mazao ya wakulima wote wa zabibu na wakulima wamekata tamaa. Lakini mwaka 2005 niliongea na mkulima mmoja wa zabibu aliniambia pamoja na kuuza kwa hao wauzaji wadogo wadogo alipata shilingi milioni kumi, sasa itakuwaje kama tutakuwa na Kiwanda cha Mvinyo na wananchi wengi wakalima zao la zabibu. Naomba Serikali itufikirie tupate Kiwanda cha Mvinyo hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, wananchi pia wamejitahidi sana kulima alizeti. Lakini walipolima alizeti kama zao la biashara hawakupata soko, wengine alizeti zimeozea majumbani, wengine zimeozea mashambani kwa sababu hawana soko. Kama waliwapata wanunuzi ni wale wanaotoka Singida kwa vinu vidogo vidogo ambavyo vipo Singida, lakini kama wakulima watakopeshwa vinu vya kukamulia alizeti, nafikiri wananchi wa Dodoma watajikwamua kutoka katika hali mbaya ya uchumi waliyonayo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali sasa kupitia *SACCOS* tulizo nazo basi wananchi hawa wakopeshwe vinu vya kukamulia alizeti, kwa sababu mafuta ya alizeti yana soko sana ndani ya nchi na nje ya nchi, pia kama tutapata mikopo ya vinu vya kukamulia alizeti tutajikomboa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Dodoma pia hawapendi kuwa na njaa kila mwaka. Kila mwaka tunalalamika hatuna chakula, sio kwamba hatulimi, tunalima lakini tunalima bila ushauri wa Maafisa Ugani, kila mmoja analima anavyojijua mwenyewe na bado wakulima wanapanda mahindi yaliyopandwa mwaka 1979, mbegu ile ya mwaka 1979, 1980 ndio bado wakulima wanayo katika majumba yao. Mahindi yanayochukua miezi sita ndio yaive, yale yanayohitaji mvua nyingi. Lakini kwa nini wakulima wapande mbegu zisizo bora? Kwa sababu mbegu zilizo bora hatuzipati kwa muda unaotakiwa na pia mbegu bora hazina ruzuku. Mikoa mingine wana ruzuku za pembejeo, lakini Mkoa wa Dodoma hatuna ruzuku za mbegu, sisi hatutaki pembejeo kwa sababu Mkoa wa Dodoma una mbolea na ardhi yetu ni nzuri sana kwa kilimo, lakini hatupati ruzuku kwa mbegu bora zinazotakiwa na za muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo mazao tunayohimizwa kulima kila siku tunahimizwa kulima uwele, mtama, mihogo yaani mazao yanayostahimili ukame na nawashukuru wananchi wa Dodoma wanaitikia wito wa Serikali wa kulima mazao yanayostahimili ukame lakini wananchi hawa wanakatishwa tamaa kwa kukosa soko. Ukisoma hotuba ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kuna tani themanini pale za mahindi, lakini hawakusema tani za mtama, mihogo, ulezi na uwele ni kiasi gani. Sasa kila siku tutawahimiza wananchi kulima mtama, mihogo na uwele lakini soko hawana, *SGR* wananunua mahindi tu na kipindi cha njaa mahindi ndio chakula.

Naomba sasa *SGR* waweze kununua uwele, ulezi na mihogo ili wananchi wanaolima mazao hayo na wao wahamasike kulima mazao hayo. Lakini kama

tutawahamasisha lakini hawatapata soko maana kwetu huku hatuna maghala, maghala yetu yako nje, kwa hiyo, mazao hayawezi kustahimili kukaa muda mrefu. Sasa kama Serikali itatusaidia, tutakapolima mazao hayo yatapata soko, naamini wananchi wa Dodoma watalima mazao hayo kwa hali ya juu sana na hata hali mbaya ya njaa tuliyonayo na umaskini vitapungua kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliposoma pia bajeti ya Wizara ya Kilimo nimeona kuna shamba darasa. Lakini mimi ninavyojua Maafisa Ugani wapo wachache mno, sasa sielewi hao watafanyaje kazi katika vijiji. Wanatakiwa kuwa na shamba darasa katika kila kijiji na sasa sielewi kwamba watakapokuwa na shamba darasa kijiji cha Mvumi, je, kijiji cha Handali au Kikombo kitapataje shamba darasa? Sasa tungepata maelezo mazuri kwamba haya mashamba darasa itakuwaje kwa sababu maafisa ugani wapo wachache na kama alivyosema Mbunge mmoja kwamba watu hawa hawana hata usafiri ni kweli kabisa. Katika Manispaa ya Dodoma kuna gari moja, nadhani la miaka mingi sana iliyopita, likikupita barabarani linatoa moshi kama vile mpira wa gari umechomwa. Kutokana na hali hiyo hata kwenda mwendo wa mbali kutembelea vijiji haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Dodoma Vijijini hawana gari ya ofisi ya kilimo. Sasa sielewi kwamba hawa Maafisa Ugani watawasaidiaje hawa wananchi kule vijijini, watawaelimishaje wananchi kule vijijini kwa sababu maeneo mengi wananchi bado tunalima kama tulivyolima miaka kumi au ishirini iliyopita. Hatujui kulima kilimo cha kisasa kwa sababu Maofisa Ugani hatuwaoni na kama tunawaona wanatembelea maeneo yanayopitika, maeneo yasiyopitika Maafisa Ugani hawafiki. Naiomba Serikali na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, wafikirie hilo kwamba Maafisa Ugani lazima wafike katika vijiji na wawasaidie wananchi kulima kilimo kilicho bora lakini wasipowasaidia wananchi ushauri wa kulima kilimo kilicho bora tutabaki tunapiga kelele tuna njaa kila kukicha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala la majembe ya kukokotwa na ng'ombe. Wananchi wa Dodoma ni wafugaji pamoja na kwamba ni wakulima lakini pia ni wafugaji lakini hawana ujuzi na hawana uwezo wa kununua majembe hayo. Naomba sasa kama kuna uwezekano Serikali ione uwezekano wa kuwakopesha wale ambao wameanzisha *SACCOS*, wakopeshwe majembe ya kukokotwa na ng'ombe na matrekta ikiwezekana kwa sababu kilimo kinalipa, kwa hiyo, wakikopeshwa naamini kabisa kwamba watarudisha hizo pesa. Lakini pia katika Mkoa wetu wa Dodoma kuna Mto Bubu ambao unafaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji na nimeona katika bajeti hii Serikali imeonyesha nia thabiti ya kuhamasisha wananchi kulima kilimo cha umwagiliaji.

Naomba sana Mto Bubu uwe katika mpango huo, mabonde ya Mima katika Wilayani Mpwapwa yawe katika mpango huo wa Serikali wa kilimo cha umwagiliaji. Mabonde ya Mpwapwa yanatosha kabisa kulisha Dodoma. Mto Bubu unatosha kabisa kulisha Mkoa wa Dodoma. Kwa hiyo, kama tutapata kilimo cha umwagiliaji katika Mto Bubu na Mabonde ambayo yapo Wilayani Mpwapwa nina hakika Serikali haitahangaika tena kutafuta chakula kwa ajili ya Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nimalizie kwa kumpongeza Mheshimiwa Mkuu wetu wa Mkoa kwa mikakati mizuri aliyoiweka kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha Mkoa wa Dodoma. Tupo pamoja naye na tunamuunga mkono kwa asilimia mia moja kwa jitihada zake anazofanya kuukomboa Mkoa huu kwa mikakati mizuri aliyoiweka kwa ajili ya kufanikisha kilimo katika Mkoa wa Dodoma na kuondoa njaa kabisa katika Mkoa wa Dodoma. Lakini mpango wake huu utafanikiwa tu kama atapata mkono wa Serikali, kama kilimo cha umwagiliaji kitatiliwa maanani na kama mazao ya biashara ambayo tunayategemea, yatapata soko kiuhakika Serikali itusaidie katika kujenga Kiwanda cha Mvinyo na tukikopeshwa vinu vya kukamulia mafuta ya alizeti tutafanikiwa. Nina hakika Mkoa wa Dodoma tutakuja kusikia njaa masikioni mwetu tu lakini hatutakuwa na njaa tena.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache nakushukuru tena na pia naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana. Sasa ni zamu ya upande wa Wizara kujibu hoja. Kwa hiyo, kwa jinsi tulivyokubaliana ataanza Naibu Waziri, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, kwa robo saa na atafuatiwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Christopher Chiza kwa robo saa na mtoa hoja mwenyewe kwa muda wa nusu saa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE):** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Wizara yetu ya Kilimo, Chakula na Ushirika ambayo iliwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Waziri hapo jana. Napenda nitangulie kusema kwamba naiunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kwa kutoa hotuba tokea Bunge lako Tukufu hili lianze katika Awamu hii ya Nne, ningependa nichukue fursa hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivi karibuni kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nichukue fursa hii kuwapongeza viongozi wote waliopata nyadhifa mbalimbali nikianza na Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais lakini vile vile kwa kuidhinishwa na Bunge letu kwa kura nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wetu pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, Baraza la Mawaziri lote kwa ujumla nawapongeza kwa nyadhifa hizo ambazo tumeaminiwa na wananchi pamoja na viongozi wetu pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kipekee napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu kwa heshima aliyonipa ya kuniteua kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Napenda nimshukuru sana na kusema naahidi kwa mara nyingine tena kuwa nitatumia uwezo wangu wote kuweza kutekeleza majukumu ambayo nimepewa chini ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nataka nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba wananchi wangu wa Jimbo la Chilonwa walimpa kura nyingi sana Mheshimiwa Rais wetu kwa asilimia 94.8. Kwa hiyo, tuna imani kubwa sana na uongozi wake. Lakini pia niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Chilonwa kwa kunirudisha hapa Bungeni kwa mara ya tatu kama Mbunge wao, nawaahidi ushirikiano mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwasemee wananchi wenzangu wa Chilonwa hapa kwa sababu mimi ndiyo mwakilishi wao, kwa kuishukuru Serikali kwa kukubali ombi letu la kuigawa Wilaya ya Dodoma Vijijini kuwa Wilaya mbili za Bahi na Chamwino na Jimbo letu la Chilonwa liko ndani ya Wilaya ya Chamwino. Tunadhani katika mgawanyiko huo tutafanya kazi kwa karibu zaidi na Serikali. Kwa hiyo, nawasemea na kuishukuru Serikali kwamba imetufanyia jambo zuri sana. Tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, nataka tu niseme kwamba nimesimama hapa kumsaidia Mheshimiwa Waziri katika kuchangia hoja yake kwa kutoa maelezo kadhaa katika baadhi ya maeneo na eneo ambalo tumekubaliana nijielekeze nalo ni katika eneo la Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kwanza nitambue umuhimu wa wachangiaji wote waliochangia katika hoja hii kwamba wote ni wanaushirika wazuri kwa sababu wao ndiyo wanaishi na wanaushirika kule vijijini. Kwa hiyo, mchango wao wote sisi tunauthamini kwa sababu unatoka kwa watu ambao wanahusika na ushirika moja kwa moja. Tunawashukuru sana wale waliochangia katika hoja hii na sisi tutazingatia hayo yote waliyotueleza hapa. *(Makofi)*

Mchango mwingi uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika eneo hili kusema kweli umeelezea matatizo na tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wametoa ushauri ambapo mimi nataka kusema kwamba ushauri ule tutauthamini sana na tunauzingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pengine niseme tu kwamba matatizo ya Vyama vya Ushirika ni ya kihistoria kidogo kwa sababu kama sote na ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengine wamesema hapa vyama vya ushirika vilikuwa vikifanya kazi nzuri sana huko nyuma na wengine wametoa mifano mizuri tu. Lakini kutokana na mabadiliko ya hapa na pale nadhani hapo katikati vyama vya ushirika vikapata kudhoofika kidogo na ndiyo maana Serikali ikaanza kuchukua hatua za kadhaa wa kadhaa za kuweza kurekebisha kasoro hizo ambazo zilikuwa zimejitokeza na moja ya hatua iliyochukuliwa na Serikali kama sote tutakavyokumbuka mwaka 2000 Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu, aliunda Kamati Maalum ya kumshauri juu ya kutafuta matatizo na kuyatafutia ufumbuzi na Kamati ile ilipokamilisha kazi yake

iliandaa mapendekezo yako kwenye taarifa na kutokana na mapendekezo hayo sasa ndiyo yamezaliwa maelekezo mengine ambayo sasa hivi tunadhania tukiyatumia vizuri yanaweza yakasaidia kwa kiwango kikubwa sana kutatua matatizo ya Ushirika hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya maandalizi yaliyofanyika ilikuwa kwanza ni kuandaa Sera ya Ushirika mpya ambayo ilitakiwa ijielekeze katika mwelekeo mpya wa Ushirika na kuainisha matatizo mbalimbali na kutafuta suluhisho la matatizo hayo. Kwa hiyo, sera hiyo ilitungwa mwaka 2002. Lakini sera pekee yake ikaonekana haitoshi ikabidi itungwe sheria mpya ya ushirika ambayo sasa utekelezaji wake ndiyo tunausimamia hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme kwamba Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani alikuwa amependekeza itungwe sheria mpya ambayo inakwenda na wakati. Mimi nasema hakuna sababu. Kwa sababu sheria hiyo mpya ilitungwa mwaka 2000 na imeanza kutumika mwaka 2004. Kwa hiyo, bado ni sheria mpya kabisa. Kwa hiyo, suala la kuwa na sheria mpya kama walivyokuwa wamependekeza wenzetu wa upande wa Kambi ya Upinzani nadhani sasa hivi hakuna haja hiyo. Kinachotakiwa ni kutekeleza vipengele vilivyomo katika sheria hiyo mpya.

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na sheria hiyo mpya ilionekana ni lazima sasa tuandae mkakati kamilifu ambao utazingatia sera pamoja na sheria na mkakati huo ndiyo tunauita kwamba ni mkakati wa mageuzi na *modernization* ya ushirika ambao umeshaanza kutumika kuanzia mwaka jana na utekelezaji wake unaendelea katika awamu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na niseme kwa ujumla wake hapa tukizingatia utekelezaji wa programu hiyo matatizo mengi pamoja na ushauri uliotolewa hapa na Waheshimiwa Wabunge kwa kiwango kikubwa utakuwa umekidhi uendeshaji mzuri wa vyama vya ushirika. Lakini sitaki niseme kwamba labda utekelezaji wa *program* hiyo utakuwa ndiyo muarubaini wa kuondoa matatizo yote ya vyama vya ushirika hapa nchini, la hasha. Ninachojaribu kusema hapa ni kwamba matatizo mengi ambayo tayari hata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri aliyaeleza yameainishwa katika hiyo programu. Nataka kutoa ushauri hapa sambamba na ushauri ambao Waheshimiwa Wabunge wameutoa kwamba tukizingatia utekelezaji wa hiyo programu kwa kiwango kikubwa sana tutakuwa tumetatua matatizo yanayousibu Shirika hapa nchini.

Meshimiwa Spika, sasa baada ya maelezo hayo ya utangulizi labda sasa nijielekeze kwenye hoja mahsusi zilizokuwa zimetolewa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Gideon Cheyo ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, katika taarifa ya Kamati, moja ya kipengele ambacho kilisisitizwa sana kule ilikuwa ni kwamba Serikali iendelee kuimarisha ushirika ili kuwapa wakulima nguvu katika kupanga bei za mazao na hili ni jambo la msingi na sisi tunasema kwamba tunalizingatia kwa sababu ukishakuwa katika Umoja wa Vyama vya Ushirika vilivyo imara. Kwa hiyo, hili suala la kutafuta masoko, suala la kuwasiliana na

wanunuzi mbalimbali, suala hata hili la kutafuta pembejeo kama ambavyo wengine walikuwa wameshasema na kama nitakavyosema hapo baadaye kusema kweli kupitia vyama vya ushirika ambavyo ni imara inaweza ikawa ni kazi rahisi. Kwa hiyo, tunashukuru kwa pendekezo hili na sisi tunachotaka kusema ni kwamba tutalizingatia hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia lipo pendekezo ambalo lilitokana na taarifa hiyo ya Kamati ilikuwa kwamba Wizara izipatie umuhimu unaostahili shughuli za ushirika ndani ya Wizara na hii nataka tu niseme kwamba ulikuwa ni ushauri mzuri, lakini mimi kwa sababu ndiyo nafanya kazi ndani ya hiyo Wizara nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kupitia Bunge lako Tukufu kwamba shughuli za Idara ya Ushirika ndani Wizara ya mpya ya Kilimo, Chakula na Ushirika zina uzito wa hali ya juu sana. Kwa sababu kwanza, hiyo programu imeingizwa katika ule mkakati mkubwa sana wa utekelezaji wa maendeleo ya kilimo kama ilivyoelezwa kwenye hotuba hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata mafungu ya fedha katika programu hiyo imepangiwa. Kwa hiyo, naomba kuwatoa wasiwasi kwamba pengine shughuli za ushirika zitakuwa zimedhoofika kwa kuwa ziko katika Wizara ambayo ni kubwa kidogo. Kwa hiyo, nataka niwatoe wasiwasi wenzangu na sisi tunataka tuseme kwamba tutafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa sana ili kuweza kuimarisha shughuli za ushirika.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo lilielezwa na hiyo taarifa ya Kamati ilikuwa ni kwamba Serikali isambaze kwa lugha rahisi elimu kuhusu sera pamoja na huu mkakati niliousema. Kazi hii ndiyoi tunaendelea kuifanya wenzetu wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania pamoja na Chuo cha Ushirika wanaifanya hiyo kazi wanadhania kwamba ili watu waweze wakaelewa vizuri sheria lazima iwe katika lugha ya Kiswahili ambayo wananchi wanaweza wakaitafsiri kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, liko suala ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana ni suala la kuvidhamini Vyama vya Ushirika hususan *SACCOS* kuweza kufanya shughuli za kusambaza pembejeo na kudhamini vyote vikaingia katika utaratibu wa soko la kusambaza pembejeo.

Mheshimiwa Spika, sisi tunachotaka kusema katika hili Serikali haina kipingamizi. Isipokuwa tunachosema kwa sababu ile ni biashara na ina taratibu zake na masharti. Kwa hiyo, vyama vitakavyokuwa vimekidhi masharti, vina uwezo wa kifedha vitaruhusiwa kuweza kuingia biashara ya kusambaza pembejeo kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge walikuwa wameisemea na hii imezungumzwa kwa uchungu sana na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana na hapa mwisho na Mheshimiwa Felister Bura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme kwamba hilo si tatizo na kazi yetu kubwa ni kuviimarisha hivi Vyama vya Ushirika hususan *SACCOS* ili viweze vikawasaidia wakulima katika kutatua matatizo yao mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kwamba Serikali itunge sheria mpya ambayo tayari nimeishalitolea maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ieleze hatua zitakazochukuliwa dhidi ya wale wanaofilisi Vyama vya Ushirika. Tunazo hatua mbalimbali za kuwafikisha Mahakamani, lakini ikifikia mahali haiwezekani mrajisi wa vyama vya ushirika anayo mamlaka ya kuwa- *sur-charge* yaani kwenda kuwafilisi mmoja mmoja mali zao mpaka waweze kufidia zile mali za Vyama vya Shirika walizoziiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pengine nilisemee suala la Nyanza ambalo Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mbunge wa Tabora Kaskazini, amelizungumzia.

Kwanza tunapenda tumshukuru sana kwa jinsi ambavyo amekuwa karibu sana katika kushughulikia suala hili na sisi tunataka tumuunge mkono tu kwamba sisi tusingependa Nyanza ife isipokuwa tungependa tusaidieni katika kutatua matatizo yake. Ndiyo maana hivi sasa tumeshapeleka timu yetu ya wataalam kule Mwanza, wakija na ile taarifa ambayo itakuwa imeeleza vipengele mbalimbali ambavyo vinatakiwa tuvitekeleze. Basi zile hatua ambazo Mheshimiwa Dr. James Msekela, pamoja na Mheshimiwa Richard Ndassa, walikuwa wamependekeza Serikali haitasita kuchukua hatua. Aidha, kuweka hiyo *Care taker Committee*, kumkasimu madaraka Mkuu wa Mkoa pamoja na Mamlaka ya Mrajisi inaweza ikatumika. Lakini tunadhani kwamba tuchukue hatua kwanza za kwenda kufanya uchunguzi. Kwa hiyo, nataka niwatoe wasiwasi katika hili.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ilikuwa ni kufikisha elimu ya ushirika kwa walengwa na kwa wakati. Hilo limezungumzwa na watu wengi tu, akiwemo Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Maafisa Ushirika kupatiwa mafunzo amelizungumzia Mheshimiwa Wilson Masilingi na Mheshimiwa Monica Mbega tena. Hapa nasema kwamba katika utaratibu wa hiyo programu ya mageuzi na *modernization* ya ushirika hayo yote yatazingatiwa na kusema kweli sasa hivi mafunzo yamekwishaanza katika maeneo mbalimbali kwa kuwapa elimu Maafisa Ushirika waweze wakasimamia uchaguzi wa Vyama vya Ushirika ili wapatikane viongozi walio bora na wanaowajibika. Kwa sababu matatizo yetu makubwa sana katika Vyama vya Ushirika ni uongozi usiowajibika na wasio waaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la uchaguzi sasa hivi litatiliwa mkazo. Kwa hiyo, hata Maafisa Ushirika wanaokwenda kusimamia uchaguzi wanapewa mafunzo maalum. Lakini baada ya kuchaguliwa uongozi mpya vile vile unapewa mafunzo maalum na hivyo hivyo, wanachama wetu kabla hata ya kuanza Vyama vya Ushirika ambalo sasa hivi tunasisitiza sana Vyama vya Ushirika vya Msingi ili viwe imara elimu ya ushirika imepewa kipaumbele kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie ombi moja mahsusi ambalo lilitolewa na Mheshimiwa Richard Ndassa kuhusu uuzwaji wa jengo la Nyanza ambapo imeelezwa hapa kwamba liliuzwa kwa bei ya chini kuliko jinsi ambavyo ilivyokuwa na sisi kwa

kweli tumelifuatilia hilo. Ni kwamba jengo lile kwanza liliuzwa mwaka 2002 na tathmini imefanyika mwaka huu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaona hapo kutakuwa na tofauti hizo. Lakini pamoja na hilo tunasema kwamba maadam timu yetu imekwenda kuchunguza matatizo ya Nyanza jinsi yalivyo na hili litakuwa tatizo mojawapo ambalo watalichunguza watuletee taarifa. Ikija hiyo taarifa pamoja na ujumla wake masuala ya Nyanza yatasimamiwa sasa na kuweza kutafuta ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme tu kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia udhaifu wa usimamizi wa Vyama vya Ushirika. Nataka niseme kwamba yote haya tutayasimamia kutegemeana na programu hii tunayoitekeleza. Lakini niseme tu kwamba mengi ambayo mmeyaeleza hapa yalikuwa ni ushauri tumeuchukua na sisi tutayathamini sana na tutayatumia.

Mheshimiwa Spika, lakini niahidi kwamba pamoja na mengine ambayo wataongezea wenzangu watakapokuja hapa tunaahidi tu kwamba tutaandaa majibu kikamilifu kwa kila Mbunge na hoja yake na kuwapa majibu ambayo tukishaweka yale yanakuwa kama ni ahadi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Bunge bado linaendelea, mtaendelea kuyafuatilia kwa njia mbalimbali kwa kuja kutuona ofisini na kutukumbusha kwa njia ya maswali. Lakini nataka niahidi kwamba michango yote mliyoieleza hapa tutaizingatia. Tunawaomba sana sana tukubaliane.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, mimi niungane na mwenzangu kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi mnono, mzito alioupata na hatimaye kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi. Naomba pia nimpongeze Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, naye kwa ushindi wake na kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia na wewe mwenyewe na Naibu Spika wako, niwapongeze kwa kuchaguliwa kwa kishindo katika Bunge hili. Aidha, nawapongeza pia Mawaziri, Manaibu Mawaziri wenzangu na wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais ambao wamepewa nafasi ya kusimamia dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimshukuru kipekee Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri na mimi ninamuahidi kama nilivyomuahidi siku ile nikiapa kwamba nitajitahidi kwa msaada wa Mungu kufanya kazi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba kwa kuwa na mimi ni mara yangu ya kwanza katika Bunge hili niwashukuru wananchi wa Jimbo la Buyungu na wale wa jirani wa Jimbo la Muhambwe ambao ndiyo walionileta katika Bunge hili walipouliza tumtume nani Bungeni, nikasema mimi hapa wakakubali. Nawashukuru huko waliko wanaonisikia na kuniona kwamba nao sitawaangusha katika kazi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimshukuru kipekee zaidi Waziri wangu, Mheshimiwa Joseph Mungai, kwa sababu anaendelea kunilea, kufundisha kazi hii ya Unaibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba na mimi nijielekeze sasa katika kuchangia hoja hii ambayo kwanza naiunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba wachangiaji walikuwa wengi na hoja zilikuwa nyingi na haiwezekani katika muda huu wa robo saa nikazijibu zote. Lakini ninaahidi kwamba nitazizungumza kwa ujumla. Baadaye tutapata nafasi katika *matrix* tutakayotoa Kiwizara kila mchangiaji atapata jibu kwa maandishi tena kwa kina kuhusu yale mambo yote ambayo ameyauliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nichangie maeneo makubwa mawili katika hoja zilizohusu kilimo cha umwagiliaji ambacho kimegusa kila mtu na pia nitazungumzia matumizi ya zana za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja kubwa ya umwagiliaji. Naomba kwa haraka haraka kwa sababu wachangiaji ni wengi na najua sitajasema kila mmoja amesema nini. Niwatambue waliozichangia kwa haraka haraka ni Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa John Malecela,

Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Bujiku Sakila na Mheshimiwa Dr. Laus Mhina.

Wengine ni Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Mohamed Sinani, Mheshimiwa Paschal Degera na Mheshimwia Lucas Selelii. Nina hakika orodha itaendelea kutajwa na Mheshimiwa Waziri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie kwa ujumla suala la kilimo cha umwagiliaji ambalo lizungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba niseme kwamba ushauri wote uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge hapa tumeuzingatia na tutaufanyia kazi. Lakini pia naomba niseme kwamba kama nilivyosema asubuhi ya jana kwamba tumeandaa *National Irrigation Master Plan* ambayo ndiyo inatupa dira ya uwekezaji katika kilimo hiki cha umwagiliaji, uwekezaji katika ngazi ya wakulima wadogo, uwekezaji katika ngazi ya wakulima wa kati na uwekezaji katika mashamba makubwa ya kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata katika orodha tunazowapa zinazingatia maeneo hayo makubwa matatu. Napenda niwaambie kwamba leo hii sitataja miradi yote kwa sababu itakuwa ni kazi kubwa. Lakini nawaahidi kwamba baada ya Bunge hili au wakati linaendelea basi tutatengeneza orodha ya ile miradi ambayo tutaitekeleza kwa mwaka huu na miradi mingine ambayo tutaendelea kuipa kipaumbele katika Mpango huu wa *ASDP* ili kila mmoja wenu aweze kujua kwamba eneo langu liko wapi. Nawaahidi Waheshimiwa Wabunge kwa sababu najua hilo mmelizungumzia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la uwekezaji mdogo katika kilimo cha umwagiliaji maji. Sisi katika utafiti wetu tuliofanya na kama mtakavyoona katika *National irrigation Master Plan* tumekadiria kwamba ili Taifa hili liweze kujitosheleza hususan katika zao la mpunga ambalo tunaona ni zao kubwa sana tunahitaji eneo la takriban hekta 400,000 ziwe zinalimwa na kumwagiliwa na ikiwezekana ziwe na *double crop*. Sasa tukifanya bidii kufikia hapo tunaweza tukafika mahali ambapo tunasema Taifa sasa linaweza likapata mchele wa kuwatosheleza wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ili tufikie hapo tunasema lazima uwekezaji uwe kiwango cha bilioni 30 kila mwaka. Sasa kiwango hiki ni kikubwa mno ukilinganisha na mapato yetu ya Serikali. Kwa hiyo, wakati mwingine tunaposusua si kwamba tunasusua labda kwa sababu hatutaki kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji na kwa kutambua hili ndiyo maana basi tunajitahidi katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kutafuta vyanzo vingine mbadala ili miradi mingine iendelee kutekekezwa

pamoja na zile fedha zinazotengwa na Serikali, lakini miradi mingine iwe inaendelea. Nina hakika baadhi yenu ni mashahidi.

Mheshimiwa Spika, najua katika wiki hii baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, nimewapelekea barua nikiwafahamisha kwamba tumepokee shilingi 1,345,000,000/=kutoka katika Mfuko wa Msaada wa Pamoja wa Chakula Tanzania na *Japan Food Aid Counterpart Fund.* Tunachofanya sasa ni kwamba wataalam wetu ambao wako katika ofisi za Kanda ambazo nina hakika mmekwisha kuzifahamu tume-*encourage,* tunawaambia wawatembelee katika Halmashauri ili waweze kuibua miradi ambayo inafaa kwa kupewa fedha. Maana tulipoanza mpango huu wa *DADPs,* mimi niliambiwa kwamba miradi mingi iliyoletwa haikuwa miradi, ilikuwa ni orodha tu, ilikuwa ni *shopping list.* Sasa ile hata wale wanaotoa fedha ilikuwa ni taabu sana kutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachofanya sasa ni kuhakikisha kwamba Wizara yetu ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kutumia wataalam wetu walioko katika Ofisi za Kanda wanakwenda Wilayani na wanakwenda vijijini kama alivyosema Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi katika uchangiaji wake, kuwasaidia wananchi kuibua miradi hii.

Sasa wanapoibua si tu kwa ajili ya kuombea fedha hizi ambazo Mheshimiwa Waziri ameomba katika Bajeti, tunaibua miradi ile ikiwa katika *standard* ambayo ukipeleka katika *Food Counterpart Fund* waseme ndiyo wanatusaidia pesa kama hizo ambazo tumewasaidia katika Majimbo tisa wale Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata najua pale walipo wanafurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunapeleka kwenye vyanzo vingine kama *TASAF* na *NGO's* na hii ndiyo njia nyingine Waheshimiwa Wabunge ya kupata fedha mbali ya hizi fedha ambazo mnazisoma katika kitabu na mimi nataka niwahakikishie kwamba tuna uwezo wa kuwaandalia miradi vizuri na hata mimi mwenyewe nina uwezo huo tena wa kutosha. Basi nawaomba mtutumie ili tuweze kusaidia Serikali pia kutafuta vyanzo vingine.

Mheshimiwa Spika, mabonde ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumzia, napenda niwahakikishie kwamba mabonde yote haya tunayatambua yamo katika *National Irrigation Master Plan* na lengo letu si kutawanya fedha kama tulivyokuwa tunafanya miaka mingine, tunataka angalau tuangalie ni mabonde gani ambayo tunaweza kupata *quick win,* ukiingiza fedha usiingize nyingi sana, lakini tuanze kupata matokeo haraka haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo si kwamba tutaacha maeneo mengine. Maeneo mengine tunaendelea kuyaendeleza kwa taratibu hizi za kawaida ambazo nimesema. Kwa hiyo, kwa kipaumbele tunasema kwanza tutaanza na kukarabati *schemes* zilizochakaa kwa sababu ni rahisi kuzishughulikia zile ambazo zimechakaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu *priority* namba mbili, itakuwa ni kuvuna maji katika majaruba na katika malambo na kujenga mabwawa mengine makubwa makubwa na ya kati. Ndiyo maana basi hata *RUBADA* ambayo watu walikuwa wanasema *RUBADA* sasa

inafanya kazi gani, tunasema tutaipa kazi ya kuhakikisha kwamba inaandaa miradi, inapima mashamba kwa ajili ya wawekezaji ambao watalima kilimo cha kibiashara.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijikite katika suala la teknolojia hii ya uvunaji maji. Tumesikia tangu asubuhi nafikiri ilikuwa ni Dodoma na maeneo mengine, wamezungumzia sana kuhusu mabwawa ambayo yako katika Mkoa wa Dodoma yapo katika *Central Plateau*. Nataka niwahakikishie kwamba mradi wa *PIDP* ambao unaendelea hivi sasa huo tuliuandaa mahsusi kwa ajili ya kuendeleza hii *Central Plateau* ambayo maji yake yanapatikana kwa shida.

Sasa pamoja na kwamba mradi huu unaenda ukingoni, lakini tumeshajifunza, tumepata *experience* ya kutosha na baadhi ya vyombo vipo. Tutakachofanya ni kuhakikisha kwamba tuna-*tape experience* ya mradi huu wa *PIDP* kwenda mbali zaidi ya hii Mikoa tuliyokuwa tunashughulikia ya Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga na sehemu za Mwanza ili maeneo mengine yanayofaa kwa kuvuna maji tuweze kupeleka teknolojia hiyo. Kwa hiyo, nina hakika maeneo yote hayo tutayafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niseme pia kwamba mabonde haitawezekana tuyataje yote hapa. Nitakapowakabidhi *master plan* mtaona ni mabonde gani ambayo tumesema tunataka tujikite huko tuki-*invest* hela ziingie. Yale ambayo hatuyatajitaji kila mara msifikiri tumeyasahau. Kwa mfano, Bonde la Bubu hilo tunayo na maandishi yake ninayo kabisa. Kwa hiyo, msije mkafikiri labda tumesahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Bonde la Ruiche Mkaoni Kigoma hatujasahau hilo, kuna Bonde la Ngono kule Bukoba, ni bonde ambalo watu wanafikiri tumelisahau, lakini ni mabonde ambayo tunayo kabisa na ukifungua *master plan* yetu utayaona pamoja na mabonde mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kidogo kuhusu matumizi ya zana za kilimo. Mheshimiwa Waziri alisema takriban asilimia 70 ya Watanzania wanaolima wanatumia jembe la mkono, asilimia 20 wanatumia wanyama kazi na asilimia 10 tu ndiyo wanatumia matrekta.

Mheshimiwa Spika, hii ni kutokana na ugumu au ughali wa suala lenyewe. Maana yake matrekta tumesikia wachangiaji wengi wakisema kwa nini matrekta yasiletwe, yakasambazwa tu Tanzania nzima. Bado suala liko pale pale kwamba Serikali haijawa na fedha ya kuweza kununua matrekta ya kusambaza Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tunachosema ni kwamba, tuzisititize zile njia za kupata fedha za kununulia matrekta. Huu Mfuko wa Pembejeo, kwa mfano, baadhi yenu mmeutumia na ndio tunawa-*encourage* kwamba, huu Mfuko wa Pembejeo tuutumie na mimi kwa makusudi kabisa, nimewaomba wataalamu walete *pamphlets* ili waonyeshe ni hatua zipi zinazotakiwa kupitiwa katika kukopa katika Mfuko huu wa pembejeo. Maana baadhi yetu nimesikia kwamba, hatuujui Mfuko wa Pembejeo. Lakini Mfuko huu unatusaidia kukopa ili tuweze kununua matrekta na *spare* za kufufua matrekta yetu yaliyoharibika, pamoja na zana za kilimo nyingine.

Kwa hiyo, tunahamasisha sekta binafsi kuomba mikopo kutoka katika Mfuko huu wa pembejeo na hasa kwa ajili ya kuanzisha vituo vya kukodisha matrekta. Haiwezekani kila Mtanzania akawa na trekta na hata tukiwa na trekta kila mmoja, labda tutalima mashamba yetu. Kwa hiyo, tunachohamasisha ni kwamba, watu wajiunge katika vikundi hata katika hizo *SACCOS* tulizokuwa tunasema ili waweze kukopa na kuanzisha vituo vya kukodisha matrekta na kuwapatia wengine. Nawashukuru sana wale ambao wameshaanzisha vituo hivi, lakini ni wachache sana na wengi ni Mashirika ya Dini ndio wamejitahidi kufanya hivyo, lakini hata wale wengine ambao si Mashirika ya Dini, naomba mfanye hivyo.

Kuhusu uingizaji nchini wa matrekta yaliyotumika ya bei nafuu, baadhi ya Makampuni na watu binafsi, wamechukua fursa hii kuingiza nchini matrekta yaliyotumika. Makampuni hayo ni pamoja na *Tanzania Pharmacy Service Centre, Tractors Limited* na *Farmcom Limited*. Labda tu niseme kwamba, naomba mtumie Ofisi yetu, Idara ya Umwagiliaji na Huduma za Ufundi, kwa sababu tunacho Kitengo cha Huduma hii ya *Mechanisation.* Ukitaka kujua ni matrekta gani yanayoweza kulima katika eneo lako, ni *horse power* gain, naomba myatumie.

Mheshimiwa Spika, nadhani muda mnaotupa ni mfupi, lakini naomba kuunga mkono hoja hii, nawashukuruni sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja yangu. Nakushukuru sana kunipa *bonus* kidogo ya kutaja majina, kwa sababu wachangiaji kwa kweli wamekuwa wengi sana. Katika kuanza kuhitimisha hoja yangu, napenda niseme nashukuru kwa fursa ya pekee, niliyopata leo, ambayo sijawahi kupata katika Bunge hili kwamba, mwanzoni mwa kikao cha jioni hii, nilijikuta ni Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni. Nashukuru sana kwa fursa hiyo, nafahamu wenzangu walikuwa katika Kikao cha Kabineti na walikuwa wanamalizia malizia mambo, ikaniangukia bahati yangu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru sana wote ambao wamechangia katika hoja hii. Waliochangia kwa kuongea humu Bungeni ni 34, nao ni wafuatao: Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Salim Khamis, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, wakifuatiwa na Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, Mheshimiwa Brigadia Jenerali Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge na Mheshimiwa Ephraim Madeje.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa John Magale Shibuda, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Adam Malima,

Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Phares Kabuye, Mheshimiwa Juma N'hunga, Mheshimiwa Festus Limbu, Mheshimiwa Dr. Omar Nibuka, Mheshimiwa Kilonsti Mporogomyi, Mheshimiwa Felister Bura na Manaibu wangu, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje na Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza. Wote nawashukuru kwa michango yao na hususan nawashukuru sana hawa Mawaziri wenzangu katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa kunipunguzia sana maelezo ya kutoa hapa Bungeni. Wametoa maelezo mazuri sana na mimi napenda kurudia kwamba, hatuwezi kueleza kila kitu, mengine tumeyachukua tutayafanyia kazi. Mimi nitapata nafasi ya kujazia maeneo machache, ambayo wenzangu tulikubaliana hayo niyashughulikie.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa John Malecela, Mheshimiwa Dr. Lucas Siyame, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Kanal Feteh Mgeni, Mheshimiwa Kiumbwa Mbaraka, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Phillemon Sarungi, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Phillip Marmo, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Abdukarim Shah, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Aziza Ally, Mheshimiwa Dr. Cyril Chami na Mheshimiwa Juma Said Omar.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Capt. George Mkuchika, Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Abbasi Mtemvu na Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka. Wote nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo ambao tulipata maoni yao kutokana na michango yao wakati wa hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nao ni wafuatao: Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa John Samwel Malecela, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Meryce Emmanuel na Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Raphael Ligallama, Mheshimiwa Devotha Likokola, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Godfrey Zambi,

Mheshimiwa Joyce Massunga na Mheshimiwa Laus Omar Mhina. Wote tunawashukuru kwa michango yao, tuliipokea kutoka kwa Ofisi ya Waziri Mkuu na pia afisa wetu alikuwepo kuchukua na kila wakati miongoni mwetu sisi Mawaziri mmoja, alikuwepo Bungeni wakati wa hoja hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo pia waliochangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, nao ni kwanza Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Joyce Machimu, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Fred Tungu, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Elisa Mollel na Mheshimiwa Godfrey Zambi.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Devotha Likokola, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Mariam Kassembe, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Phares Kabuye, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Yono Kevela na Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama. Wote nao tunawashukuru kwa michango yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, tumepata michango katika Idara mbalimbali. Hifadhi ya Chakula cha Taifa imekuwa na wachangiaji watano na mambo waliyohoji ni kiwango kidogo cha hifadhi ya Taifa ya Chakula na uzalishaji wa *SGR* katika ngazi ya Mikoa na Wilaya ununuaji wetu katika ngazi hizo. Ningependa kutoa maelezo kwamba, hifadhi ya chakula, inao uwezo wa kuhifadhi kwenye maghala tani 241,000, lakini ili kujaza maghala hayo na kuweza kuyatunza mazao hayo katika hifadhi ya chakula, tunahitaji kiwango cha shilingi bilioni 72. Hiyo ni kuhifadhi.

Kwa hiyo, napenda ifahamike na Waheshimiwa Wabunge kwamba, jambo hili la kuhifadhi chakula ni la gharama kubwa sana. Kwa hiyo, kiwango ambacho tunanunua na kukihifadhi kinakuwa ni kile ambacho tunaweza kukimudu katika bajeti yetu kila mwaka. Sheria inatutaka tufikie tani 150,000, lakini mpaka sasa tunafikia zaidi kidogo ya tani laki moja. Kwa hiyo, wingi mkubwa ambao ungefaa zaidi ni kule kuwepo kwa fedha katika bajeti.

Idara ya Maendeleo ya Mazao imekuwa na wachangiaji 35. Nikisema nawataja wote wenzangu wamewataja baadhi yao. Lakini mambo waliyohoji ni huduma za ugani, ruzuku ya mbolea, kuwepo kwa kiwanda cha Mbolea nchini, umuhimu wa mbegu bora, kukuza kwa mazao ya biashara, pamoja na kuomba tutoe maelezo zaidi, kuhusu mazao

mapya ambayo tunayahimiza. Idara ya Utafiti imekuwa na wachangiaji watano waliohitaji tuyafafanue, ni matokeo ya utafiti kuwafikia wakulima kwa ufasaha zaidi na pia Mheshimiwa Bujiku Sakila, alitueleza hapa kuhusu ugonjwa wa zao la dengu kule Kwimba. Kwa sababu hili ni jambo kubwa, ningependa nitoe maelezo kwamba, Wizara imekwishabaini kuwepo kwa tatizo hili la ugonjwa huo, sio tu Wilayani Kwimba, bali karibu maeneo yote yanayolima zao hilo yaliyomo katika mikoa ya Shinyanga, Tabora, Singida na Dodoma. Kituo cha Utafiti cha Ukiliguru, kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mazao ya Nchi Kame, iliyoko India, kinatathmini aina bora zaidi za mbegu zenye ukinzani dhidi ya ugonjwa huu na kadri tunavyoikuza mbegu hiyo, ndivyo tutakavyojaribu kuisambaza iwafikie wakulima.

Idara ya Usalama wa Chakula imekuwa na wachangiaji 17, nao walichohoji sana ni bei kubwa za chakula. Napenda kulifahamisha Bunge kwamb, kwa kuwa tuko katika soko huria, bei hizi hazisimamiwi na Serikali. Jitihada ya Serikali ni kuliwezesha soko huria, lifanye kazi yake vizuri na kutangaza. Vyombo vya Serikali, tunatangaza bei katika maeneo mbalimbali. Kama alivyoeleza Naibu Waziri jana ni kwamba, sasa unaweza ukapiga kwenye simu ya *VODACOM*, namba 155 ukapeleka neno “MAZAO” ukaweza kuletewa bei za mazao katika maeneo mbalimbali. Yote hiyo ni kujaribu kulisaidia soko huria liweze kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, wapo waliochangia kuhusu Mfuko wa Pembejeo. Tumesema katika bajeti kwamba, Mfuko huu wa Pembejeo, tumeendelea kuupangia fedha. Yako matatizo mbalimbali ya usimamiaji na kama alivyosema Naibu Waziri, tutajitahidi kuendelea kuyasimamia kwa kadri matatizo hayo yanavyotufikia. Lakini na sisi tunalo tatizo la kukusanya, kuna baadhi ya wakopaji ambao wamechukua fedha, lakini hawalipi kwa utaratibu unaotakiwa. Kama nilivyosema katika hotuba yangu hapa, tutachukua hatua maalum mwaka huu na fedha badala ya kutengwa shilingi bilioni tano, kama mwaka 2005, zimetengwa shilingi bilioni tatu na zaidi kidogo mwaka huu. Ili pia tuweke juhudi kubwa zaidi kukusanya zile ambazo bado ziko na wale waliokopa. Nachukua nafasi hii, kumwomba kila anayedaiwa, asisubiri hatua kali ambazo tutalazimika kuchukua ikiwa ni pamoja na kukamata dhamana walizozitoa na kuzipiga mnada kama inavyostahili kwa yeyote ambaye halipi fedha aliyokopeshwa.

Mheshimwa Spika, mambo yanayohusu Idara ya Sera na Mipango nayo yamechangiwa na wachangiaji 17, muda hauruhusu kuweza kuwataja. Pamekuwa na uchangiaji pia kuhusu Sera ya ubinafsishaji, ama hatua ambayo imechukuliwa na Serikali kubinafsisha mashamba ya Mbarali, ambayo imechangiwa na Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, akiungwa mkono na Wabunge wengine, hususan Mheshimiwa Aloyce Kimaro, aliunga mkono kwa nguvu sana. Nijipe nafasi ya kutosha kidogo, kutoa maelezo kuhusu jambo hili ili liweze kueleweka. Kwanza, liweze kueleweka na Mheshimwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, kwa sababu yeye linamhusu moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu shamba hili, maelezo yake ni yafuatayo: Kwanza, napenda tukumbushane tu kuwa Ubinafsishaji ni Sera ya CCM. Ni Sera ambayo tunayo na iko katika Ilani yetu na iko katika mwelekeo wa Sera za CCM tangu

miaka ya 1990 mpaka miaka 2000 – 2010. La pili, kuhamasisha na kusukuma kwa maana ya ku-*promote* mashamba makubwa ya kilimo, nayo ni Sera ya CCM. Ilani ya CCM ya mwaka 2005 kifungu cha 31 (m) cha Ilani na ningependa kukinukuu kinasema: "CCM itazitaka Serikali kuongeza msukumo katika kuvutia uwekezaji katika mashamba makubwa ya kilimo cha biashara. Hii ni *assignment* maalum kwa Serikali ya Awamu ya Nne, kwa sababu ndiyo inayotekeleza Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2005. Pamoja na kusema kwamba, hii ni sera sahihi ya CCM, ambayo tunaitekeleza, napenda niseme hoja za Mheshimiwa Estherina Kilasi ni nzito na amezieleza kwa ufasaha na haiwezi ikatosha tu niseme liko katika Ilani.

Kwa hiyo, napenda nitoe maelezo kwa upana zaidi na nikiri kwamba, aliyoyasema hapa Bungeni ni wajibu wake kuyasema kama Mbunge. Kwa sababu kazi moja ya Mbunge ni kuangalia matatizo au mabadiliko yanayowagusa watu wake na hasa pale watu wanapodhani yatawaathiri. Lakini ninaamini kwa maelezo nitakayoyatoa hapa, Mheshimiwa Kilasi pamoja na wananchi wa Mbarali, wataelewa ninachosema.

Mashamba haya ya Mbarali na Kapunga, Serikali imeamua yabinafsishwe kwa sababu kubinafsishwa kama ambavyo Mheshimiwa Kilasi ameniambia, si lazima ubinafsishe kwa mtu mkubwa ama kwa mwekezaji mkubwa. Unaweza ukabinafsisha hata kwa wawekezaji wadogo. Kwa hiyo, napenda nitoe maelezo kwa nini yamebinafsishwa kwa wawekezaji wakubwa. Sababu ya kwanza, mashamba haya tangu yalipoanzishwa yalianzishwa kama mashamba makubwa yaliyojengewa miundombinu ya mashamba makubwa, yaani ile *layout* ya mashamba kwa ajili ya *irrigation* ni ya *large scale farming*. Hiyo sababu ya kwanza. Ya pili, haki ya kutumia maji ile *Water Right* ni ya shamba kubwa kwa utaratibu ambapo mwenye shamba akimwagilia yale maji yakitumika mashambani, yale yanayobaki yanatakiwa yarudishwe kwenye mto.

Kwa hiyo, kuna mifereji ambayo inatakiwa itunzwe, maji yarudi kule mtoni. Lakini walipoingia kulima hawa wakulima wadogo ambao walikodishwa na *PSRC* katika kipindi hiki ambacho yalikuwa hayajabinafsishwa, ile mifereji ikawa haitunzwi na badala yake ikawa inatengenezwa mifereji mingine ya kwenda mbele zaidi bila ya kutekeleza ule utaratibu wa kurejesha maji. Hii imechangia kwenye kuathiri kuwepo kwa maji katika Bwawa la Mtera. Inatakiwa maji yatumike kama yalivyokusudiwa katika *Water Right* na utumiaji huu unaweza ukafanywa vizuri na mwekezaji wa shamba kubwa.

Mheshimiwa Spika, sababu ya tatu, katika mashamba haya kuna viwanda vya kukoboa mpunga. Kwa hiyo, mashamba haya si kwamba ni mashamba tu ya *scale farming*, napenda ifahamike kwamba, mashamba haya pia ni *agro-industry*, ni *food processing industry,* kwa maana ya kwamba, pana vinu vya kukoboa kutoka mpunga tuweze kupata mchele. Huduma hii sio kwa ajili ya shamba lenyewe tu, uwekezaji ulioko katika viwanda hivi ni ili na wakulima jirani nao wapate soko la kuuza kwenye viwanda. Naamini kabisa mimi ni mwenyeji wa eneo hilo, napita Mbarali mara nyingi nikienda Mbeya na maeneo mengine, wakati wa msimu utakuta wananchi wanauza mpunga pale na mchele kwa bei za chini mno, kwa sababu wanategemea soko la wale wanaopita. Lakini kwa kuwepo viwanda hivi watategemea soko la kuuza kwenye viwanda.

Sababu ya nne, Shamba la Mbarali mpango wa Mwekezaji ambao aliuleta mbele ya Serikali ni pamoja na asilimia 50 mpaka asilimia 70 ya eneo la shamba lile kulimwa na wakulima wadogo kwa mkataba, yaani ndani ya shamba, liko eneo lisilo chini ya asilimia 50, ambalo litalimwa na wakulima wadogo kwa mkataba na yule mwenye shamba. Kwa hiyo, sehemu ya wakulima ambao Mheshimiwa Estherina Kilasi anawaelezea, ambao wanalima mle, watabakia kulima mle kwa mkataba maalum wa mwenye shamba, yaani kwa utaratibu wa *contract growing.* Naamini hii ni kwa faida ya wakulima na wananchi wa Wilaya ya Mbarali.

Huyu mwenye shamba chini ya mpango wake na kwa utaratibu wa mipango hii ya *privatisation*, ule mpango anaouleta mwekezaji unatazamiwa kwamba, unatekelezwa kama ulivyoletwa na akikiuka kuna hatua zinazotakiwa kuchukuliwa. Atatoa kwa wakulima hawa walio ndani ya shamba huduma zifuatazo; huduma ya matrekta, huduma nzima ya *mechanisation* tangu kulima mpaka kuvuna kwa *combine harvesters*, atatoa pembejeo kwa mkopo, atatoa maji na atotoa soko la uhakika, kwa sababu unalima kwa mkataba kwa hiyo, kile mlichokubaliana mavuno yale ananunua yeye mwenyewe. Sasa unaweza ukasema atatoaje huduma ya maji mbona huduma ya maji ipo. Ukweli ni kwamba, huduma ya maji pale imefifia sana, inahitaji kuboreshwa. Lakini huyu kwa sababu pia atakuwa na *nuclears estate*, atakarabati ile *system* nzima ya maji na hii itakuwa faida pia kwa wale wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika, Shamba la Kapunga lina eneo pia la wakulima wadogo. Tangu ule Mradi wa Kapunga ulivyoandaliwa, kuna eneo la heka 800 kwa ajili ya wakulima wadogo. Leo hii hilo eneo la eka 800, nalo halihudumiwi vizuri kwa sababu ya kufifia kwa miundombinu pale. Shamba hili lina eka 3,000, ambazo ni za yule mkulima mkubwa, lakini zipo eka 800. Katika mpango wa muda wa kati, Wizara imekwishafanya utafiti wa kujenga bwawa lingine katika eneo linaloitwa Salimwani. Likijengwa hili Bwawa la Salimwani, kwa *irrigation* ya Kapunga ya wakulima wadogo, zitaongezeka sekta nyingine 3,500. Naomba Mheshimiwa Mbunge wa Mbarali, binamu yangu, Mheshimiwa Estherina Kilasi, aelewe kabisa, nasema binamu yangu kwa ukweli wa kihistoria. Kwa sababu tangu wakati wa Mtwa Mkwawa na Mtwa Merere wa Usangu, walivyowekeana mkataba wakati baba Mtwa Mkwawa, Mtwa Mwinyigumba, alimwoza binti yake Kilemaganga kwa Mtwa wa Usangu, tukawa na uhusiano wa kihistoria wa namna hiyo, ndiyo maana tunaitana binamu.

Napenda kumhakikishia pia kwamba, katika mpango wa mwaka huu wa maeneo yafuatayo yaliyo katika eneo hilo hilo la Mbarali na nikiyataja Mheshimiwa Mbunge atanielewa zaidi; *Irrigation* ya Ruwanyo ambayo inatekelezwa mwaka huu, pana eka 500; Utulo pana eka 700, Gwiri pana eka 500 na Tungamalenga pana eka 250. Jumla hizo ni eka 1,950, ambazo wale watakaokosa kilimo cha mkataba na hao wawekezaji niliowataja na zile eka 800, bado wanaweza kwenda katika maeneo haya ninayoyaeleza, ambayo yako katika bajeti hii. Isitoshe katika katika muda wa kati, Bonde la Usangu eka 6,700, Idodi eka 800 na Isenge eka 300, jumla ni eka 7,800. Ukichanganya na Madibira ambayo iko mbali kidogo na Mbarali, lakini ndani ya Wilaya hiyo hiyo ya Mbarali, ule Mradi wa Madibira ambao umekwisha kamilishwa *design* na kila kitu na tumeshauombea fedha kutoka *Millennium Challenge Corporation,* utaongeza ekta za *irrigation* pale

Madibira kwa mtindo wa *small scale irrigation* eka 3,600. Kwa hiyo, jumla tunazungumzia eka 10,400. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mimi niko tayari kabisa, mara baada ya kikao hiki, kushirikiana naye, kutembelea maeneo haya, kuiona hii miradi ili kuhakikisha inatekelezwa na pia kusaidia kuwaeleza wananchi, waelewe kwamba, Serikali iko *serious* na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naona muda unakimbia, ziko hoja nyingine kadhaa ambazo zimezungumzwa hapa, ambazo naona zinastahili majibu. Mheshimiwa Vita Kawawa, alizungumzia hii miradi tuliyoieleza katika Kiambatanisho Na. 6 cha Hotuba ya Bajeti. *PADEP, ASPS, DASP,* alielekea kusema kiungwana sana kwamba, mbona inakwenda maeneo mengine na maeneo mengine miradi hii haipo. Napenda kumhakikishia kwamba, miradi yote hii iliyosimama peke yake, hizi *stand alone projects,*ambazo nyingi zimeanzishwa katika maeneo kwa misukumo ya wahisani fulani Fulani, itaingizwa katika *ASDP,* itakuwa ni sehemu ya programu. Kule hizo ndizo zitakuwa vianzio vya ile mipango ya killimo ya Wilaya. Sasa zile Wilaya ambazo hazikuwa na wajomba, hizi ndio moja kwa moja Wizara itashirikiana na Mikoa na Wilaya hizo, kutengeneza ile mipango ya Wilaya. Ndiyo maana katika mafungu ya *ASDP* niliyoyaeleza katika ukurasa wa 43 na 44, ukiangalia kwa makini, kuna mafungu ya fedha kwa ajili ya *grand* ya kuzisaidia Wilaya, kuandaa hiyo mipango. *Focus* yetu ya kwanza, itakuwa ni Wizara kwenda kwenye Wilaya zile zisizo na wajomba ili tufikie mahali kila Wilaya iwe na mpango wake wa maendeleo ya kilimo wa Wilaya, unaochota fedha kutoka kwenye lile kapu la Kitaifa chini ya *ASDP*. Kwa hiyo, naomba kabisa kusiwe na wasiwasi juu ya jambo hilo.

Kuhusu kilimo cha matrekta, *irrigation* na huduma za ugani, naomba Waheshimiwa Wabunge, waangalie sana zile *bullets* nilizoziweka katika ukurasa wa 43. *Bullet* namba mbili ukurasa wa 43, inazungumzia miradi ya kuendeleza kilimo. Chini ya fungu hili Wilaya inaweza kutengeneza mpango wake wa *mechanisation,* ukapewa fedha kutoka kwenye *ASDP Basket Fund*. Kwa hiyo, ni suala la kuibua ile miradi ambayo Wilaya na wakulima pale kwao wanaridhika, iingizwe kwenye mpango na fedha zitapatikana kutoka kwenye lile fuko la Kitaifa. Hali kadhalika huduma za ugani, ambazo zimeuliziwa na wengi hapa katika Bunge hili, nazo tumezipangia fedha, mkiangalia katika *bullets* hizo ni kuimarisha huduma za ugani.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja imetolewa hapa kuhusu makato ya shilingi tano kwa kilo, ambayo wajukuu zangu, Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa John Shibuda, wakagongana kidogo hapa. Inawezekana kwamba, wale wazee waliotangulia kule waliona mnataka kuleta makombora mengi mno kwa babu, yenu ikabidi yafanywe maarifa mgongane hapa hapa. Lakini mimi ninachotaka kusema ni kwamba, hizi shilingi tano tunaposema sasa zisikatwe kwa ajili ya elimu, hatusemi Mifuko ya Maendeleo ya Elimu isiwepo hata kidogo. Tunachosema ni kwamba, tuondoe vitu ambavyo vinamfanya mkulima asiwe na *incentive.* Ukisema shilingi tano inaonekana ni ndogo sana, lakini elewa kilo 100 maana yake ni shilingi 500, anayeuza kilo 1,000 maana yake ni shilingi 5,000. Nenda kwa anayeuza kilo 1,000,000 mara shilingi tano ni shilingi 5,000,000. Wapo wakulima ambao wameanza, wengine ni wafanyabiashara wanasema

nikalime pamba, anakwenda analima pamba anauza kilo 1,000,000 unamkata shilingi 5,000,000, anahama kwenye pamba anarudi kwenye kufanya biashara yake kule.

Mheshimiwa Spika, tunataka walime, kwa hiyo, tunachotaka kuondoa ni *disincentives*, zinazozuia kilimo. Mifuko iendelee na kama kuna *fund raising* zozote, tutashirikiana kama sisi wenzenu tunavyofanya katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie hizi dakika chache za mwisho, nizungumzie kidogo kuhusu hoja niliyoona kama ina hoji uwezo wangu wa kujiamini kwa jukumu la kuwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Niliwasikia waliochangia hoja hii, inawezekana si kwa maneno hayo, lakini nilivyowaelewa mimi kama Mbunge mwenzao, niliona kama wanahoji hivyo. Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Juma Suleiman Nh'unga, anasema nilishindwa kidogo jambo fulani. Yalizungumzwa maneno hapa, rekodi ya kutofanikiwa hapa na pale. Mheshimiwa Mwambalaswa anesema, angekuwa yeye angekataa, lakini mimi napenda niseme kwamba, wote humu ndani ya Bunge, wote hawa wawili ni wanatimu wenzangu na timu yetu ni moja ya CCM hapa Bungeni. *(Makofi)*

Sasa pengine, nitoe mfano wa timu ya mpira labda Simba, kuna mwingine anasema nimevaa kuelekea huko. Kwa mfano, Simba, umejiunga na timu ya Simba mnafanya mafunzo kama ni *trotting* wote mko kwenye *trotting*, wanatimu wote hakuna anayebaki, mnafanya *trotting* na mafunzo. Lakini siku ya mechi, kuna *Team Manager*, Mwalimu na *Captain*, wanakaa pamoja na kusema wale kumi na moja wavae jezi. Sasa unaweza ukachukuliwa. Mungai vaa jezi, Mwambalaswa vaa jezi, lakini ukisema unakataa, wenzako watakushangaa. Maana katika *trotting* ulikuwepo na mimi nasema hapa Wabunge wote sisi Mawaziri ni timu inayotoka Bungeni kwenye Chama cha Mapinduzi kilichopata ushindi. *(Makofi)*

Tumeingia, tumeshinda, tumekuwa timu moja, sasa Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakapanga wale wa kuvaa jezi waende kucheza mechi, siku hiyo imetokea na mimi nimo humo. Nikikataa wewe, umekwishapangiwa umekuwepo kwenye *trotting*, umo kwenye timu, ukikataa shauri yako, maana walioko kwenye *trotting* ni wengi atachukuliwa mwingine. Halafu uelewe kwamba, la kwanza hilo ukikataa shauri yako atachukuliwa mwingine, lakini lipo la pili, ole wako kwa wapiga kura. Wapiga kura wamekuleta hapa uingie kwenye hii timu, wanasikia Mheshimiwa Mwambalaswa umeteuliwa kuwa Waziri umekataa, hamtaelewana na wananchi, mimi nina hakika. Tena hata ikitokea uvumi tu kwamba, kuna fulani anataka kutoka kwenye Baraza, *trotting* huwa unaona zimekwisha anza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna wanaohoji nimefanikiwa wapi? Mimi nasema wanaosema sijafanikiwa, waseme sikufanikiwa wapi. Mimi nimekuwa Waziri wa Elimu hapa, kifungu cha 60 cha Ilani hii, kwa ruksa yako napenda kukinukuu, kinasema hivi: Baada ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa MMEM, CCM katika kipindi cha 2005, kitazielekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-

Mafanikio ya MMEM, Waziri aliyesimamia MMEM ni mimi hapa leo naomba niseme kabisa. Pale Dar es Salaam, vijana wengine pale mjini, ilikuwa wakiniona naweza nikawa nakwenda tu dukani, walikuwa wananiita Mzee wa MMEM. Nimefanya ratiba Chunya kuhimiza Elimu ya Msingi Chunya mpaka Makongorosi nimefika, mpaka kwenye lile gereza la mbali kabisa nimefika. Kwa hiyo, nilipoteuliwa kuwa Waziri, watoto wa miaka saba mpaka miaka 13, waliokuwa shuleni ni asilimia 58 tu. Maana yake asilimia 42 ilikuwa nje ya shule. Nilipoondoka mwaka 2005, niliacha shuleni asilimia 95; huko ni kushindwa huko?

Mheshimiwa Spika, mwaka 2000, sio tu kwamba, watoto walikwenda shuleni, waliofaulu mtihani wa darasa la saba kwa mwaka huo ilikuwa ni asilimia 20. Mwaka 2005, mwaka wangu wa mwisho mimi kuwa Waziri wa Elimu, walifaulu asilimia 62. Huko ni kushindwa huko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba radhi kujipigia tarumbeta, lakini yuko Mzungu mmoja aliniambia nilipokuwa kijana, kule *Tanzania Elimu Supplies*, wakati tukiandika *annual report*, nilikuwa naona sifa nyingi. Aliniambia kwa Kiingereza, tafsiri yake anasema: "Sikiliza kama umenunua tarumbeta, halafu ukaenda ukaliweka stoo hulipulizi pulizi, ukija kuchukua linapata kutu." Kwa hiyo, ndiyo maana na mimi nimeamua nijipigie tarumbeta kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, waliohoji kwamba; je, najiamini? Napenda kuwahakikishia kabisa kwamba, mimi najiamini kabisa, kumudu madaraka niliyopewa na napenda nitoe sababu za kumudu madaraka niliyopewa. Sababu ya kwanza, ninayo dira, dira ni Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Sababu ya pili, Rais ameniamini, wewe Rais amekuamini halafu hujiamini, toka basi. Mimi najiamini, Rais wetu aliyekabidhiwa nchi hii, ameniamini niwe Waziri. Lakini sababu ya tatu, Rais tarehe 18 Januari, 2006, kama nilivyolitaarifu Bunge, kwenye ukurasa wa 48 *paragraph* ya 81, alikuja Wizarani na alitupa maelekezo kinagaubaga, mfanye moja, mbili, tatu, nne na nimeyaorodhesha pale katika zile *bullets* nne. Sasa nina wasiwasi gani wa kutokujiamini, dira ipo, maelekezo nimekwisha pewa na Mheshimiwa Rais, sina wasiwasi hata kidogo. Lakini, pia ninayo timu nzuri ya wataalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie, ilikuwepo hoja imeulizwa hapa kuhusu *SACCOS*. Imeulizwa na Mwenyekiti wetu na ni *very senor MP*, kutokulijibu sio vizuri, Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba, wao wangependa kule Ruvuma *SACCOS* wawe ndiyo wakala. Mimi napenda kusema kabisa, sisi Wizara tunasikiliza mawakala waliopendekezwa na Wilaya na Mikoa. Kwa hiyo, kwa *SACCOS* pale inapooneka inaweza kuwa wakala wa mbolea, ni ruksa kabisa, bila wasi wasi wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kuwashukuru tena, wote waliochangia na wote ambao wanatutia moyo, tuweze kutekeleza madaraka haya na wajibu tuliopewa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na kuungwa mkono, haiwezi kupitishwa hadi tuingie katika Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, ninapowahoji sasa sio kwa kingine, sio kupitisha makadirio, nawahoji katika hatua hii ili tuingie katika Kamati ya Matumizi, kwa sababu ni hatua muhimu ya utaratibu

Kwa hiyo, sasa muiamue hoja hiyo.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika**

Kif. 1001- *Administration and General* … ….. Sh. 5,810,669,100/=

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *program* ya 10, *sub-vote* 1001, kasma 250100, naomba tu maelezo, wakati wa *briefing* Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, alitoa hali ya chakula katika nchi yetu na katika majedwali ambayo aliyatoa kuhusu hali ya chakula, Mkoa wa Dodoma, Wilaya ya Kondoa, haikuwemo kwenye majedwali hayo. Nilishauri kwamba, iwemo kwa sababu kuna maeneo ya Tarafa mbili, ambayo yana upungufu mkubwa wa chakula. Niliomba watalaam watumwe katika Tarafa hizo za Farkwa na Kwamtoro katika Jimbo la Kondoa Kusini, waweze kufanya tathmini upya, tuweze kuona hali halisi ya chakula katika mwaka huu wa 2006/2007.

Nashangaa kwamba, tangu wakati ule, katika hotuba yake pia ametoa jedwali ambalo linafanana na lile lile lililoko ukurasa wa 97, ambalo linaonyesha upungufu na upungufu ni ule ule. Ni dhahiri kwamba, Waziri hakupeleka wataalam katika eneo hilo, kufanya tathmini. Napenda nimkumbushe Waziri kwamba, hata msimu wa 2005/2006, jambo hili limejitokeza na nilitoa taarifa kwamba, wataalam wapelekwe maeneo haya lakini hawakupelekwa mpaka dakika za mwisho na wananchi waliathirika sana. Sasa naomba nipate maelezo kwamba; je, Waziri yuko tayari kutekeleza ombi langu la kupeleka wataalam wafanye tathmini katika Tarafa mbili tu za Farkwa na Kwamtoro na hasa katika Kata za Mpendo, Sanzawa Makorongo, Farkwa na Gwandi? Naomba maelezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, sijui kama umelipata vizuri, Mheshimiwa Paschal Degera, anaulizia tathmini ya kuona kama hali ya chakula ndiyo inayotakiwa.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo kwamba, kuna upungufu mkubwa katika maeneo hayo ambayo katika taarifa ya Wizara, inasema hakuna upungufu. Sasa mimi kama Mbunge, najua tatizo lipo.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Paschal Degera kwamba, kama ameangalia vizuri kwanza, namwomba radhi kama kuna kitu nilichomwahidi halafu hatukukitekeleza, inabidi nichunguze nini kilitokea. Napenda kumhakikishia kwamba, katika tathmini ambayo nimetoa ripoti, siwezi kukumbuka katika *paragraph* ipi, lakini nimesema tathmini ya uhakika inafanywa mwezi Julai, maana yake ni mwezi huu. Kwa hiyo, namwomba yale yaliyopita tusameheane, tathmini inafanywa *up-dated* mwezi huu, kujua hali ilivyo katika kila Wilaya nchi nzima. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nyingine tena na namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri. Sasa naomba kwamba, pindi watakapofanya tathmini na mimi wanishirikishe ili niweze kuwapeleka kwenye maeneo ambayo yanahusika. Asante.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri, unaukubali mwaliko huo?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haina *problem*, ingawa nilitaka kumweleza Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli si kazi ya Mbunge, kwa sababu kuna watu ambao huwa wanaifanya hii kazi. Kwa vile ameomba ombi maalum, labda ana wasiwasi fulani, nitawaelekeza wanatathmini wanaotoka Wizarani kwamba, wawasiliane na Mheshimiwa Mbunge, kama atakuwepo pale Wilayani.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *program* 10, *sub-vote* 1001, kifungu 250100, napenda kujua kuhusu hatima ya vyuo vya kilimo hapa nchini. Kwa sababu nililizungumzia wakati wa kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha, akasema kwamba, sasa hivi tunataka kuendeleza kilimo kwa nguvu zote na tunahitaji watalaam wengi sana. Lakini sina hakika, vyuo hivi Mheshimiwa Waziri hakunijibu kwamba, viko katika hali gani na kama bado vinaendelea kutoa wataalam; je, vimepangiwa fungu lolote kwa ajili ya kuendeleza vyuo hivyo au hakuna? Kama havikupangiwa naomba nipate maelezo.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mbunge, kwa swali ambalo ameuliza juu ya hatima ya vyuo vya mafunzo. Akiangalia katika hotuba yangu ya bajeti ukurasa wa 44, pale kwenye gharama za utekelezaji katika ngazi ya Taifa, *bullet* ya kwanza ni kuboresha huduma za ugani na utafiti. Sasa katika kuboresha huduma za ugani na utafiti, huwezi ukaboresha huduma za ugani na utafiti mpaka uwe na Maafisa Ugani. Kwa hiyo, fungu hili ambalo limetengwa katika *ASDP* shilingi bilioni 104, asilimia 16.9 ya fungu lile la Kitaifa ndilo la ku-*revamp, research and training* ili kuimarisha huduma za ugani. Kwa hiyo, vyuo sasa hivi vilikuwa vinakwenda wa wastani wa asilimia 25, kuanzia mwaka huu, tunaanza kuviendesha vile vyuo kwa kuvijaza tu *capacity* ili tutoe Maafisa Ugani wa kutosha, tuweze kuwapanga kwenye Wilaya mpaka kwenye ngazi ya Kata na pale inapobidi mpaka ngazi ya vijiji.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kama nitakuwa nimeangalia vibaya, sielewi fedha hizi za vyuo zimewekwa wapi, kwa sababu *sub-vote* ya mbele kabisa ya 1004, kipengele hiki hakijawekewa fedha kabisa; sasa sielewi hizi fedha ziko wapi?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge, aangalie kwenye *sub-vote* 1004, *Agricultural Training Institutes*. Kama anahitaji maelezo zaidi, wataalam wangu wamenisaidia hapa kwamba, Wizara ina vyuo vinane vya mafunzo, vyenye uwezo wa kufundisha wanachuo 800 kwa mwaka na utavikuta kwenye *vote* 3001.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Mlata, nitakupa nafasi kwenye *vote* 3001 kama utakuwa bado una tatizo.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *program* 10, *sub-vote* 1001 kifungu 250100, mshahara wa Waziri. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 17, anasema kuna skimu 63 zenye jumla ya ekta 14,396, ambazo zimekamilika. Sasa ningependa nijue hizi skimu ziko sehemu gain? Halafu ningependa nieelezwe ni vegezo vipi vimetumika kuyachagua maeneo haya?

**MWENYEKITI:** Kabla ya Mheshimiwa Waziri kujibu, nadhani tukubali kwamba, kuna matumizi mabaya sana ya kutumia hiki kifungu kidogo cha 1001. Waheshimiwa Wabunge, nadhani tunafanya kwa kweli uvivu na uzembe, kwa sababu inatulazimisha tukiuke Kanuni. Hayo mengine mnayouliza yako tena mbele na kwa mujibu wa Kanuni ya 54 ni kwamba, tunaanza kuwahisha shughuli ya mbele kabla hatujamaliza ile nyingine. Kwa hiyo, mimi ningeshauri kwa leo tuendelee tu, maana yake nadhani bado ndiyo upya wenyewe. Kila mtu anakaa 1001 halafu anauliza jambo lolote, Kitabu cha Nne, sijui cha ngapi si utaratibu. Najua bado tunajifunza, lakini siku nyingine, Mkutano ujao, nitang'ang'ania uende kwenye *sub-vote* inayohusika, kama hukusoma, huwezi kuendelea na hoja kwenye kifungu chochote unachagua tu. Mshahara wa Waziri, basi unaendelea na mambo mengi kabisa. Mheshimiwa Waziri, kwa leo basi tusaidie.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama nilivyosema wakati natoa *briefing* yangu hapa, skimu zile ni orodha ndefu. Kwa hiyo, hatukupenda kuandika orodha ndefu na nimeahidi kwamba, tutawapatia orodha ya skimu zote, kila mtu ataona zile ambazo zimetekelezwa na zile ambazo tutazitekeleza.

Lakini pia kuhusu kigezo kinachotumika, uibuaji wa hii miradi ni ule ule ambao tumeeleza kwamba, unaanzia Mawilayani, katika mipango ile ya *DADPs* na ndiyo maana nilisema kwamba, Wizara yetu inasaidia wananchi kuibua miradi hiyo, kwa kutumia ile *National Irrigation Master Plan*, ambayo pia nimewaahidi kwamba, wale ambao hawana nitawapatia. Huo ndiyo utaratibu unaotumika kuibua miradi hii.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. La kwanza kabisa, linahusu maelezo ya Waziri, ambayo aliyatoa juu ya shilingi tano, ambayo nakubaliana naye vizuri sana na namshukuru leo amesisitiza kwamba, hazikatwi. Lakini pia kwa kuwa sasa tunafunga hiyo, ni vizuri basi wakulima wakaelezwa katika miaka kwa mfano, kumi zilikatwa ngapi na zilifanya nini, sasa tunafunga akaunti. Lakini kuliacha tu jambo linaelea namna hii, sioni kuwa kama ni umahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, wakati nachangia nilizungumzia juu pembejeo, ametuambia ameweka shilingi bilioni 21 kwa ajili ya pembejeo. Sasa nasema mbona wengine hatutumii mbolea, mbona inavyoonekana kwamba, Serikali inaelekeza kila kitu kwenye mbolea tu, jambo ambalo mimi nimemwambia si vizuri. Kwa sababu kama nchi hii tutaletewa utegemezi wa kemikali za mbolea, watoto wetu wataisha baadaye, hawatakuwa na ardhi ya kulima, hilo nimemwambia. Lakini sasa kwa upande wa wakulima wa pamba, kwa nini basi kama pembejeo upana wake ni pamoja na madawa ya pamba, wakulima wanakatwa shilingi 15 kwa ajili ya dawa, wanakatwa shilingi tano kwa ajili ya utafiti; kwa nini basi katika hiyo shilingi bilioni 21, Waziri akate angalau shilingi 10 kwa kila kilo?

Kwa mwaka 2005, maana yake ni shilingi bilioni nne hizo, ziwe ruzuku kwa ajili ya pembejeo inayoitwa dawa ya pamba. Hilo nataka maelezo, la sivyo tunatoa hapa shilingi bilioni 21, kwa wakulima wachache tu.

La tatu, kila siku naangalia haya mavitabu haya, yananishangaza kwa kutotoa Bungeni maelezo bayana, hizo fedha zinazowekwa kwenye mafungu zinaenda kufanya nini? Nimeangalia hapa katika kitabu kizima hiki nusu ya fedha zote ambayo ni shilingi 39,144,000,000 ni *other goods and services not classified above*, yaani ni vitu ambavyo hatuvijui, vitu ambavyo havijatajwa. Hivi vitu ambavyo havijatajwa vya zaidi ya shilingi bilioni 39 ni vitu gain, ambayo karibu ni nusu ya bajeti yote ya Wizara shilingi bilioni 77, ambayo ni sawa sawa na bilioni 37, ambazo zinatoka nje?

Haya madudu yaliyofichwa fichwa huko ambayo hatuyajui sisi na hayawezi kuorodheshwa, Waheshimiwa Wabunge, wakaweza kuelewa ni madudu gani hayo, Waziri tuambie tujue ni nini, *those unclassified goods and services*, ambazo unasema nyingine ni shilingi bilioni 25, nyingine ni shilingi bilioni saba na nyingine ni shilingi bilioni moja? Kama unataka orodha ninayo hapa kufuatana na kitabu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumpa maelezo Mheshimiwa John M. Cheyo kwamba, shilingi tano ambazo ilikuwa ndiyo makato kwa ajili ya elimu katika miaka mitatu, yaani misimu mitatu ya hivi karibuni, ilikuwa ni jumla ya shilingi bilioni nne, ambazo hazikwenda kwa wakulima, zilikatwa kuelekezwa kwenye Mifuko hiyo. Sasa akitaka kwa miaka zaidi inabidi tupate nafasi ya kuchambua hizi, nazitaja ambazo tulikwisha ziangalia.

Sasa kuhusu ruzuku ya mbolea hii shilingi bilioni 21, ni kwamba, kama nilivyosema, sera imelenga kukuza utumiaji wa mbolea za kemia, kwa sababu mageuzi ya kilimo huletwa na mbolea za kemia. Kwa hiyo, *focus* kubwa imekwenda kwenye mbolea za kemia. Lakini uwezo wa bajeti yetu mwaka huu ilikuwa kututoa toka shilingi bilioni saba mpaka shilingi bilioni 21. Kama tungetaka kufanya yote kwa mbolea, tungehitaji shilingi bilioni 40. Kwa hiyo, imebidi kwa utaratibu wa kupanga ni kuchagua, tuamue kitu muhimu ambacho tunataka kukipa umuhimu wa kwanza ni nini na uamuzi wa Serikali ikawa ni *food security*, uhakika wa chakula. Kwa hiyo, utakuta ruzuku hii imeelekezwa kwanza, kwenye kulihakikishia Taifa letu uhakika wa chakula na ambacho kwa kweli ndiyo kilio cha Wabunge wengi, tusiwe omba omba hata kwa chakula. Sasa kwa maana ya kuendelea na sera hii kwenye maeneo mengine, ndiyo kadri uchumi wetu unavyokua, tutazidi kuendelea kufanya hivyo, tutazidi kuendelea kuongeza kiwango cha *subsidy* kwa kadri tutakavyoamua.

Sasa hivi upande wa pamba, kuna ule utaratibu ambao wadau wenyewe wamejiwekea, ambao Mheshimiwa John Cheyo, ameueleza ule wa shilingi 15 halafu wana-*finance*. Ule utaratibu mimi nisingenda upuuzwe. Nilikwenda kukaa kwenye kikao pale Mwanza na wadau wote wa pamba na *overwhelmingly* kabisa, walisema walipenda uendelee kwa sababu ni mkato inabidi Waziri *approve* na niliwauliza bado mnataka kuendelea na utaratibu huu, wakasema ndio tunataka kuendelea nao. Nikawaambia hata mimi maoni yangu muendelee nao, kwa sababu ndio imewatoa kutoka kwenye marobota 350,000 mpaka mmefikia marobota 695,000. Kwa hiyo, niwapongeze sana wadau wa pamba, kwa uamuzi wao kwa sababu unaleta matokeo. Sasa hiki kipengele kingine alichoulizia, zile ambazo zimekuwa *unclassified*, nimeambiwa huu ni mfumo wa *GSF Budget Classification*, ambazo zinatumika zote zinahuisha fedha ambazo sehemu kubwa zinatolewa na taasisi, yaani *subvention* zilizo chini ya Wizara. Zimewekwa pale ili kuja kuchangiwa kwenye *projects* hususan maeneo ambayo kuna fedha za kutoka nje ili programu zetu ziweze ku-*take off*.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni yetu wote, hatuwezi kuchangia shilingi bilioni ishirini na moja za walipa kodi, halafu zote zikaelekezwa Mikoa minne inayolima mahindi. Sisi tunaposema tunalima pamba, maana yake hatulimi kwa nguvu hiyo hiyo mpunga au mahindi, kwa hiyo, kuna *opportunity cost*. Sasa Serikali kwa sababu tumechangia, inatuacha tuendelee kuchangia, kwa nini tusipewe na sisi hela ambayo inaweza kutusaidia?

**SPIKA:** Mheshimiwa keti chini. Waheshimiwa Wabunge, nataka kufafanua. Kwa mujibu wa kanuni zetu, hatua ya Kamati ya Matumizi ni kupata maelezo. Suala hapa sio kwamba, Sera imridhishe mtu, suala hapa ni kwamba, maelezo yanatosheleza yakishakuwa hivyo, hata kama hayakufurahishi, ndio maelezo ya Serikali. Hatukai hapa mpaka kila mtu aridhike kwenye Kamati au hela zitahamishwa kuwe na tegemeo zitatoka zao moja kwenda jingine. Unapata maelezo ya kile ambacho Serikali imetenga na kwa hakika kama ni wa Upinzani, pengine hata hukubaliani na hiyo Sera, sasa huwezi kuibadili kwa kutumia Kamati. Kwa hiyo,Waheshimiwa tunaendelea na tahadhari ni hiyo. Sio kwamba, hapa tunadai tupate kile tulichoshindwa kwenye hoja, hapa tunataka maelezo ya Serikali kwa mantiki waliyotumia wao.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu 1001, kifungu kidogo 250100, mshahara wa Waziri. Nilichangia kwa maandishi, lakini bahati mbaya Mheshimiwa Waziri sijui ni kwa nini hakupata nafasi ya kunijibu na nilikuwa nimeuliza vitu ambavyo angenijibu, nisingekuwa na sababu ya kuweza kusimama. Kwanza, katika hotuba yake ukurasa wa 41, anasema kwamba, tumeanza kutekeleza *agricultural sector development program* mwaka 2002/2003, kwa hiyo, sasa hivi tayari tuna miaka takriban mitano, kutekeleza programu ambayo ilikuwa ni ya miaka saba, ambayo ilikuwa ni ya jumla ya shilingi trilioni mbili nukta moja. Lakini wakati huo huo katika ukurasa wake wa 45, Mheshimiwa Waziri anasema tena kwamba, mwaka huu wa 2006/2007, ndio tunaanza kutekeleza hiyo programu. Naomba afafanue ni makosa tu ya uchapishaji au ni *by design*?

Pili, katika hali hiyo hiyo, kwa wastani wa shilingi trilioni 2.1 kila mwaka, inabidi zitengwe jumla ya shilingi bilioni 343, lakini mwaka huu umetenga shilingi bilioni 45 kwa mujibu wa hotuba. Ukienda kuhesabu zile *vote* za *ASDP* ni shilingi bilioni 23 tu. Kwa hiyo, shilingi bilioni 22 haziko *budgeted,* naomba nipate maelezo hizi hela ziko wapi na zinafanya nini?

Mwisho kabisa, kwa mujibu wa Ilani ya CCM, ambayo Mheshimiwa Waziri ameionyesha, ukurasa wa 22, inatakiwa kuanzia sasa, Serikali iweze kuweka utaratibu wa mashindano ya Wilaya na Mikoa kuzalisha na kupewa zawadi au vivutio. Lakini katika hotuba yake yote, nimejaribu kuangalia hicho kitu hakipo kabisa. Napenda Mheshimiwa Waziri, anipe maelezo anaitekeleza Ilani ya CCM nusu nusu au ana Ilani ya CHADEMA chini ambayo anaitekeleza, ambayo haina hilo?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uandaaji wa programu ulianza mwaka 2002 na nimesema kwenye Hotuba ya Bajeti, utekelezaji wa programu iliyokwisha kamilika, programu nzima, ndio tunaanza na bajeti hii. Sasa unapoandaa programu, huandai ukakaa ile *component* ya programu ambayo imekwishakamilishwa unaanza kuitekeleza kwa hiyo kuna *components* nyingine ziko kwenye programu mama lakini zenyewe zilikuwa tayari kuanza hizo ndizo zilizoanza tangu mwaka 2002/2003 na ndizo tumeziorodhesha kwenye jedwali namba sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa wakati nafanya wind-up nikijibu hoja ya Mheshimiwa Zitto kwamba, hizo *stand alone projects* zilizoanza kabla ya *ASDP* nzima kuanza, sasa nazo zitaingizwa kwenye *ASDP Basket Fund*. Kwa hiyo, hatima ya yote tunapoanza bajeti ya mwaka huu vile vi-*stand alone projects* vyote vitaingizwa kwenye hii programu kubwa na wote tutakuwa tunachota katika kapu moja. Lakini pia napenda ieleweke hiyo ambayo amezungumzia Mheshimiwa Zitto kwamba hazioni fedha nyingine kwamba hii *ASDP* ni *sectorial* sio *ministerial*. Kuna Wizara ya Mifugo, Wizara ya TAMISEMI, Maliasili kwa maana ya mambo ya uvuvi na kadhalika, *sector* nzima ya kilimo ipo kwenye programu hii. Kwa hiyo, ili upate picha kamili inabidi pia uangalie mafungu yaliyo katika Wizara nyingine, pia inabidi uangalie mafungu ya *DADPs* ambayo yamepita kwenye Wizara ya TAMISEMI. Kwa hiyo, inabidi utazame zote kwa pamoja.

Mambo haya ya uchambuzi wa ndani, kuweza kujua vizuri, kwa kweli tunayafanya zaidi kwenye ile Kamati ya Kilimo na Ardhi, ambapo kuna nafasi ya kuweza kutoa uchambuzi mkubwa zaidi na tungeweza kutoa picha kamilifu zaidi. Kwa hiyo, napenda Mheshimiwa Zitto na Wabunge wengine, waamini kwamba, Kamati ile ilifanya uchambuzi huo na walipitisha bajeti hii kwa sababu waliridhika na maelezo ambayo tuliwapatia. Kuhusu mashindano, mambo yote yaliyopo katika sera ya CCM, hatuanzi kutekeleza mara moja, tunaanza kwa kufuata umuhimu wa suala moja baada ya jingine. Naelewa mashindano haya katika baadhi ya Wilaya, yameshaanza lakini tutaendelea tena katika Wilaya zile ambazo hazijaanza.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 81(6), sasa ni dakika kumi kabla ya kuahirisha Bunge. Sijapata hoja yoyote chini ya kifungu cha 21(4) cha kuongeza muda wa Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, sasa nitamwita Katibu tupitishe mafungu moja baada ya lingine.

Kif.1002 *Finance and Accounts* ..... ... .... .... .... ..... Sh. 649,166,600/=
Kif.1003 *Policy and Planning* ..... ...... ..... ......... Sh. 1,779,282,400/=
Kif.1004 *Agriculture Training Institutes*. ... ... ..... Sh. 8,239,118,100/=
Kif.2001 *Crop Development* ..... ...... ....... ..... .... Sh.41,620,907,300/=
Kif.2002 *Directorate of Irrigation and Tech. Serv.* ... Sh.44,741,776,000/=
Kif.3001 *Research Development* .... .... ..... ..... ..... Sh.13,010,592,900/=
Kif.4001 *Cooperative Development* .... .... .... ..... Sh. 3,271,540,900/=
Kif.5001 *National Food Security* ..... ..... .... ... ...Sh. 1,034,988,900/=
Kif.5002 *Strategic Grain Reserve* .. .... ...... ... ..... Sh. 6,982,915,200/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Matumizi mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika**

Kif.1001 *Administration and General* .... .... ..... ... Sh. 150,000,000/=
Kif.1003 *Policy and Planning* .. .... .... ..... ..... Sh. 9,201,454,700/=
Kif.2001 *Crop Development* .. .... ... ..... ... Sh.15,582,370,250/=
Kif.2002 *Directorate of Irrigation and Tech. Serv.* ... Sh. 7,281,762,000/=
Kif.3001 *Research Development* ..... .... ... ... ... Sh.12,771,147,050/=
Kif.4001 *Cooperative Development* . ...... .... ... Sh. 450,000,000/=
Kif.5001 *National Food Security* ...... ..... ...... ...... Sh.45,812,449,600/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu, limekaa kama Kamati na kupitisha bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Fungu Na.43 ya mwaka 2006/2007 na kuipitisha bila mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Katibu kuna shughuli yoyote?

**ND. JAPHET SAGASII – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, shughuli zilizokuwa zimepangwa kwa ajili ya kikao cha leo, sasa zimekamilika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa shughuli zilizopangwa kwa kikao cha leo zimekamilika dakika tano kabla ya wakati, namwomba Waziri wa Nchi, kabla sijaahirisha atoe hoja ili tuweze kuahirisha kabla ya wakati.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema, shughuli zilizopangwa leo kwa kuwa zote zimekwisha na bado tuna muda wa dakika kama nne, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liahirishwe sasa mpaka Jumatatu, saa tatu asubuhi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 01.42 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 10 Julai, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*